9 789976 588125

# JARIDA LA TUZO

TOLEO LA 0001 SEPTEMBA 2024



# Mahiri wa Habari

## Uwekezaji wa Kimkakati - PSSSF
Unavyoboresha Mafao ya Pensheni

## Marie Stopes
Inabadilisha maisha

WADHAMINI
PSSSF Public Service Social Security Fund
MARIE STOPES TANZANIA
TAIFA GAS Taifa Gas Tanzania Limited

JARIDA LA

# TUZO

## MAELEZO YA MATUMIZI

| | VIDEO | AUDIO | PHOTO | WEB |
|---|---|---|---|---|
| Bofya kupata | (i) Video | (ii) Sauti | (iii) Picha | (iv} Tovuti |

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# Yaliyomo


Tahariri.....03
Mshindi wa Jumla.....04
Kishindo cha Habari.....08
Je Wajua?.....22
Mahiri wa Habari.....65
Habari zilizogusa Umma.....69
Kumbukizi Gwiji wa Habari.....74
Anayeinukia kwa Umahiri wa Habari.....78
Jicho la Wahariri.....82
Jicho la Majaji.....86
Kifuatacho katika Jarida laTuzo.....91
Usiku wa EJAT katika picha.....92
EJAT 2023 ilivyovunja rekodi zake.....96
Vigezo vya Kumpata Mshindi wa Jumla EJAT.....98
Vigezo vya Kutathmini Habari Shindani.....100
Orodha ya Washindi.....104





Mshindi wa Jumla



Pg. 4

Mahiri wa Habari



Pg.66

Gwiji wa Habari



Pg. 75

Anayeinukia



Pg.79

# TIMU

**Kiongozi:** Ernest Sungura

**Uzalishaji na Uhariri:** Josephat Mwanzi

**Masoko na Usambazaji:** Derek Murusuri

**Uratibu:** Ziada Kilobo

**Picha:** Mwanzo Millinga



9 789976 588125

Kwa mawasiliano: +255 685 089 690


Jarida La Tuzo linamilikiwa na
Baraza la Habari Tanzania (MCT)
House No. KUN/MTN/532,
Tegeta Skansa Area, Bagamoyo Road
P.O. Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 719 494 640 / + 255 767 494 826
Website:http://www.mct.or.tz

mctanzania mediacounciltanzania
mediacounciltanzania mediacounciltanzaniamct

# Tahariri

## Jarida la TUZO kuenzi Umahiri



Ndugu msomaji na mdau wetu mpendwa,
Umahiri ni uwezo wa juu wa kufanya jambo kwa ustadi na ufanisi mkubwa. Ni mchanganyiko wa maarifa, ujuzi na uzoefu ambao humwezesha mtu kutekeleza majukumu au shughuli fulani kwa ubora wa hali ya juu.

Uongozi wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) umeamua kuzindua Jarida la TUZO kuhamasisha umahiri katika sekta mbalimbali nchini Tanzania na nje ya nchi. Katika toleo hili la kwanza la uzinduzi, jarida litaangazia sekta ya habari wakati uongozi ukikamilisha mipango itakayowezesha kuangazia sekta zingine na kuwaibua watu mahiri na umahiri wao katika kilimo, teknolojia, bima, afya, elimu, uhandisi, na kadhalika.

Jarida hili, linatolewa kwa mara ya kwanza kuenzi Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) ambazo zimekuwa zikitolewa kwa miaka 15 mfululizo. Moja ya maudhui katika jarida hili ni habari za kishindo zinazotokana na waandishi wa habari mahiri walioshinda tuzo.

Jarida la Tuzo linabeba maudhui yanayosimulia maisha ya mwandishi mahiri na kilichompa sifa ya umahiri ikiwemo undani wa maisha na mahusiano kazini na nyumbani. Simulizi zinathibitisha ujuzi, maarifa, na uzoefu wa hali ya juu katika tasnia ya habari. Ni simulizi zinazochambua uwezo wa waandishi katika kuchanganua, kutafsiri, na kuripoti habari kwa usahihi na uadilifu.

Simulizi hizi zinaangazia kina cha maarifa kuhusu mada zilizofanyiwa kazi na kushinda tuzo. Zinadhihirisha uandishi wa kiufundi unaotumia lugha sahihi kwa mtindo unaovutia na kuelimisha. Pia, zinathibitisha uwezo wa waandishi kuchunguza kwa kina, kuhoji vyanzo, na kutathmini uhalali wa taarifa kabla ya kuziripoti.

Utashuhudia juhudi za umahiri wa habari katika ubunifu na uvumbuzi wenye namna mpya za kuwasilisha habari au kuhusisha hadhira kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko.

Mbali na simulizi za watu mahiri katika sekta mbalimbali na kishindo cha kazi zao katika jamii, Jarida la TUZO litakuwa likiibua mchango wa taasisi na makampuni mbalimbali katika kuleta maendeleo na mabadiliko katika maisha ya watu. Jarida litawaenzi wanaostahili kuenziwa kutokana na mchango wao mkubwa katika kukuza sekta zao. Aidha, Jarida litawaibua vijana wanaoinukia katika umahiri wa sekta zao husika kwa kudhihirisha weledi, uadilifu, ubunifu, uvumbuzi na maono waliyo nayo katika sekta.

Uongozi wa Jarida la TUZO utalisambaza jarida hilo bila malipo na kuwafikia watu wa kada zote kupitia njia za kidigiti na nakala ngumu zitakazopatikana katika njia za usafiri hususan wa treni ya kisasa, ndege na katika maduka makubwa mijini.

Jarida litakuwa likipatikana pia katika kila tukio la maonesho ya sekta mbalimbali popote Tanzania na nje ya nchi na wakati wa maadhimisho ya kitaifa na kimataifa. Kwa mfano, wakati wa maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Mei Mosi, Siku ya Vijana, Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, na kadhalika.

Karibu ufuatilie mwanzo na mwendelezo wa maudhui kwa kila toleo la Jarida la TUZO litakalokuwa likitoka kila baada ya miezi miwili.

**Ernest Samson Sungura**
Kiongozi Mkuu wa Timu ya Jarida la TUZO

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

**Mshindi**
wa Jumla

**Kwa mara ya kwanza toka mtandaoni na Zanzibar**



# Mukrim Mohamed Khamis

**Na Mwandishi wetu**

Hakujawahi kutokea ushindi wa jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania tangu zianze miaka 14 iliyopita kwa kazi ya TV ya mtandaoni, au kwa mwandishi wa aina yoyote ya chombo cha habari, iwe redio, televisheni au magazeti kutoka Zanzibar.

Haijawahi pia kutokea suala jipya ambalo limepewa kipaumbele na serikali likampa ushindi wa jumla mwandishi wa habari nchini, na suala lenyewe ni Uchumi wa Buluu, kipaumbele cha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Hussein Ali Mwinyi.

"Kila kitu ni kwa mara ya kwanza au haijawahi kutokea," hivyo ndivyo unavyolazimika kusema kuhusu Mukrim Mohamed Khamis aliyeibuka mshindi wa jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2023 kama alivyotangazwa katika kilele cha kinyang'anyiro hicho, Jumamosi, Septemba 28, mwaka 2024. Mohammed alijikita kufuatilia kwa karibu jitihada za kukuza Uchumi wa Buluu Zanzibar na mazingira yanayoathiri uchumi huo. Mfululizo wa habari alizoandika umeshinda tuzo katika kundi la Biashara, Uchumi na Fedha na nyingine katika Mazingira na Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji.

### Mukrim Mohamed Khamis ni nani?

"Nimezaliwa Zanzibar, wazazi wangu wote ni Wazanzibari. Nina miaka 29 sasa. Nimesoma shule ya msingi Mwanakwerekwe B na shule ya sekondari nilikohitimu kidato cha nne ni Mwanakwerekwe A,"anasema Mukrim anapoanza kusimulia historia ya maisha yake na kuongeza kwamba kutokana na kuipenda kazi ya utangazaji wa habari aliamua kujitolea kutangaza mwaka 2014 mara baada ya kumaliza kidato cha nne.

“Mara nyingi unapojitolea unapewa nafasi ya kuamsha popo, yaani unatangaza vipindi vya usiku wakati waandishi na watangazaji waajiriwa wamekwenda nyumbani, wewe unaambiwa ukeshe ukitangaza au kusimamia vipindi vya usiku,” anasema Mukrim akifafanua maana ya kuamsha popo.

Baadaye alisoma katika Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar, kozi ya ununuzi ambako alihitimu na kupata cheti mwaka 2016.

Akijitambua vipaji vyake, uwezo na shauku ya maisha yake ya baadaye, Mukrim aliamua kuanzisha TV ya mtandaoni akiita Zanzibar 360. Jina la TV linatosha kuashiria fikra zake kuhusu aina ya maudhui ambayo yangehitaji ujasiri, maarifa, ujuzi katika ukusanyaji na uchakataji. Hata hivyo, masharti ya usajili ya TV za mtandaoni yalipoanza, anakiri, hakuyamudu.

Baadaye Mukrim alipata nafasi ya kusimamia matangazo ya redio ya Assalam FM huko Unguja. Redio hiyo ndiyo ilikuwa imeanza, hawakuwa na habari wala vipindi vya aina yoyote.

Wajibu wa kusimamia matangazo ulimsukuma akasomee taaluma ya habari. Alijiunga na Royal College, Dar es Salaam alikohitimu mafunzo yake ya uandishi wa habari na utangazaji. Mara baada ya kuhitimu akafanya kazi rasmi akiwa mwajiriwa kituo cha Swahiba FM kati ya mwaka 2017 hadi 2020.

Kwa sasa Mukrim anajiona anaishi katika ndoto yake kutokana na fursa aliyoipata ya kusimamia na kuendesha KTV TZ Online. Anasema, mmiliki mpya wa kituo hiki cha mtandaoni ambaye kwake ni sawa na mzazi wake alimuomba akisimamie.

“KTV kwangu ni future, ulimwengu upo kinganjani, watu wanahitaji kupashwa habari kiganjani. Ninafurahia kutimiza matakwa ya kikatiba ya kuwapatia wananchi habari. Ninafurahi kwamba vyombo vya mitandaoni vinatambulika kama vyombo vingine. KTV kwangu ni sehemu ya maisha, ninafurahi kuishi katika ndoto yangu. Ninawafikia wafuatiliaji zaidi ya laki tatu, sasa naelekea laki nne, “

Mukrim anasema mafanikio yake yametokana na mafunzo zaidi aliyoyapata kutoka Jamii Media. Anawataja wasimamizi wa mafunzo hayo kuwa ni Mike Mushi na Gervas Mahimbi ambao kwa pamoja kupitia mradi uliofadhiliwa na Ubalozi wa Uswisi waliwajengea uwezo na kuwafanya wabobee katika maeneo mahsusi.

“Mbali na utalaamu wa namna ya kuandika maudhui ya mitandaoni, tulisisitizwa kubobea katika eneo mahsusi. Mimi niliamua kubobea katika uandishi wa habari za mabadiliko ya tabia nchi, mazingira na hifadhi ya vyanzo vya maji,” anasema Mukrim na kuongeza, “Kutokana na kubobea katika eneo hilo, nimejikuta kazi zangu zikitambuliwa na kuwa miongoni mwa wateule wa tuzo za umahiri wa uandishi wa habari tangu nilipoanza kushiriki tuzo za mwaka 2022 na hata hizi za mwaka 2023,”




*Mheshimiwa Balozi Didier Chassot kutoka Ubalozi wa Uswizi nchini Tanzania akimkabidhi Mukrim Mohamed cheti cha kuhitimu mafunzo ya maudhui ya mtandaoni yalioendeshwa na Jamii Media, 17 Novemba 2023.*




Ikumbukwe kwamba Mukrim amehitimu mafunzo ya mwaka mmoja ya habari za mitandaoni mwaka 2023 ambapo walikabidhiwa vyeti vyao vya kufuzu mafunzo na Balozi wa Uswisi nchini Tanzania.

Anajivunia kuwa mshindi wa pili katika EJAT ya mwaka 2022 katika kundi la hifadhi ya mazingira na anajivunia kuona mwaka huu pia kwa EJAT ya mwaka 2023 yu miongoni mwa wateule 72, ambapo wakati wa mazungumzo haya hakujua hatima yake siku ya Jumamosi tarehe 28 Septemba, 2024. Hakujua kama angeibuka kidedea au angeendelea kushika nafasi ya pili kama ilivyokuwa mwaka jana.

Mukrim anasema moja ya vitu vikubwa alivyojifunza kutokana na mafunzo aliyoyapata Jamii Media ni umuhimu wa kuchagua eneo la ubobezi katika uandishi wa habari ili ujikite huko na kubobea katika maudhui mahsusi, badala ya mwandishi kuwa katika kila aina ya habari. Kujikita katika eneo fulani ni kujitengeneza na kujitofautisha katika biashara ya habari, anasisitiza.

Hoja yake inaungwa mkono na mkufunzi wa mafunzo hayo Mike Mushi ambaye katika mazungumzo na Jarida la Tuzo anamkumbuka kijana kutoka Zanzibar kuwahi kupitia mafunzo yao.

"Tulikuwa tukiendesha mafunzo ya siku tano na kisha wanaofunzwa wanaendelea kuwa chini ya Mwanaumezi kwa mwaka mmoja. Tulianza na watu 20, wanaume 10 na wanawake 10. Lakini tukawachuja na kubaki na watu 10 waliohitimu mafunzo hayo yaliyolenga kuwajengea udadisi wa habari ili wajitenge na habari za matukio, na pia wafahamu namna ya kufanya biashara mitandaoni," alisema Mike wakati wa mazungumzo.

"Tuliwafunza kwa undani kuhusu biashara za mitandaoni, uandishi wa habari za mitandaoni, uzalishaji wa maudhui ya mitandaoni, namna ya kutumia kamera, kufanya uhariri kidigitali na waliofuzu tuliwapa vifaa vya kufanyia kazi," anasema Mike.

Vijana 20 walipatikana kutoka katika mchujo wa waombaji 410. Na mchujo wa vijana 10 waliofuzu ulizingatia nani mpaka wakati wa mchujo alikuwa akimiliki chombo cha habari cha mtandaoni na kwamba ni mwandishi wa habari. Mike anasisitiza kuwa mafunzo ya aina hii yanasaidia sana kulinda maadili ya uandishi wa habari za mitandaoni.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutangazwa kuwa ni mshindi wa jumla wa tuzo za umahiri wa uandishi wa habari, Mukrim anasema; "Ushindi huu ni kumbukizi ya kumuenzi baba yangu aliyetangulia mbele ya haki. Hajafaidi mafanikio ya kazi yangu. Ni kwa heshima pia ya mama yangu ambaye yupo hai na wadogo zangu."

Anasema anamshukuru mmiliki wa KTV TZ Online kwa kumfungulia fursa ambayo imemfanya hatimaye awe mshindi wa jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania.

Mukrim ambaye hajaoa wala hana watoto amekuwa akijipatia kipato kati ya shilingi laki saba hadi milioni moja kwa mwezi kwa wastani kutokana na kazi yake ya habari za mtandaoni, kipato kinachomwezesha kumtunza mama na wadogo zake na kuendesha maisha kwa ujumla.
Anawashukuru baadhi ya waandishi wenzake wengine walio nje ya KTV ambao kutokana na mawazo ya habari humsaidia kuboresha wazo lake na wakati mwingine kumuuganisha na vyanzo muhimu vya habari. Ni kwa ushirikiano wa aina hiyo, Mukrim anathibitisha kwamba huwezi kuwa mshindi peke yako bila msaada wa wenzako.

"Mimi ninahariri habari yangu mwenyewe. Lakini hunilazimu wakati mwingine nitumie hata siku tano kujitafakarisha na kuboresha kabla sijamshirikisha mwenzangu mwingine kuipitia na kabla ya kuirusha habari yenyewe," anaongeza Mukrim na kuthibitisha maarifa, ujuzi na uadilifu katika kazi yake ulivyompaisha na kuwa mshindi wa kwanza wa jumla kutoka Zanzibar baada ya miaka 14.

Inaaminika kuwa habari iliyompa ushindi Mukrim imezingatia vigezo nane muhimu ikiwa ni pamoja na uthabiti wa utalaamu, ufundi wa kiuandishi mtandaoni kiasi cha kuvutia hisia za wasomaji.

Vingine ni ubunifu, mchanganyiko wa sauti, maandishi, takwimu, picha mnato na mgando, viunganishi vyote vikitumika kusimulia habari. Umahiri wa maudhui yanayoongeza thamani kwa msomaji. Maarifa mapya yanayoendana na wakati. Kuzingatia maadili na uadilifu. Habari inayoleta mabadiliko katika jamii. Kuunganishwa kwa habari na mitandao ya kijamii na matumizi sahihi ya lugha.



*Mukrim Mohamed akimuhoji Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi.*

*Mimi ninahariri habari yangu mwenyewe. Lakini hunilazimu wakati mwingine nitumie hata siku tano kujitafakarisha na kuboresha kabla sijamshirikisha mwenzangu mwingine kuipitia na kabla ya kuirusha habari yenyewe.*

# Kishindo! cha Habari

Karibu usome kishindo kinachotokana na maudhui. Kila maudhui katika kurasa hizi yana nia ya kufahamisha, kuelimisha, kuhamasisha au kuiongoza hadhira kuchukua hatua. Ni maudhui yanayounda uhusiano wa maana na hadhira na kuchochea mabadiliko halisi na chanya katika jamii. Yanazingatia mahitaji ya jamii, misingi na usuli. Kishindo cha habari hujenga uhusiano wa kihisia na hadhira, kwa kutumia mbinu za kusimulia hadithi na picha. Ni maudhui yanayotegemea ukweli, utafiti, na vyanzo vya kuaminika, yakihusisha takwimu, funzo mahsusi na ushuhuda. Kishindo cha maudhui yanachaguliwa kutoka katika ingizo la maudhui yanayoshindanishwa katika tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania na kuangazia kishindo cha habari kwa maisha ya watu katika jamii.

Kishindo! cha Habari

# Vifuu mbadala wa Zebaki kwa wachimbaji wadogo

**Na Florence Majani**



Ni katika maonyesho ya kimataifa ya biashara ya Sabasaba, Esau Ezra, mwanahabari wa kampuni ya Habari ya Nukta Afrika, amefika hapo kutimiza majukumu yake ya kazi.

Esau anaingia katika banda la Tume ya Sayansi na Vyuo Vikuu (COSTECH), na hapa anakutana na kampuni ya Timasu, inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na nazi.

Katika mahojiano yake, Esau, alibaini kuwa kampuni hii ya Timasu, pamoja na kutumia nazi katika kuzalisha bidhaa lukuki, akabaini zaidi kuwa nazi, inatumika kuzalisha *'activated carbon'* bidhaa inayosaidia kusafisha madini ya zebaki, ili yasilete athari za kimazingira na za kiafya kwa wachimbaji wa madini.

Na hapa ndipo Esau, alipoandika makala iliyopewa kichwa cha habari kisemacho: *'Teknolojia ya vifuu vya nazi itakavyo waokoa wachimbaji na madhara ya zebaki'*.

"Nikaona, kama bidhaa inaweza kutumika katika uchenjuaji madini, hapo ndipo kuna stori, kwa sababu niliwahi kufanya makala inayoeleza athari za uchimbaji wanazopata wachimbaji wadogo mwaka 2022".

Esau anasema aliamua kuifanya habari hii kwanza kueleza uwepo wa bidhaa hii ambayo ni mbadala wa zebaki, ambayo itasaidia kupunguza na baadaye kuondoa kabisa matumizi ya zebaki.

"Hilo ndilo lililonisukuma kuandika hii habari," anasema Esau anaeleza, baada ya kupata wazo, aliliwasilisha kwa mhariri, Nuzulack Dausen, na baada ya hapo yeye kwa kusaidiana na mhariri walijikita kwanza katika kufanya rejea, kwa mfano, takwimu ili kufahamu idadi ya wachimbaji wadogo Tanzania, je viongozi wa serikali wamesema nini kuhusu athari za kimazingira za matumizi ya zebaki, je kuna hatua yoyote kuhusu athari hizi.

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

"Lakini nilikwenda kufanya utafiti zaidi, je kuna hii bidhaa ya *'activated carbon'* na tukabaini kuwa Tanzania inatumia zaidi ya shilingi bilioni 32, kila mwaka kuagiza bidhaa hiyo, kwani haitumiki kwenye madini bali viwanda vinavyojikita katika usafishaji wa maji," anasema alifanya utafiti wa kina wa makala hii na wakati akiendelea alibaini zaidi kuwa Tanzania ni nchi inayozalisha nazi kwa wingi duniani na kwa Afrika, ni ya pili.

Esau, alikusanya maudhui haya na kuyaweka kwenye habari moja katika mtiririko unaofaa. Anasema mhariri wake alimsaidia katika hili kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, anasema, haikuwa rahisi, ingawa alipata wazo la habari mwezi Julai, wakati wa maonyesho ya Sabasaba, lakini makala yake ilirushwa mnamo Agosti 22, mwaka 2023.

Mwanahabari huyu, hakuishia hapo, kadhalika alizungumza na wadau wa mazingira, alikusanya takwimu za Shirika la Afya Duniani.

Katika makala yake, Esau, ameandika: "Upatikanaji wa bidhaa hiyo mbadala wa zebaki katika shughuli za uchechuaji itakuwa mkombozi kwa wachimbaji pamoja na jamii ambayo inaweza kuathirika kwa kuvuta hewa, kula chakula au kunywa maji yaliyo na sumu ya zebaki."



*"Kuwa mshindi kumenitia moyo lakini nimepata hamasa, ambayo inanifanya kuendelea kufanya habari na makala ambazo zinaweza kuwasaidia watu,"*

Lakini pia habari yake ilitumia mifumo tofauti ya kuwasilisha habari hii. Kwa mfano, habari hii ilikwenda pia katika mfumo wa video, na ikawekwa katika mtandao wa YouTube, mfumo wa takwimu zinazoeleza habari kwa wepesi zaidi.

"Kwa kutumia takwimu na data unamsaidia mtu kuelewa kwa urahisi ajue nini kinachowasilishwa, kwa hiyo ni kubadilisha mtazamo wa watu kuhusu ile dhana kuwa habari za mtandao ni za uzushi na udaku, sisi tunawapa watu habari bora kwa kutumia mitandao hii," anasema.

## MATOKEO CHANYA

Mara baada ya kuchapishwa kwa habari hii, Esau anasema kumekuwa na ongezeko la watumiaji wa bidhaa hii, 'activated carbon' jambo ambalo yeye anaona limesaidia kupunguza athari zitokanazo na madini ya zebaki.

"Niliyajua haya kwa sababu tulikuwa tunapata simu nyingi kutoka kwa wasomaji, wakitaka kununua bidhaa hii na sisi tuliwapa namba ya wazalishaji," anasema.

Pamoja na mafanikio hayo, kadhalika kampuni ya Timasu, ilifanikiwa kupata mtambo mkubwa wa kuzalisha kilogramu 400 kwa siku.

Awali, mtambo waliokuwa wanautumia kuzalisha bidhaa hii ulikuwa ukizalisha kilogramu 120 pekee kwa siku.

Kampuni ya Timasu, ilifanikiwa kupata mtambo mkubwa zaidi wa kuzalisha 'activated carbon, chini ya mradi wa Imbeju unaotekelezwa na CRDB. Timu ya Jarida la Tuzo ilifanikiwa kuzungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni inayozalisha bidhaa hizi za activated carbon, Tiberius Mario, ambaye amesema, tangu habari hii ichapishwe kwenye tovuti ya Nukta, wamejitokeza wauzaji wa vifuu vya nazi lukuki.

"Hapa nilipo kuna tani 14 za vifuu vya nazi Morogoro, na tani nyingine 60, wilaya ya Mkurunga Pwani, wauzaji walikuja kwa wingi mpaka nikashindwa kuwamudu, hii kwangu ni faida kwa sababu sasa naona watu wameona fursa, ambayo pia inasaidia kuondoa uchafuzi wa mazingira," anasema.

Tiberius anasema matokeo chanya mengine ni kuuza bidhaa hii kwa wachimbaji wadogo, ambao walihama rasmi katika kutumia madini ya zebaki.
"Waliponipigia simu wakitaka kununua bidhaa hii hawakuamini kama inatengenezwa Tanzania, wao waliamini inazalishwa nchi za nje tu," anasema.

Pamoja na hayo, kadhalika Tiberius anasema: "Tulipata mtambo mkubwa wa kuzalisha bidhaa mbadala wa zebaki. Kwa sababu tuliona mahitaji ni makubwa na uzalishaji ni mdogo, kwa hiyo tukapata msaada kutoka CRDB na kununua machine inayozalisha kilo 400 kwa siku."

## TUZO ZA EJAT

Hii ni mara ya kwanza kwa Esau kuingia kama mteule katika kinyang'anyiro hiki cha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania, za EJAT.

Awali, alikuwa akiwasilisha kazi zake, lakini hazikuwahi kufika katika hatua ya fainali "EJAT imekuwa ni chachu ya kufanya uandishi wa habari zenye tija na zenye mashiko, ambazo zinawasaidia watu kufanya maamuzi sahihi," anasema.

Anasema kilichompa hamasa ni tuzo iliyowekwa katika chumba cha habari cha Shamba FM, ambayo Esau anasema, tuzo ile pale studio, ilimpa chachu ya kutamani naye kutuzwa kama wanahabari wenzake.

"Kuwa mshindi kumenitia moyo lakini nimepata hamasa, ambayo inanifanya kuendelea kufanya habari na makala ambazo zinaweza kuwasaidia watu,"

Kishindo! cha Habari



# Habari iliyomtoa machozi Mwandishi

**Na Peter Nyanje**

"Niliifanya habari hii huku machozi yakiwa yananitoka. Nilitokwa na machozi wakati wa kufanya mahojiano kama ambavyo nilitokwa machozi wakati nikiwa naandika. Hii ni kwa sababu kama mwanamke nilikuwa napata yale maumivu na uchungu ambao niliokuwa nawahoji wanapitia kwani mimi mwenyewe pia nilikuwa na tatizo linalofanana na haya niliyokuwa nayasikia kutoka kwa waathirika," anasimulia Zourha Malisa, kuhusiana na habari yake ambayo majaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) waliafiki kuwa ni moja ya habari zinazostahili kushindanishwa kwenye tuzo hizo.

Malisa, ambaye ni mwandishi anayefanya kazi katika kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL) na mtaalamu wa habari za kidijiti, anasema wakati anaandika habari hiyo kwa sehemu ilikuwa kama anaandika kuhusu yanayomsibu yeye mwenyewe kwani naye alikuwa amepitia changamoto za kupata mtoto.

Anasema kuwa safari aliyopitia wakati akitafuta suluhisho ya changamoto anayokabiliana nayo kuhusiana na masuala ya kupata mtoto ndiyo ilizaa wazo la kuifanya habari hii.

“Ni mwaka wa nane sasa nahangaika kutafuta mtoto na ni katika mahangaiko hayo ndiko nilikopata wazo la kuandika habari hii baada ya kukutana na wanawake wengi waliokuwa wanahangaika kutafuta watoto. Ni kwenye mahangaiko yangu hayo ambako nilikutana na wale niliwatumia kama vyanzo katika makala yangu,” anasimulia.

Habari ya Malisa inahusu simulizi ya mama ambaye alilazimika kuchoma sindano 38 tumboni katika kipindi cha miaka 13 akihangaika kupata mtoto.

Umuhimu wa habari unatokana na ukweli kuwa tatizo la watu kusaka watoto ni kubwa sana nchini lakini haliongelewi kwa uwazi sana na sababu kadhaa, kubwa ikiwa ni unyanyapaa ambao wanawake wanaohangaika kutafuta mtoto wanakumbana nao, aidha majumbani mwao au katika jamii.

Malisa anakiri kuwa uzoefu aliokutana nao wakati akifanya habari hii unadhihirisha kuwa usiri katika suala hili unasababisha maumivu na mateso makubwa kwa wanawake wengi ambao wanalazimika kuugua kimya kimya kwa sababu tu wana hofu ya mrejesho hasi watakao kumbana nao katika jamii iwapo watajitambulisha wazi wazi kuhusu matatizo wanayoyapitia.

Malisa anasema aliamua kuifanya habari hiyo ili kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na masuala ya afya ya uzazi. Kwa mujibu wa mwandishi huyu, watu wengi katika jamii wana tafsiri finyu sana kuhusiana na afya ya uzazi.

“Watu wengi wanaposikia afya ya uzazi wanadhani ni masuala yanayohusiana na msichana kupata ujauzito. Wengi wanadhani afya ya uzazi ni masuala ya wasichana au wanawake. Kumbe ni suala pana sana likihusisha mambo mengi yanayowahusu watu wote katika jamii,” anasimulia.

Ukiacha uzoefu binafsi kwenye tatizo hili, ukosefu wa elimu na uelewa kuhusiana na suala hilo ni jambo jingine ambalo lilimsukuma mwandishi kufanya habari hii. Anasema alipenda kutumia uzoefu wake katika tatizo hilo na uwezo wake wa kuelimisha kupitia vyombo vya habari kuisaidia jamii kutafuta suluhisho la tatizo la wanawake kushindwa kupata watoto.

Malisa anasema wakati akiandaa habari hii alibaini kuwa pamoja na kuwa tatizo la wanawake kushindwa kupata watoto lina sababu zake kisayansi lakini kwa kiasi kikubwa linahushwa na masuala ya mila na desturi jambo ambalo si sahihi. Aidha, anabainisha kuwa kwa bahati mbaya mila hizo nazo zinakwaza suala hilo kuongelewa kwa uwazi na mapana yake kama njia ya kutafuta suluhisho.

> *“Ni kwenye mahangaiko yangu hayo ambako nilikutana na wale niliwatumia kama vyanzo katika makala yangu,”*

"Kuna uwezekano mkubwa kuwa kama suala hili lingeongelewa kwa uwazi na kwa mapana na jamii nzima yale maumivu na mateso ambayo wanawake wanapitia kusaka mtoto kwa njia za kitaalmu yangepungua sana. Tungekuwa wawazi masuala haya yangekuwa yanabainika mapema na hivyo hata kupunguza gharama ambazo zinaingiwa iwapo tatizo linachelewa kubainika," anasema.

## Habari yenyewe

Ni kisa cha mwanamke ambaye alihangaika kutafuta mtoto kwa miaka 13. Licha ya maumivu ya kimwili yaliyotokana na aina ya matibabu aliyopatiwa yanayohusisha kuchoma sindano nyingi, lakini kisa kinaonyesha jinsi mwanamke huyo alivyopitia maumivu ya kihisia na gharama kubwa alizozitumia akitafuta suluhisho.

Ilifika mahali alilazimika kuchukua mkopo wa Sh20 milioni zilizohitajika kwa ajili ya matibabu. Lakini fedha hizo zilitumika zote na hakufanikiwa kupata ujauzito. Tatizo la kutokuwa na mtoto likabaki pale pale lakini akiongezewa na mzigo wa deni.

Habari inaonyesha jinsi mwanamke huyo alivyokuwa jasiri na jinsi alivyoamua kuisimamia dhamira yake ya kusaka mtoto. Baada ya jaribio la kwanza la kupata mtoto kwa njia ya kupandikizwa kushindikana huku akibaki na deni kubwa, hakukata tamaa.

Baada ya hospitali iliyompatia matibabu hayo kubaini uimara wa dhamira yake iliamua kumsaidia sehemu ya gharama ili afanye matibabu kwa mara ya pili. Lakini matibabu hayo nayo hayakuzaa matunda.

Hapo watu wengi waliamini kuwa mwanamke huyo ataachana na harakati za kusaka mtoto kwa njia ya upandikizaji. Lakini wakati watu wakidhani hivyo yeye mwenyewe alikuwa na mawazo tofauti.

Alienda kufanya majaribio hayo mara ya tatu na aliposhindwa akafanya mara ya nne na ikashindikana pia.

Lakini hakukata tamaa, na majaribio ya mara ya tano yakampatia kile alichokuwa anakipigania, akashika ujauzito na kujifungua salama.

Ingawa sasa anajivuna kuwa ni mama wa mtoto wa miaka mitano, lakini ni mtoto aliyepatikana kwa maumivu na gharama kubwa. Hata hivyo, kwake yeye maumivu na gharama hizo haziwezi kulingana na thamani anayoiweka kwa kiumbe alichokileta duniani, yaani mtoto wake.

"Akina mama wa aina hii wapo wengi sana. Wapo ambao wakishindwa mara moja wanakata tamaa na kuachana na kusaka mtoto kwa njia ya upandikizaji. Hawa wanalazimika kuishi maisha ya uchungu kwani ukiona mtu anaingia gharama kama hizi kusaka mtoto ina maana ni jambo ambalo moyo wake unalitamani kwa kiasi kikubwa. Hivyo anapokosa akaamua kuacha kuendelea kumtafuta kwa njia hii ina maana anaishi huku moyo wake ukiwa hauna furaha kwa sababu ya kukosa mtoto," anasema Malisa.

## Changamoto

Kwa mujibu wa Malisa, hata wale ambao wanaendelea na jitihada za kusaka mtoto kwa njia hii ni wengi pia.

"Kuna mama ambaye nilikutana naye yeye ameshafanya majaribio ya kupandikiza ujauzito kwa zaidi ya mara 14 bila mafanikio na bado hajakata tamaa. Nilisikitika sana alipokataa kuongea nami ingawa mwanzoni tulikubaliana anieleze kisa chake. Lakini naelewa kwa nini alikataa kuwa muwazi," anasema Malisa.

Malisa anabainisha suala la waathirika kutokuwa tayari kulizungumza suala hilo kwa uwazi ni changamoto kubwa aliyokutana nayo wakati akifanya habari hii.

Pia, yeye binafsi alikutana na changamoto nyingine kutokana na kuwa suala alilokuwa analiandikia ni suala ambalo yeye mwenyewe ni muathirika.

“Kuna wakati nikiwa nafanya mahojiano nilikuwa najikuta kama mimi ndiye mwathirika kutokana na yale tuliyokuwa tunaulizana na kujibizana. Inafika wakati *source* (chanzo) analia na mimi najikuta nikitokwa na machozi kwa sababu ya kuufahamu kwa undani uchungu ambao anaupitia,” anasimulia.

### Matokeo

Kuhusu matokeo ya habari yake katika jamii, Malisa anasema kuwa imekuwa na matokeo chanya kwani inaonekana kuwa imewaamsha wanawake wengi ambao wana tatizo la kutopata ujauzito lakini hawakujua kuwa kuna suluhisho la kisayansi la tatizo linalowakabili.

“Bahati nzuri habari yangu ilianzia katika hospitali ambayo mimi pia napata matibabu hapo. Hivyo wameendelea kuwasiliana na mimi na wamenieleza kuwa baada ya habari ile idadi ya wanawake wanaokwenda kutafuta suluhisho la kukosa ujauzito imeongezeka,” anasema.

Aidha, Malisa anasema wapo pia watu, wakiwamo wanaume, ambao wamekuwa wakimtafuta yeye binafsi kutaka maelezo ya kina kuhusiana na suala hilo.

“Baada ya kusoma habari niliyoiandika wapo watu wengi wananipigia wakiniambia kuwa wanataka maelezo ya kina kuhusiana na upandikizaji mimba. Wengine wananiuliza maswali moja kwa moja wakidhani kuwa mimi ni mtaalamu wa masuala hayo na wengine wanaulizia kuhusu hospitali ambayo inatoa matibabu hayo,” anasema.

Anasema hilo linaonyesha kuwa habari hiyo imewagusa watu katika jamii.

Aidha, Malisa anasema visa alivyovisikia wakati akiwahoji waathirika vimempatia nguvu yeye kama mwathirika kukabiliana na hali aliyokuwa nayo. Pia vimempatia nguvu ya kuendelea kusaka suluhisho la tatizo lake bila kukata tamaa.

ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

Do You Have Any Opinion?
Complaints?
Inquiries or Advice

ZRAFunguka
Submit your comments digitally



DOWNLOAD HERE
Available on the App Store
GET IT ON Google Play

For more Info
Free Call **0800 712 533**

Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar

zanzibar_revenue_authority
www.zanrevenue.org

VIDEO AUDIO PHOTO WEB



Kishindo! cha Habari

# Upande wa pili wa shilingi ya ugumba

**Na Peter Nyanje**

Katika jamii nyingi, si Tanzania tu, bali Afrika nzima, wanandoa wanaposhindwa kupata mtoto basi lawama zote humwangukia mwanamke. Mwanamke huonekana ndiye mwenye tatizo linalosababisha wanandoa hao wakose mtoto.

Ni nadra sana kukuta mwana mume akilaumiwa pale mke wake anaposhindwa kushika ujauzito.

Aidha, madhila yanayotokana na familia kukosa mtoto humwangukia pia mwanamke peke yake. Kama ni masimango basi yatamkabili yeye, kama ni aibu basi itakua ni ya kwake peke yake.

Ni nadra sana kusikia kuwa mwana mume anapata misukosuko ya aina yoyote kwa sababu tu kwenye ndoa yake wameshindwa kupata mtoto.

Lakini ukiingia kwa undani kuliangalia suala hilo wataalamu wanabainisha kuwa suala la wanandoa kupata mtoto linahusisha wote wawili, mume na mke.Zipo familia nyingi ambazo zinakosa kupata mtoto kutokana na matatizo ya kibaolojia ya mwana mume.

Aidha, taarifa zinaonyesha kuwa wapo wanaume wengi ambao wamepata madhila mengi kutokana na tatizo la kukosa mtoto.

Na ndicho mwandishi Adam Hhando alichokionesha katika habari yake iliyopewa kichwa cha habari 'Ukatili dhidi ya waume wanaoshindwa kutungisha mimba wake zao.'

Hiki ni kipindi cha radio ambacho mwandishi anaonesha upande wa pili wa shilingi, yaani jinsi wanaume nao wanavyoteseka kutokana na kukosa mtoto katika mahusiano yao ya kindoa.

"Kilichonisukuma kuandika habari hii ni baada ya mwaka juzi kuandika habari kuhusu wanawake wanaonyanyaswa kwa kukosa watoto. Wakati nafanya utafiti wa habari hiyo nikagundua pia kuwa kuna wanaume ambao nao wanateseka kutokana na kukosa watoto. Baada ya habari ile ya kwanza kuchapishwa nikaamua kufanya utafiti mwingine safari hii ukilenga kuonesha jinsi wanaume nao wanavyoteseka na suala hili," anasema Hhando alipozungumza na Jarida la Tuzo.





Hhando anasema kuwa habari yake imeonesha kuwa wapo wanaume wanaoteseka kutokana na kukosa watoto. Ukiacha mateso ya kisaikolojia lakini wapo wanaopata mateso ya kimwili pia kwani wapo wazee ambao sasa hivi hawana watu wa kuwatunza kwa sababu tu hawakujaliwa kupata watoto.

"Kuna mzee nilikutana naye ana zaidi ya miaka 70. Ni mtu ambaye kutokana na uzee anahitaji msaada wa watu wengine kwenye maisha yake lakini analazimika kujihudumia kwa kila kitu kwa sababu hana mtoto na mke alimkimbia zamani baada ya kubaini kuwa hana uwezo wa kutungisha mimba," anasimulia Hhando, mwandishi wa CG FM ya Tabora.

Hhando anabainisha kuwa kujificha kwa tatizo hili linalowakabili wanaume ni moja ya mambo yaliyomsukuma kuandika habari husika na kuitangaza ili kutoa elimu kwa jamii kuwa kunapaswa kuwepo kwa mikakati ya kuwasaidia wanaume wa aina hii kama ambavyo wanawake walioathirika na kukosa watoto wanavyosaidiwa.

"Kama unavyojua katika mila na desturi za Kiafrika wanaume kwa kawaida huwa ni wasiri sana. Hawapendi kueleza matatizo yao. Ukiona mwana mume anatoka hadharani kueleza tatizo lake basi ujue kuwa kweli hilo ni jambo linalomsumbua kupita kiasi," anasema Hhando na kuongeza: "Ndio maana nikaona ni vema nitumie nafasi niliyo nayo kwenye chombo chetu cha habari kuelezea hili ili jamii ijue, wahusika wafahamu na hatua zichukuliwe kukabiliana na tatizo hilo."

### Umuhimu wa habari hii

Mwandishi anabainisha kuwa katika jamii nyingi inaaminika kuwa suala la ugumba linamhusu mwanamke peke yake. Lakini ukizungumza na watalaamu wanabainisha kuwa hata wanaume nao wanapatwa na tatizo hilo.

Kwa kuwa jamii nyingi hazielewi suala hilo na jamii nyingi zikikataa kukubaliana na ukweli huo, ndipo mwandishi akaamua kujikita kuandika habari hii kama sehemu ya kuelimisha jamii kuhusu suala hilo.

"Naamini kuwa waliosikiliza kipindi hiki wameelimika sana kuhusiana na masuala ya ugumba kwani nimewahoji watalaamu kadhaa wanaolielezea suala hilo kwa undani," anasema Hhando.

### Habari yenyewe

Ni kipindi cha radio cha dakika 15 kinachoelezea mikasa ya wanaume kadhaa ambao wanaishi bila watoto kwa sababu ya ugumba.

Baadhi ya waathirika wa tatizo hili wanakiri kupitia kipindi hicho jinsi wanavyoteseka kutokana na kuishi maisha ya upweke baada ya kukimbiwa na wanawake waliokuwa wamewaoa. Kwa kuwa hawana watoto, basi sasa hivi wanalazimika kuishi maisha ya upweke.

Pia kipindi kimepata maoni kutoka kwa wataalamu wa masuala ya afya ya uzazi ambao wanaelezea kuhusiana na masuala ya ugumba na jinsi ambavyo wanaume nao wanahusika kwenye tatizo hilo tofauti na imani katika jamii nyingi kuwa ugumba ni tatizo linalowakumba wanawake peke yao.

### Changamoto

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari hii, changamoto kubwa aliyokutana nayo ni wanaume wengi wanaokabiliwa na changamoto zinazotokana na ugumba kukataa kuzungumzia matatizo yao wazi wazi.

"Wapo watu wengi sana wenye tatizo hili ambao nimekutana nao lakini ni wachache tu ndio walikuwa tayari kuzungumza na kurekodiwa bila masharti. Wapo ambao walikubali niwarekodi lakini nisiwataje majina yao. Lakini wengi ni wale waliokiri kuwa na tatizo hilo lakini hawakutaka kulizungumza wazi," anasimulia Hhando.

Changamoto hii ilimnyima mwandishi mawanda mapana ya kupata taarifa ambazo zingesaidia sana kuiboresha habari yake lakini alijitahidi kutafuta vyanzo vingine mbadala kupata maoni ya kutosha kushibisha habari yake.

Mathalani, aliwatumia wataalamu wa afya ya uzazi kuelezea visababishi vya wanaume kuwa wagumba. Aidha, watalaamu walimpatia pia maelezo kuhusiana na undani wa tatizo hilo kisayansi na jinsi ya kukabiliana nalo.

Kwa kuwa tatizo hili ni la kisaikolojia pia, labda mwandishi alipaswa pia kuzungumza na watalaamu kutoka katika eneo hilo ambao maelezo yao yangewasaidia sana wanaume ambao wanashindwa kujitokeza hadharani kuelezea changamoto wanazozipitia kutokana na ugumba.



*"Kama unavyojua katika mila na desturi za Kiafrika wanaume kwa kawaida huwa ni wasiri sana. Hawapendi kueleza matatizo yao. Ukiona mwana mume anatoka hadharani kueleza tatizo lake basi ujue kuwa kweli hilo ni jambo linalomsumbua kupita kiasi,"*

Kishindo! cha Habari

# Simulizi ya Watoto wanaoishi kwa makombo ya mifupa

NI kama msemo wa ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno, ndivyo unavyoweza kuelezea hali ya umasikini wa baadhi ya kaya katika jiji la Dodoma zinavyoishi kwa kuponea makombo ya mifupa kutoka mnada wa Msalato. Maisha yao kwa sura nyingine ni kielelezo cha jinsi umasikini unavyotweza utu wa wanakaya ambazo makombo ya mifupa ndiyo riziki ya kuendesha maisha yao.

Udhalili huu uko wazi mbele ya macho wa mamia ya watu wenye kipato cha kumudu kununua nyama katika mnada huu maarufu katika uchomaji nyama na vinywaji siku za mwisho wa wiki. Watoto wanaokadiriwa kuwa na umri wa miaka 9 hadi 18, wanapita huku na huku wakikusanya makombo ya mifupa ili kuponya njaa.

Pengine habari hii ya uchunguzi iliyofanywa na Mwandishi wa Habari wa kituo cha ITV, Benjamin Mzinga na kupewa kichwa kisemacho "Watoto wanaoishi kwa kula makombo ya mifupa mnada wa Msalato" inaweza kumtoa machozi kila anayetazama simulizi hiyo kwani ni kielelezo cha umasikini uliokithiri.

Makala hii iliyorushwa kwenye kipindi cha ITV cha Ripoti Maalum, inafungua fahamu za wengi juu ya madhila yanayozikumba kaya masikini mkoani Dodoma, ambazo mnada wa Msalato umekuwa ni kimbilio la kusaka chakula cha kujinusuru dhidi ya njaa kutokana na kukosekana kwa kipato. Ni simulizi inayobeba machungu juu ya kushindwa kwa mipango ya kifamilia, kijamii na pengine ya taifa ya kunusuru watu wenye uhitaji wa kweli wa kusaidiwa walau kupata mlo mmoja kwa siku.

Watoto hao hujikimu njaa na makombo hayo ya mifupa lakini pia huyakusanya na kuuza kwa watu wanaofanya biashara ya kuuza vyakula vya mifugo kama mbwa na kuku ili kupata fedha za kusaidia kaya zao kumudu mahitaji muhimu.

Watoto hao wanaeleza sababu za kugeuza makombo fursa ya kujipatia chakula, lakini mbaya zaidi wakila makombo hayo papo hapo mnadani bila hofu ya kupata athari zozote za kiafya. Wanasema UMASIKINI ndiyo umewafikisha hapo.

Mwanasaikolojia Cosmas Maduru, anasema watoto hao wanaofanya mambo yasiyo ya kawaida kama kuokota makombo ya watu wengine na kuyala, maisha yao yote watakuwa wameathirika hata kama baadaye wakitafutiwa suluhisho la hicho wanachokabiliana nacho kwa sasa. Mwanasaikolojia huyo anasema kuwa "hawa wamekwisha kuhama kutoka kawaida na sasa wanapambania kuishi."

Anafafanua kuwa muda wa kuwajenga watoto hawa kimaadili na kutambua utu wao ndiyo huo wanaingia kula makombo, hali hiyo ya kuokota vitu watakuwa nayo daima. Anaasa kwamba jambo hilo ni zaidi ya aibu na watoto watakuwa na ubovu huo maisha yao yote.

Makala hii inafichua pia udhaifu mkubwa wa Mpango wa Serikali wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) kwani watoto hao ambao wametumbukizwa kwenye ajira mbaya inayotweza siyo tu utu wao, bali pia familia zao, ni kwa sababu ya kukosa njia mbadala ya kupata uhakika wa chakula.

Miongoni mwa watoto waliotembelewa na mwandishi wa makala haya ni wa kaya mbili ambazo watoto wake wamegeuzwa kuwa ndio watafutaji wa chakula cha familia. Dada wa watoto wawili alithibitisha kwamba makombo hayo ya mifupa huwa wanayachemsha, kisha kuyaunga kwa mafuta kitunguu na nyanya kisha kuwa kitoweo cha kula ugali. Katika kaya hiyo, umasikini unashuhudiwa kwa macho bila hata utafiti wowote. Malazi yao ni duni, hakuna mzazi ila watoto peke yao wanaendesha maisha yao. Picha inayopatikana ni kuwa wazazi wamewatelekeza hawa watoto wajitegemee katika umri mdogo sana.

Katika kaya nyingine watoto hao wanakoishi pamoja na bibi yao, ambaye kwa hakika ni kikongwe, umasikini unakulaki unapofika katika mazingira yao. Maisha ya nyumbani kwao yanathibitisha umasikini wa kutupa. Bibi yao aliyetambulika kwa jina la Fatma Rakia, ingawa umri hautajwi, mwili wake unazungumza kwa wazi kabisa kwamba ni kikongwe. Mwili umedhoofu kwa sababu ya uzee, lakini pia kwa sababu ya lishe duni kama ambavyo yeye binafsi anashuhudia kwamba kama 'hujala siku mbili' unapata wapi nguvu ya kufanya chochote.

Anakiri kuwa wajukuu zake wanakwenda mnadani kuokota makombo, ingawa hawatumi wanajiongeza wenyewe kwa kuwa hawana chochote hapo nyumbani kwako. Bibi Fatma anasimulia kwamba hana fedha, hana chakula hata unga wa kukoroga uji hana, mbaya zaidi anaumwa. Mbali na hao watoto (wajukuu) wawili waliokutwa mnadani wakiokota makombo, anao wajukuu wengine kama wanne hivi. Wote wana umri mdogo unaokadiriwa kuwa chini ya miaka saba.




Soko la Mnada - Msalato

Anaeleza kwamba aliwahi kuwa chini ya mpango wa TASAF, lakini baadaye aliondolewa bila kuelezwa sababu yoyote. Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TASAF, Zuhura Mdungi, anaainisha vigezo vya kaya kuingizwa kwenye mpango wa TASAF kuwa ni pamoja na kuwa na makazi duni, watoto wengi ambao kaya haina nguvu ya kuwalea, kaya ya mzazi mmoja asiyemudu kutunza watoto, walemavu na kutokuwa kabisa na vitega uchumi vyovyote vinavyoweza kuwaletea kipato. Kwamba kaya ikijikwamua kwenye vigezo hivyo, huondolewa kwenye TASAF.

Kilio dhidi ya TASAF pia kinapazwa na Mzee Daudi Magati anayesema kwamba ruzuku ya TASAF haitabiriki. Kuna nyakati wanalipa baada ya miezi miwili au mitatu au minne, na pesa inayolipwa ni kati ya Sh 20,000/- hadi 25,000/- ambayo amehoji kwamba haiwezi kuwakwamua kwa kiwango kikubwa.

Kadhia hii ya kugeuza makombo kuwa ni shughuli rasmi ya kuokoa kaya masikini dhidi ya njaa ni kama imefumbiwa macho na mamlaka za usimamzi wa mnada wa Msalato na uongozi wa serikali ya mtaa wa Msalato. Kuna kukosekana kwa uwajibikaji. Ingawa Kiongozi wa Wafanyabiashara wa Mnada wa Msalato Abdul Hamis, anasema walipata kutumia mgambo kuwasaka watoto wanaojishughulisha na uokotaji wa makombo huku wakiyala hadharani, haikuwa endelevu.

Naye Afisa Afya Kata ya Msalato, Heri Mfungwa, anaeleza kuwa wamekuwa wakitoa elimu kwa umma na kuwaasa watoto hao wasile makombo hayo, hata hivyo, hali bado haijabadilika. Afya za watoto hawa ziko hatarini kutokana na kula makombo ya mifupa anatahadharisha Daktari Celestine Mpiri. Anaeleza kuwa maambukizi wanayoweza kupata watu wanaokula makombo ni pamoja na magonjwa ya tumbo na kutapika na yale ya njia ya upumuaji kwa sababu mabaki ya chakula yana uwezekano wa kuwa na vimelea vya maambukizi kutoka kwa mlaji wa awali.

Wakati kilio dhidi ya TASAF kutokuwafikia baadhi ya walengwa kikipazwa mkoani Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo, Rosemary Senyamule, anasema hana taarifa za kuenguliwa kwa baadhi ya kaya masikini katika mpango huo. Hata hivyo, anasema kuwa mkakati wa mkoa kwa sasa ni kuhamasisha wakazi wa Dodoma kulima mtama kwa wingi kama zao la biashara ili wapate kipato cha kununua mahindi kwani ukame unaathiri kustawi wa mahindi.

Mzinga akizungumzia kazi yake anasema kuwa anakumbuka kutafutwa na maofisa ustawi wa jamii kutoka Dodoma ambao walipiga kambi kwa muda eneo la mnada wa Msalato wakiwasaka watoto wanaofuata makombo ya mifupa. Walimpa uhakikisho kwamba wanafuatilia kadhia hiyo.

Ama kuhusu TASAF ana taarifa za kufanyika kwa rejea kwa watu waliokuwa wameondolewa, ijapokuwa hatua zaidi za kwenda kuonana na waathirika zinahitajika.

# Je Wajua?

Karibu katika kurasa za Je wajua? Utajifunza jambo jipya. Mada za kipekee zinazovutia na muhimu kwa maisha yako ya kila siku. Yumkini utabadilisha mtazamo wako au utaongeza maarifa na uelewa. Je Wajua ni maudhui yanayofanyiwa utafiti wa kina ili kuhakikisha usahihi na ukweli wa taarifa unaotokana na vyanzo vingi mbalimbali vya kuaminika. Utakutana na taarifa kwa muundo mfupi na rahisi kueleweka, lugha rahisi na ya moja kwa moja. Utakutana na hoja na mifano halisi inayoeleweka. Utakutana na ushawishi wa takwimu na ukweli wa haraka unaoimarisha hoja. Utakutana na mtindo wa kuvutia wenye maswali ya kuchochea fikra. Lengo kuu la kurasa hizi ni kukufunza kitu kipya kwa njia ya kukufurahisha na kukuelimisha. Utakutana na picha au michoro pale inapofaa ili kufafanua hoja. Mwishoni utakutana na swali au mawazo ya kuchochea fikira. Usikose kufuatilia maudhui ya Je wajua kila mara, utajifunza mengi.

> “*Je Wajua ni maudhui yanayofanyiwa utafiti wa kina ili kuhakikisha usahihi na ukweli wa taarifa unaotokana na vyanzo vingi mbalimbali vya kuaminika.*”

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Uwekezaji wa Kimkakati PSSSF

## Waongeza Ufanisi katika Malipo ya Pensheni

**Na Waandishi wetu**

Kuna msemo kwamba *"Takwimu hazidanganyi."* Hivyo, kuelewa jinsi takwimu zinavyofichua hali halisi imekuwa zawadi adimu kwetu kwani takwimu hizo zinafunua maajabu ya maboresho endelevu ya PSSSF, ambayo yameweza kupunguza muda wa kusubiri malipo ya mkupuo kwa wastaafu kutoka zaidi ya siku 365 hadi chini ya siku 60.

"Mfuko umepunguza muda wa wastaafu kusubiri pensheni. Mstaafu, akiwa na taarifa sahihi, analipwa ndani ya siku 60 kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mfuko," anasema Abdul-Razaq Badru, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Bw. Badru ambaye kazi yake katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilitambuliwa kuwa ya mfano wa kuigwa, amekuwa akibadilisha mfuko mkubwa wa hifadhi ya jamii wa Tanzania, PSSSF, kuwa mfuko wa hifadhi ya jamii unaozidi kuwa na ufanisi na msingi imara wa kifedha unaoaminika.

Kabla ya mageuzi ya 2018, yaliyoimarishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2022, mfanyakazi mstaafu angeweza kusubiri kwa zaidi ya mwaka mmoja hadi mitatu kuanza kufurahia matunda ya miaka ya jasho na kukesha akihudumia taifa la Tanzania. Leo, ni siku 60 tu. Ni afueni kubwa.

Bw. Badru anafafanua waziwazi, "Hii ni kutokana na kuboreshwa kwa hali ya kifedha ya Mfuko na mifumo yake ya utoaji huduma kwa wanachama. Wanachama wanapata taarifa sahihi kwa urahisi. Uwekezaji wa Mfuko ni muhimu sana katika kudumisha thamani ya michango ya wanachama dhidi ya mfumuko wa bei."

Ustahimilivu wa kifedha wa PSSSF uliongezeka kutoka wastani wa 22.30% mwaka 2020/21 hadi 36.4% kwa mwaka ulioishia Juni 2023.

### Mfuko Uwekezaji wa PSSSF

Mbinu ya uwekezaji wa Mfuko inayojumuisha aina mbalimbali za mali inajumuisha dhamana za serikali, hati za makampuni, mifumo ya uwekezaji wa pamoja, mikopo, mali isiyohamishika, amana za kudumu, hisa zilizoorodheshwa, hisa zisizoorodheshwa, na miradi ya miundombinu.

Uwekezaji katika dhamana za serikali ulifikia TZS bilioni 5,301.88, ikionyesha ongezeko la 5.50% kutoka mwaka uliopita. Ukuaji huu unaonyesha dhamira ya Mfuko ya kufadhili nakisi za bajeti kuu na kusaidia miradi mikubwa ya miundombinu, huku pia ikisaidia Benki Kuu ya Tanzania katika kudhibiti usambazaji wa fedha za taifa.

### Chanzo Kikuu cha Fedha

Vyanzo vikuu vya mapato ya Mfuko vinajumuisha michango ya wanachama na mapato yanayotokana na uwekezaji, ambayo yameongezeka hadi TZS bilioni 1,681.65 kufikia Juni 2023 kutoka TZS bilioni 1,420.87 kufikia Julai 2020. Hii ni sawa na ongezeko la 18%.

### Hati za Makampuni

Kwa upande wa hati za makampuni, uwekezaji wa Mfuko ulifikia TZS bilioni 28.57 ukijumuisha uwekezaji mkubwa katika hati za kijani, ambazo zinachangia katika uendelevu na uhifadhi wa mazingira. Ushiriki wa Mfuko katika mifumo ya uwekezaji wa pamoja, hasa katika UTT AMIS na WHI Reit, unaonyesha jukumu lake katika kuongeza thamani halisi ya mali na hivyo kunufaisha wawekezaji wa kipato cha chini.

### Amana za Kudumu

Amana za kudumu katika taasisi za kifedha zilirekodi ongezeko kubwa, zikiongeza ukwasi na utulivu wa taasisi hizi, hivyo kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla. Uwekezaji wa Mfuko katika hisa, zilizoorodheshwa na zisizoorodheshwa, unaendelea kukua, kukiwa na jumla ya thamani ya TZS bilioni 628.38 katika hisa zilizoorodheshwa na TZS bilioni 336.32 katika hisa zisizoorodheshwa, zikisaidia sekta mbalimbali zikiwemo za fedha, viwanda na kilimo.

### Kituo cha Mabasi cha Msamvu, Morogoro

Mfuko umefanya uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu, hasa katika ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Msamvu ambacho kinatumika kama kitovu cha kiuchumi, kikizalisha fursa nyingi za ajira na pia kusaidia biashara za ndani.

### Dhamana za Serikali

Kufikia tarehe 30 Juni 2024, thamani ya jumla ya dhamana za serikali ilikuwa TZS bilioni 5,301.88, ikionyesha ongezeko la 5.50% ikilinganishwa na TZS bilioni 5,025.36 zilizorekodiwa katika mwaka wa fedha uliopita (2022/23). Uwekezaji katika dhamana za serikali una jukumu muhimu katika

*Kituo cha Mabasi cha Msamvu, Morogoro*



kufadhili nakisi za bajeti ya serikali kuu, hasa kwa kukusanya mtaji kwa ajili ya miradi mikubwa kama vile maendeleo ya miundombinu ikijumuisha barabara, madaraja, mitambo ya umeme na kusaidia mfumo mpana wa kifedha nchini.

### Dhamana za Kampuni

Mfuko wa dhamana za kampuni ulikuwa na thamani ya TZS bilioni 28.57 kufikia tarehe 30 Juni 2024. Hii inajumuisha zile kutoka TMRC, Imaan Finance Ltd, NBC Bank, CRDB Bank na Tanga Uwasa. Katika mwaka huo, uwekezaji mpya katika dhamana za kampuni ulifikia TZS bilioni 18.50, na riba iliyopatikana ilikuwa TZS bilioni 1.92, ongezeko kubwa kutoka TZS bilioni 1.02 zilizorekodiwa katika mwaka wa fedha wa 2022/23. Mfuko uliwekeza TZS bilioni 5.5 katika CRDB Green Bond, ambapo fedha zilizokusanywa zilitengwa kwa ajili ya kufadhili uwekezaji na miradi inayostahiki ya kijani. Miradi hii inalenga maeneo kama vile nishati, ufanisi wa nishati, usafiri, maji, usimamizi wa taka, matumizi ya ardhi na miundombinu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. PSSSF pia imejitolea TZS bilioni 5.5 kwa TANGA UWASA Green Bond ambayo inatarajiwa kuwa na athari chanya, hasa katika uchimbaji, matibabu, na usambazaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa Tanga.

### Mfuko Uwekezaji wa Pamoja

Mfuko umeeneza uwekezaji wake katika Mifuko mbalimbali ya Uwekezaji wa Pamoja, ikijumuisha UTT Umoja Fund, UTT Jikimu Fund, WHI Faida Fund na WHI Reit. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya kiasi kilichowekezwa katika mifuko ya pamoja kilifikia TZS bilioni 304.98, ikionyesha ongezeko la 10.75% kutoka TZS bilioni 275.37 mwaka uliopita. Kama mwekezaji muhimu katika UTT AMIS, PSSSF imefanya uwekezaji katika Umoja Fund na Jikimu Fund ukiwa na thamani halisi ya TZS bilioni 250.36 kufikia Juni 2024. Mfuko unamiliki 57% ya WHI Reit na 63% ya WHI Faida Fund.

### Mkopo wa Mfuko

Thamani ya mikopo iliyotolewa na Mfuko ilikuwa TZS bilioni 327.93, kufikia tarehe 30 Juni 2024. Hii inaonyesha mkazo wa Mfuko katika matumizi ya kijamii na kiuchumi. Mikopo ilitolewa kusaidia miradi muhimu ya miundombinu na kuboresha viwango vya maisha vya wanachama wa SACCOS. Uwekezaji wa mali isiyohamishika, unaofikia TZS bilioni 1,163.35, unajumuisha mali za kisasa ambazo zinachangia uundaji wa ajira na maendeleo ya mijini.

"Katika mwaka wa fedha uliopita, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya TZS bilioni 8.71 kwa makampuni. Pia tulivuna TZS bilioni 19.85 kutoka kwa mikopo iliyotolewa kwa taasisi, wanachama na vikundi vya SACCOS," anasema Bw. Badru.

Katika jitihada za kutimiza moja ya vigezo muhimu vya uwekezaji wa Mfuko (matumizi ya kijamii na kiuchumi), PSSSF ilitoa mikopo kwa serikali kusaidia miradi muhimu ya maendeleo ya miundombinu. Mikopo hiyo ilikuwa muhimu katika kufadhili ujenzi wa taasisi kuu za elimu ya juu Afrika Mashariki kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Afrika (NM-AIST) na Bunge la Tanzania, miongoni mwa zingine. Kwa kufadhili miradi hii muhimu, PSSSF ilichangia sio tu katika kuboresha miundombinu ya elimu na serikali ya nchi, bali pia katika maendeleo mapana ya kijamii na kiuchumi.

### Mali Isiyohamishika

Mfuko unamiliki mali 16 za kibiashara za kisasa na mali 21 za makazi zilizoko Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma, Mtwara na Shinyanga. Jumla ya mali za uwekezaji wa Mfuko zilifikia TZS bilioni 1,163.35 kufikia tarehe 30 Juni 2024. Thamani ya hivi karibuni iliyorekodiwa na mthamini huru ilionyesha ongezeko kubwa la thamani, likifikia TZS bilioni 49.95.


Jengo la Biashara la PSSSF

Kwa kuwekeza katika mali za makazi na biashara, Mfuko unatoa suluhisho maalum kwa watu binafsi na mashirika yenye mahitaji ya makazi na nafasi za ofisi. Mali hizi za kisasa zimekuwa alama na ishara za maendeleo katika miji kadhaa ya Tanzania. Mfano mzuri ni Jengo la Biashara la PSSSF, ambalo ni jengo refu zaidi Dar es Salaam na moja ya majengo maarufu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini.

### Amna za Kudumu

Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya amana katika taasisi za kifedha ilifikia TZS bilioni 666.23, ikionyesha ongezeko kubwa kutoka TZS bilioni 497.30 zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita. Aidha, riba iliyopatikana katika kipindi hiki ilichangia TZS bilioni 50.33 kwa jumla, na hivyo kuimarisha zaidi nafasi ya kifedha ya Mfuko.

Mapato kutoka kwa uwekezaji huu yanaimarisha kwa kiasi kikubwa uwezo wa kifedha wa Mfuko.

### Hisa Zilizoorodheshwa

Mfuko umewekeza katika hisa mbalimbali zilizoorodheshwa ikiwa ni pamoja na CRDB, MCB, NICOL, NMB, SWISSPORT, TANGA CEMENT, TBL, TCC, TPCC, TOL GASES, VODACOM na TCCIA. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya thamani ya

uwekezaji katika hisa zilizoorodheshwa ilifikia TZS bilioni 628.38 ikilinganishwa na TZS bilioni 575.10 zilizorekodiwa katika mwaka wa fedha uliopita. Ongezeko la hisa zilizoorodheshwa ni kutokana na hisa za ziada zilizonunuliwa katika Tanzania Breweries Limited zenye thamani ya TZS bilioni 6.50 na TCCIA zenye thamani ya TZS bilioni 5.45 pamoja na ongezeko la bei za hisa katika DSE ikilinganishwa na mwaka uliopita.


### Hisa Zisizoorodheshwa

Mfuko umewekeza katika hisa kadhaa zisizoorodheshwa ikiwa ni pamoja na Azania Bank, Tan-Re, ZEP-RE, TCB, ACB, Ubungo Plaza, MCCCL, PPF/NHC, KLICL, Mamba Myamba Ginger Co. Ltd, WHI, Mponde Holding Co. Ltd, Nambogo Sumbawanga JV, TMX, Nguru Hills Ranch Ltd, PPF/DCC na APC Investment Centre.

Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya thamani ya uwekezaji katika hisa zisizoorodheshwa ilifikia TZS bilioni 336.32. Uwekezaji mwingine ulikuwa Mamba Myamba Ginger Co. Ltd (kiwanda cha usindikaji tangawizi), Mponde Holding Co. Ltd (kiwanda cha usindikaji chai), Nguru Hills Ranch Ltd (kiwanda cha usindikaji nyama) na KLICL (kiwanda cha utengenezaji bidhaa za ngozi). Baada ya kukamilika kwa miradi hii ya viwanda, viwanda vinatarajiwa kutoa ajira 3,480 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

### Miundombinu

Mfuko umefanya uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu kote nchini. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya thamani ya uwekezaji huu wa miundombinu ilikuwa TZS bilioni 15.07. Moja ya miradi mashuhuri ya Mfuko, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, ni ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Msamvu cha kisasa. Mradi wa Msamvu unatumika kama jukwaa muhimu la kiuchumi, likizalisha ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.




*Jumla ya thamani ya uwekezaji katika hisa zilizoorodheshwa tarehe 30 Juni 2024*

Utaratibu wa uwekezaji wa PSSSF ni kinga kwa michango ya wanachama. Asilimia kubwa ya uwekezaji huu ni wa muda mrefu. Mustakabali ni mzuri kwa uwekezaji wa sasa na ujao kadri shughuli za kiuchumi za nchi zinavyoendelea kukua.



*Majengo pacha ya PSSSF, Barabara ya Sokoine, Dar Es Salaam*

MARIE STOPES TANZANIA

# Marie Stopes inavyobadilisha maisha

**Na Mwandishi Wetu**

Jitihada za serikali kutoa huduma za kijamii zinakwamishwa kwa kiasi kikubwa na ufinyu wa rasilimali fedha, watu au vifaa. Katika mazingira hayo, taasisi binafsi huwa zina mchango mkubwa sana kuisaidia serikali kufanikisha malengo yake.

Shirika la Marie Stopes Tanzania (MST) ni moja ya taasisi binafsi ambazo zimesaidia sana juhudi za serikali kufikisha huduma za afya kwa wananchi wake.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1989, MST imesaidia sana kutoa huduma maalum za afya ya uzazi ambazo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kuleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Watanzania wa kawaida.

Kinachoifanya MST ionekane ya kipekee katika hili ni kuwa inatoa huduma zake katika maeneo mengi ya pembezoni ambayo hayafikiwi kwa urahisi na watoa huduma wengine, ikiwemo serikali.

Mara nyingi Watanzania wengi wanaoishi katika maeneo ya pembezoni, hasa akina mama, wanajikuta katika wakati mgumu katika suala la uzazi salama. Lakini wengi wa watu hawa wamesaidiwa kupitia huduma zinazotolewa maeneo yao na MST.

MST imekuwa mstari wa mbele kubadilisha maisha ya watu kupitia huduma za kipekee, za hali ya juu na nafuu za afya ya uzazi katika maeneo mengi nchini.

Chini ya kauli mbiu yake ya "dunia ambayo kila kizazi kinahitajika", MST imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha uzazi wa mpango.

Ushirikiano wake na Wizara ya Afya na TAMISEMI umehakikisha huduma hizi muhimu zinapatikana maeneo mengi nchini na hii imesaidia kuimarisha utoaji huduma na kukabiliana na matatizo yanayohusiana na uzazi kama vile kupunguza idadi ya vifo wakati wa uzazi na kuwa 104 kwa kila vizazi hai 100,000.

Mwaka jana pekee MST iliweza kuwafikia watu milioni 1.7, waliopatiwa huduma mahiri. Huduma hizo ni pamoja na mpango wa uzazi, ambapo njia mbalimbali za kupanga uzazi zilifundishwa na kusambazwa kwa wananchi.

Kupitia jitihada hizi, MST inakadiria kuwa imeweza kuzuia mimba milioni 2.6 ambazo hazikukusudiwa, matukio 723,000 ya utoaji mimba usio salama na vifo vya uzazi 3,248.

Jambo ambalo MST inajivunia ni kuwa huduma zake zinatolewa katika makundi yote katika jamii huku wale wa kipato cha chini wakipewa kipaumbele. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya waliopewa huduma na MST wanaishi chini ya mstari wa umasikini huku asilimia 58 ya hao wakiwa wanapokea huduma kwa mara ya kwanza, asilimia 56 yao hawakuwahi kupatiwa huduma kama hizo awali, na takribani asilimia tano wakiwa ni walemavu.

Aidha, asilimia 19 ya wanufaika ni vijana wadogo wenye umri wa kati ya miaka 15 mpaka 19, ikionyesha dhamira ya shirika kulifikia kundi hili kama ambavyo imepangwa kupitia Mpango wa Taifa wa Afya ya Uzazi kwa Watoto na Vijana.

Hili limesaidia kupunguza mimba za utotoni kutoka asilimia 27 mwaka 2015/16 hadi asilimia 22 mwaka 2022.

MST inatumia mikakati ya ubunifu kuwafikia vijana, ikijumuisha shughuli mbalimbali zinazokusanya watu wa rika hilo kwa wingi, programu za utoaji wa elimu katika taasisi za elimu ya juu, kliniki za mwishi wa wiki za vijana na vilabu rika zilizo shuleni na zile zilizo nje ya shule.

### Zaidi ya huduma

Katika mkakati wake, MST inajikita kuhakikisha kuwa shughuli zake zinakuwa ni zaidi ya kutoa huduma kwa jamii kwa kujikita pia kuhakikisha kuwa kinachofanyika kinalenga kudumisha haki ya kupata huduma bora za uzazi na uendelevu wake.

MST inajitahidi kuhakikisha kuwa katika utoaji wa huduma zake haisababishi unyanyapaa kwa wateja wake na kila mtu, bila kujali umri, mahali alipo au hali yake kiuchumi anapatiwa huduma katika mazingira rafiki.

Ikiwa imeajiri zaidi ya watumishi 300 wa kudumu, MST inahakikisha kuwa huduma zake zinafika maeneo yote nchini. Hilo linatekelezwa kupitia njia mbalimbali kama vile kliniki zinazotembea, kuimarisha sekta ya afya, hospitali za uzazi na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba katika eneo la afya ya uzazi.

Katika eneo hilo, MST inahakikisha kuwa upatikanaji wa vifaa tiba kwa ajili ya afya ya uzazi kama vile njia mbalimbali za uzazi wa mpango, huduma baada ya mimba kuharibika, huduma kwa wazazi na matibabu ya magonjwa yanayoambukiza kwa ngono zinapatikana kwa watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote kama moja ya haki za msingi za binadamu.

### Alama ya matumaini

Si ajabu kuwa matokeo ya yale yanayofanywa na MST yamefanikisha kupungua kwa vifo vya akina mama wakati wa kujifungua, vifo vya watoto wanaozaliwa na kuzuia utoaji mimba hatari.

MST inasimama kama alama ya matumaini kwa watanzania wengi sana ikifanya kazi na taasisi za kitaaluma kama vile Baraza la Madaktari Tanzania (MCT) na Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Akina Mama Tanzania (AGOTA) kusukuma mbele ajenda ya uzazi salama.

Hivi sasa MST inashirikiana na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kusaidia Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) ikilenga kuwatambua na kuwazawadia waandishi na wahariri ambao wamefanya vema kazi zao katika eneo la afya ya uzazi kwa kuandika habari ambazo zimeleta mabadiliko chanya katika jamii.

### Huduma nyingine

MST hivi sasa inaendesha vituo tisa katika mikoa minane, pamoja na hospitali moja ya masuala ya uzazi iliyopo eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam. MST pia inatoa huduma nyingine zisizohusiana na afya ya uzazi kama vile kuona wagonjwa wengine, huduma za ultrasound, matibabu ya magonjwa yanayosababishwa na ngono, uchunguzi wa saratani ya kizazi na maambukizi katika njia ya mkojo.

# Miaka 11 ya Azam TV na mapinduzi ya soka Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

Ni ujasiri na uthubutu tu. Hakuna jingine. Maneno hayo yanaweza kuelezea safari ya Azam Media Limited (AML) pamoja na mapinduzi iliyoleta katika sekta ya michezo nchini hasa mpira wa miguu na ngumi.

Familia ya Said Salim Bakhresa ilithubutu na ukiangalia miaka 11 iliyopita na tulipo sasa, tofauti ni kama mbingu na nchi.

Familia ya Bakhresa ilifanya ujasiri wa kizalendo kwa Taifa na nchi yao kuwekeza katika soka la Tanzania ambalo lilikuwa limepoteza mwelekeo na kukosa msisimko. Lakini, kwa upande mwingine ilikuwa ni hatari kubwa kibiashara kuwekeza katika kitu ambacho hakina uhakika.

Miaka 11 baadaye, kila kitu kimebaki kuwa historia, kila mmoja anafurahia, kila mmoja ana raha kwa sababu ya mapinduzi makubwa yaliyobadilisha kabisa taswira ya mchezo wa soka Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Kabla ya mwaka 2013, soka lilitawaliwa na wanaume tu kuanzia mashabiki pamoja na wachezaji. Leo hali ni tofauti. Mapinduzi yaliyoletwa na Azam TV yamevutia wanawake wengi viwanjani na sasa viwanjani imekuwa ni



sehemu ya mtoko kwa familia. Hilo usingeliona kabla ya mapinduzi ya Azam TV.

Nani amesema takwimu zinadanganya? Takwimu hazidanganyi. Kwa mujibu wa taasisi inayoheshimika kimataifa kwa kutunza na kutafiti kumbukumbu muhimu za kisoka duniani (IFFHS), Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa inatajwa kuwa ya sita kwa ubora na uimara katika bara la Afrika lenye nchi 54. Kwa kifupi unaweza kusema kuwa Ligi Kuu ya Tanzania Bara ipo ndani ya kumi bora Afrika. Jambo hilo lilikuwa ni ndoto za mchana kabla ya mapinduzi yaliyofanywa na Azam TV.

Uwekezaji huo mkubwa wa familia ya Bakhresa umeimarisha klabu zote zinazoshiriki ligi za Tanzania, umebadilisha maisha ya wachezaji, umeleta burudani kwa mashabiki na zaidi umeinufaisha kwa kiwango kikubwa timu za taifa za soka za Tanzania kuanzia za vijana, wanawake na wakubwa na ndio maana zimekuwa zikitamba katika mashindano mbalimbali ya Afrika.

Tuliona mwaka 2023, Simba ilitajwa kama miongoni mwa timu nane bora za Afrika ambazo zilishiriki michuano mikubwa ya Ligi ya Afrika maarufu kama Super Cup. Simba haikupata nafasi hiyo kwa bahati tu, ni kutokana na CAF kutambua ubora wa soka la Tanzania na zaidi ni ubora wa Simba ambao iliuonyesha kwa miaka ya hivi karibuni kimataifa kwa kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara nne.

Unapokuwa na klabu bora katika ligi, maana yake kuna wachezaji wazuri. Ndiyo sababu haikuwa ajabu kwamba mwaka 2019, Tanzania ilishiriki kwa mara ya kwanza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) yaliyofanyika nchini Misri, ikiwa ni mara ya kwanza baada ya miaka takribani 40 kabla ya kushiriki tena fainali hizo mwaka 2023 nchini Ivory Coast.

Klabu za Tanzania zimekuwa zikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya CAF. Yanga ilifika fainali ya Kombe la Shirikisho mwaka 2023 na mwaka huu wa 2024 ikatinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kalba ya kutolewa kimizengwe na Mamelodi Sundowns. Azam FC kwa vipindi tofauti imekuwa ikifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa pia. La kujivunia ni kuona timu ngeni nchini Tanzania, Namungo na Coastal Union nazo zikishirikishi mashindano hayo ya CAF kwa viwango tofauti.

Mafanikio haya hayapo kwenye soka pekee. Mchezo wa ngumi, umepata umaarufu mkubwa nchini kiasi kwamba nchi jirani zimeanza kualika mabondia kutoka Tanzania ili kwenda kuzimua mchezo huo katika nchi zao. Kwa ujumla mchezo huu ulipotea, lakini sasa maisha ya mabondia yamebadilika kutokana na malipo ya kuridhisha huku ajira kwa vijana zikiongezeka.

Hadithi ni hiyohiyo kwenye tasnia ya filamu ambayo ni kama ilikuwa ipoipo tu, lakini sasa wasanii wana maisha mazuri wakiwa na uhakika wa maisha kutokana na viwango vizuri wanavyolipwa na Azam TV kwa kazi zao.

Miaka 11 iliyopita, kwenye vibandaumiza, baa na maeneo mengine wanakoonesha mipira, ilikuwa rahisi kuona watu wakitazama mechi ya timu ya Ulaya wakati kuna timu za Tanzania zinacheza muda huohuo. Na ukitazama watazamaji, wengi zaidi walikuwa wamevaa jezi za timu za Ulaya kuliko za nyumbani.

Ilikuwa si rahisi kuona mtu anafuatilia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakati kuna mechi ya Ligi Kuu England inayochezwa muda huo. Hilo halipo tena.

Haya ndiyo mazingira ambayo kampuni za Bakhresa ziliyakuta wakati wakitaka kuanza kuwekeza. Ligi iliyokosa msisimko, watu wasiokwenda kutazama mpira viwanjani, mashabiki wasiopenda timu za nyumbani kama wanavyopenda za nje na kampuni za nje zinazotaka kuhodhi soko la televisheni za kulipia kwa gharama yoyote.




Kwa hakika, Tanzania ina bahati kwamba wawekezaji wa Bakhresa ni wazalendo na wana mapenzi makubwa na nchi yao. Aina ya uwekezaji uliofanywa unaweza kufanyika na mtu mwenye mapenzi na uchungu kwa nchi yake na si suala la kuwa na fedha za kufanya hivyo pekee.

Kabla ya mwaka 2013, ilikuwa vigumu kwa mechi ya mpira wa miguu kujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam wenye uwezo wa kujaza mashabiki 56,000. Sasa, Simba, Yanga na mechi za Taifa Stars zinajaza uwanja bila shida yoyote.

Yote haya yamewezekana kwa sababu ya ushirikiano mzuri baina ya Azam Media Limited (AML), Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), klabu na wadau wengine muhimu kwenye soka letu. Haitakuwa haki kusema kwamba ni Azam Media pekee yao ndiyo wamefanikisha safari hii.

Hakuna shaka kwamba Ligi Kuu Tanzania pengine inaendeshwa katika kiwango tofauti kabisa kulinganisha na jirani zetu kwenye eneo hili la Afrika Mashariki. Ligi yetu sasa inachukuliwa kuwa mfano wa kuigwa miongoni mwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

.

Sisi kupitia AML tumeonyesha ustahimilivu na uwezo wa kiwango cha juu huko nyuma na tuko tayari kutekeleza kwa uadilifu mkubwa matarajio kwenye mkataba unaofuata kwa kipindi cha miaka 10 ijayo. Lengo letu ni kufanya ligi yetu izidi kuwa miongoni mwa zilizo bora – kama si bora zaidi, kuliko nyingine barani Afrika.

Hiyo ndiyo ndoto yetu. Hii ndiyo ahadi yetu kwenu.

Inafurahisha kuona watu wakipita mitaani wakiwa wamevaa fulana za Simba, Yanga, Azam na klabu zao nyingine wakiwa na furaha tele. Hilo halikuwapo miaka 11 iliyopita.


UDANI HIZI
NDUKI
G'O
azamtv



# Bunge imara huzaa serikali inayowajibika

**Na Mwandishi Wetu**

Madaraka ya kuongoza nchi yamegawanywa kwenye mihimili mitatu mikuu, ambayo hutambulika kama mihimili ya madaraka ya dola. Mihimili hii ni Serikali Mahakama na Bunge. Kila muhimili una mamlaka yake ya kikatiba yaani mgawanyo wa mamlaka ya dola. Katika kutekeleza majukumu hayo, mihimili hii huwa inadhibitiana. Kila muhimili una kiongozi wake mkuu, serikali inaongozwa na Rais, Bunge linaongozwa na Spika na Mahakama inaongozwa na Jaji Mkuu.

Dhana hii ya mgawanyo wa madaraka ya dola ndiyo pia imeweka msingi wa mihimili hii kudhibitiana katika utekelezaji wa majukumu yake; Bunge hutunga sheria, serikali hutekeleza sheria iliyotungwa na mahakama hutafsiri sheria husika. Kila muhimili ni lazima utekeleze majukumu yake kama yalivyoanishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo, katika kutelekeza majukumu yake vyombo hivi vya mamlaka ya dola haviingiliani, ndiyo maana kwa mfano unaweza kusikia mtendaji wa serikali akisema jambo hilo siwezi kulizungumzia kwa sababu kuna kesi iko mahakamani, au unaweza kusikia mbunge akisema jambo hilo haliwezi kujadiliwa bungeni kwa sababu kuna kesi iko mahakamani.

Dhana ya mgawanyo wa madaraka ndiyo inawapa wananchi unafuu wa kuichagua serikali wanayoitaka, lakini hata baada ya kuchagua serikali kupitia sanduku la kura wanakuwa na haki na uhuru wa kuisimamia serikali kupitia Bunge.

Ni kwa msingi huo Bunge linakuwa ni chombo muhimu sana cha uwakilishi wa wananchi. Bunge lina wajibu wa kutunga sheria, kuisimamia na kuishauri serikali kama ilivyoanishwa kwenye ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muunango wa Tanzania kwamba: "Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bunge ndilo lenye uwezo wa kuifanya serikali ifanye kazi zake kama inavyotakiwa kwa sababu lina uwezo wa kuiadabisha serikali. Kwa maelezo mengine ni kwamba kama serikali haiwajibiki sawasawa chombo cha kuulizwa ni Bunge.

Katika historia ya utendaji wa Bunge yalipata kuwapo maamuzi mengi ambayo yalisababisha mawaziri kadhaa kufutwa kazi kwa sababu Bunge lilitimiza wajibu wake wa kusimamia serikali sawasawa. Mfano mmojawapo ni ule wa ripoti ya Bunge ya uchunguzi kuhusu Sakata la Operesheni Tokomeza Ujangili la mwaka 2014 ambayo ilibaini kuwepo vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mauaji, utesaji na udhalilishaji vikidaiwa kutendwa na watekelezaji wa operesheni hiyo.

Kutokana na ripoti hiyo, mawaziri wanne walijiuzulu nafasi zao kutokana na wizara walizokuwa wanaongoza kuhusika katika operesheni hiyo. Hawa walikuwa ni aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Khamis Kagasheki; aliyekuwa Waziri wa Mambo ya ndani, Dk. Emmanuel Nchimbi; aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Shamsi Vuai Nahodha; na Dk. Mathayo David Mathayo aliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mfano huu ni mmoja tu miongoni mwa mingine mingi ambayo Bunge kwa nyakati tofauti limefanya hivyo kuamsha uwajibikaji serikalini, hata hivyo tukio hili linabakia kuwa historia ya kipekee kwa Bunge la Tanzania kwa mawaziri wengi kwa wakati mmoja kujiuzulu nyadhifa zao kwa sababu ya kazi ya uchunguzi ya Kamati ya Bunge.

Bunge pia lina uwezo wa kumwondoa Rais madarakani kama linavyopewa madaraka hayo na ibara ya 46 A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge lina sehemu mbili yaani wabunge na Rais (Parliament) na wabunge peke yao (National Assembly). Bunge pia lina madaraka ya kumwondoa madarakani Waziri Mkuu kulingana na masharti ya Katiba ibara ya 53 A.

Ni dhahiri Bunge ni chombo kikubwa cha madaraka, ndicho chombo kimsingi kinachopaswa kusimamia uwajibikaji wote katika nchi kwa sababu serikali inawajibika bungeni. Ni kwa msingi huu, wananchi wanapaswa kuliangalia Bunge kama chombo kinachobeba macho na masikio yao, lakini pia na makucha yao katika kufanya mambo yaende vyema.

Bunge ndilo kikatiba lina madaraka ya kupitisha bajeti ya serikali, hakuna kodi yoyote ambayo serikali inaweza kuanzisha bila kupata ridhaa ya Bunge, kwa msingi huo, wananchi wanayo haki ya kuwauliza wabunge juu ya mambo yote ya uendeshaji wa nchi yao. Katika mfumo ambao Bunge linafanya kazi zake sawasawa, serikali inawajibika kwa nguvu zote.

Ndiyo maana kwa kutambua nguvu, madaraka na wajibu wake kwa umma, Bunge lina programu ya kuwafikia wananchi ili watambue chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi kinafanya nini.

Mbali na Bunge kurusha vikao vyake mubashara kwenye runinga ili kuwapa wananchi fursa ya kufuatilia mambo yanayojadiliwa na kuamuliwa kwa ajili ya ustawi wa nchi, pia kila mwaka wa fedha ina utaratibu wa kwenda kwa wananchi kutoa elimu ya uraia. Elimu hii hutolewa kwa kutumia maofisa wa Bunge ambao hukutana na vikundi mbalimbali katika jamii kwa ajili ya kutoa elimu hiyo.

Elimu ya uraia hutolewa mara tatu kila kwenye mzunguko wa mwaka wa fedha, kwa sasa Bunge linaendelea na programu hiyo katika mikoa ya Katavi na Kigoma, ambako kupitia kwa maofisa elimu wa serikali huandaa ratiba ya kukutana na wanafunzi katika shule za msingi, sekondari na vyuo, ili kuwajengea uelewa wa majukumu ya Bunge kama yalivyoanishwa kikatiba.

Mbali ya programu hizi za kuwafuata wanafunzi shuleni na vyuoni, pia Bunge linaalika na kupokea wanafunzi kufika bungeni kujifunza kwa kuona jinsi shughuli za Bunge zinavyoendeshwa. Kila mikutano ya Bunge inayofanyika kumekuwa na makundi ya wanafunzi kutoka shule mbalimbali



kujionea jinsi Bunge linavyoendesha shughuli zake katika kutunga sheria, kupitisha bajeti na taratibu nyingine za kuisimamia serikali kama wabunge kuuliza maswali na maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu ambaye kimsingi ni Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Kwa kuwa wananchi wote hawawezi kwenda Bungeni, dhana ya demokrasia ya uwakilishi ndiyo inatawala kwa kuchaguliwa kwa watu wachache (wabunge) kuwakilisha wananchi, ama kupitia majimbo ya uchaguzi, au viti maalum, au wabunge wa kuteuliwa na Rais ambao kisheria hawazidi 10. Hivyo basi, kila mwananchi anao wajibu wa kufuatilia kwa makini mbunge kama waliyemchagua anatekeleza wajibu wake wa uwakilishi. Utambuzi huu utawapa fursa wananchi kuamua juu ya mwakilishi wao kwa kipindi kingine cha uchaguzi.

Uamuzi wa kuonyesha shughuli za Bunge mubashara ni vema uchukuliwe na wananchi kama njia ya wao kupima uwajibikaji wa mbunge wao awapo bungeni, lakini pia kupima kama kweli anayofanya yana uwakilishi wao au la. Utaratibu huu unasaidia kujenga uwajibikaji wa mbunge kwa wapigakura wake.

> *Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bunge ndilo lenye uwezo wa kuifanya serikali ifanye kazi zake kama inavyotakiwa kwa sababu lina uwezo wa kuiadabisha serikali.*

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# Zanzibar Leo lilivyowarejeshea wananchi matumaini

**Na Mwandishi Wetu**

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar ni wachapishaji wa Zanzibar Leo, Zanzibar Mail na Zaspoti, vyombo vya habari mahususi vya serikali kwa ajili ya kusambaza taarifa na sera za serikali kwa umma.

Katika hali ya kawaida mtu angeliweza kudhani vipo kwa ajili ya kusifu tu. Uhalisia hauko hivyo, utendaji wake umeamsha uwajibikaji mkubwa visiwani humo na kusaidia kero mbalimbali za wananchi kupata majawabu.

Orodha ya mafaniko ya magazeti haya kuwarejeshea wananachi matumaini ni ndefu, hapa tunashuhudia maeneo kadhaa ambayo shida zilizokuwa zinaikabili jamii na hata mtu mmoja mmoja zimeibuliwa na kufanyiwa kazi na mamlaka za kiserikali.

Miongoni mwa maeneo hayo ni sekta ya afya. Gazeti la Zanzibar Leo liliripoti habari ya tabia sugu ya wahudumu wa afya wa kituo cha Mkanyageni, wilaya ya Mkoani ambao walijigeuza miungu watu kwa kufika kazini kwa kuchelewa na kuondoka mapema kabla ya muda wa saa kazi kwisha, hivyo kusababisha hali ya utoaji wa huduma mbovu kwa wagonjwa.

Kutokana na habari hiyo kusomwa na mamlaka zinazohusika na sekta ya afya, ufuatiliaji wa utendaji wa wahudumu hao uliongezeka, na sasa kufika kazini mapema na kuondoka muda wa kazi unaokubalika kisheria umekuwa ni utamaduni, jambo ambalo lilikuwa limezikwa siku nyingi.

Katika eneo hilo la afya wajawazito waliokuwa wanafika Kituo cha Afya cha Wesha wilaya ya Chakechake kujifungua, walilazimika kubeba ndoo za maji kutokana na kituo hicho kutokuwa na huduma ya maji. Baada ya habari hizo kuibuliwa na gazeti la Zanzibar Leo likielezea adha kwa wajawazito hao, Wizara ya Afya ilitafuta fedha na kuchimba kisima kwenye kituo hicho, hivyo kuhitimisha adha ya ukosefu wa huduma ya maji kwa wazazi waliokuwa wanajifungulia kituoni hapo.

Darubini ya Zanzibar Leo kuibua kero za jamii haikuishia kwa taasisi za umma tu, kwani habari iliyoibuliwa kwenye Kijiji cha Shumba Vyomboni wilaya ya Micheweni ikimulika adha aliyokuwa anapata mwanamke mlemavu aliyekuwa anaendesha madrasa nje huku yeye mwenyewe akiwa hana makazi ya maana, ilisukuma wasamaria wema kuchukua hatua za kumjengea madrasa ya kisasa, nyumba ya kuishi pamoja na kumpatia baiskeli ya kiti-mwendo.

Habari za magazeti hayo pia ziliwapatia tabasamu wakazi wa Kijiji cha Wingwi wilaya ya Micheweni, ambao walikuwa wanataabika kutokana na maji ya bahari kujaa na kuziba njia waliyokuwa wanatumia kupita kwenda katika kijiji kingine kupata huduma mbalimbali. Kujaa kwa maji hayo kuna husianishwa na uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo, baada kilio cha adha ya wananchi hao kukatiwa mawasiliano kuibuliwa na magazeti hayo, Taasisi ya Serikali ya Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) ilitenga fedha na kujenga daraja la mbao eneo hilo, hivyo kuondoa kero hiyo. Ukosefu wa daraja katika eneo hilo ulikuwa umeathiri wanafunzi kwenda shule, pia na wananchi wengine.

Lipo tukio la mwanamke mmoja aliyezalishwa watoto watano, akatelekezwa na watoto bila huduma yoyote. Mwanamke huyo alishindwa kuwahudumia mwenyewe, pia hakuweza kuwapeleka shule watoto hao. Habari hizi zilipoibuliwa, ziliamsha moyo wa huruma kwa watu wenye utu, matokeo yake familia yake ilijengewa nyumba ya kisasa ya kuishi na watoto wake wakarejeshwa shule.

Kama kuna watu wanasubiri kwa hamu tabasamu kubwa ni wakazi wa kisiwa cha Tumbatu kinachojumuisha vijiji vitatu, lakini kuna kituo kimoja tu cha afya. Adha ya wananchi hawa ilipewa kipaumbele kwenye gazeti la Zanzibar Leo hasa likiangazia jinsi wananchi wa Kijiji cha Tumbatu Bomani ambao hawana huduma ya afya kijijini hapo, wanavyotaabika kuvuka bahari kufuata huduma hiyo ama katika kituo cha Afya Kidoti wilaya ya Kaskazini A, Unguja au kwenda Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Kilio cha wananchi wa vijiji hivi kilifika masikioni mwa serikali na sasa imetangaza kuwa inakwenda kujenga hospitali kubwa kisiwani Tumbatu ambayo itahudumia kwa uhakika wakazi wa vijiji vyote, hivyo kuwaondolea kero ya kuvuka bahari kufuata huduma za afya.


Ukurasa wa Zanzibar Leo wa Kero, ambao ni maalum kwa ajili ya kuangazia kero mbalimbali katika jamii na kuzitoa kwa ajili ya kuibua uwajibikaji, umekuwa na mafanikio makubwa pia katika kuleta mabadiliko katika utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa umma wa ngazi mbambali.

Mathalan, zilipata kutolewa picha za maji yanayovuja ovyo na kupoteza rasilimali hiyo muhimu kwa binadamu; wenye mamlaka za maji walichukua hatua ya kwenda kurekebisha mabomba yaliyokuwa yanavuja. Kumekuwa na picha zinapigwa kuonesha magari yaliyoegeshwa kwenye barabara za watembea kwa miguu, nako hatua mahususi zimechukuliwa kuzuia uegeshaji wa magari hayo.

Magazeti hayo yamekuwa na habari nyingi kuhusu mfumo wa utoaji wa haki, kama kesi za udhalilishaji wa kijinsia kutokupewa umuhimu na pengine adhabu nyepesi kwa watuhumiwa wa kesi zinapofikishwa mahakamani, lakini sasa kumekuwa na hukumu nzito zikiwapo vifungo vya muda mrefu.

Katika eneo la haki, pia kuna suala la muhali ambalo limekuwa sugu viswani humo kwa watu kuchelea kuripoti matukio ya ubakaji na udhalilishaji, lakini baada ya kampeni ya kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kutoa taarifa sasa watu wengi wanaripoti. Hali hii inaelezwa kuwa imechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa matukio ya ubakaji visiwani humo.

Eneo jingine muhimu ambalo magazeti hayo yalipambana kufichua ni pamoja na kukithiri kwa tabia ya baadhi ya wafanyabishara eneo la Darajani, Zanzibar ya kudhalilisha na kuwatunga mimba wanafunzi katika shule za Darajani na Vikokotoni. Kampeni ya muda mrefu ya vyombo hivyo vya habari zilionesha kwamba eneo la Darajani lilikuwa hatarishi kwa kuwa wanafunzi walikuwa wanakutana kwa karibu mno na wakware hao, hatimaye serikali iliamua kuzifunga shule hizo na kuzihamishia maeneo mengine.



Zanzibar Airports Authority

# ZAA yarekodi mafanikio lukuki

Umewahi kuona taasisi ambayo inapata mafanikio katika lengo lake kiuchumi kwa asilimia zaidi ya 250? Ni taasisi chache sana zinapata mafanikio hayo na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) ni moja ya taasisi kama hizo.

Katika kipindi cha miaka mitatu tu tangu mwaka 2020 hadi 2023 ZAA ilifanikiwa kuongeza idadi ya abiria wanaoingia na kutoka Zanzibar kupitia viwanja vya ndege toka 840,599 hadi abiria 2,131,406 sawa na ongezeko la asilimia 253!

Hii inatokana na uongozi madhubuti wa Mamlaka hiyo ukisaidiwa na sera na sheria wezeshi zilizowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Ongezeko la abiria limeiwezesha pia ZAA kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 11.6 mwaka 2019/20 hadi kufikia shilingi bilioni 40.2 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 95. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa kipimo chochote kile.

ZAA imethibitisha uwezo wake wa kuhimili vishindo katika biashara inayoisimamia kwani wakati wa janga la Uviko-19, idadi ya abiria ilipungua kutoka 1,609,235 mwaka 2019 hadi kufikia abiria 840,599 mwaka 2020 wakati wa Uviko -19.

Lakini baada ya janga hilo, Mamlaka iliingia kazini na kuwezesha kupandisha idadi ya abiria hadi kufikia abiria 2,131,406 mwaka 2024.

Kutokana na uboreshaji wa mazingira ya biashara, ZAA pia ilifanikiwa kushawishi mashirika ya ndege kuanza kuvitumia viwanja vya Zanzibar ambapo mashirika mapya ya ndege yakwemo Edelweis na Eurowings kutoka Ujerumani, Etihad kutoka Falme za Kiarabu (UAE), Fly Saff Air kutoka Afrika Kusini, Air France kutoka Ufaransa, High Fly kutoka Ureno, Jambo Jet na World to Fly yalianza kutua Zanzibar.

Hili ni ongezeko la asilimia 26 kwa upande wa mashirika ya ndege yanayotua Zanzibar kutoka mashirika 68 mwaka 2020 hadi mashirika 86 mwaka 2023.

Wadau hao walivutika pia kutokana na ZAA kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege.

Ukaguzi uliofanywa na wakaguzi kutoka shirika lenye dhamana ya usiamamizi wa usafiri wa anga duniani (ICAO) kwa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Aman Karume (AAKIA), kiliiwezesha TAA kupata alama “A” kwenye

masuali ya ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege.

Maboresho ya miundombinu yaliyofanyika Abeid Amani Karume International Airport (AAKIA), yaliishawishi kampuni ya Emirate Leisure kuingia kuendesha biashara katika jengo jipya la kuhudumia abiria la TB3.

Kampuni hiyo haikuwa peke yake iliyofanya hivyo kwani kampuni ya Dnata inayojishughulisha na shughuli za uhudumiaji wa ndege, nayo ilianza kufanya kazi katika uwanja huo.

“Kupitia kampuni hizi uwanja wa ndege wa AAKIA umeweza kupata tuzo ya kimataifa inayohusiana na mabadiliko ya huduma bora za chakula na vinywaji kutoka “Airport Food & Bevarage (FAB)+ Hospitality Conference & Awards kwenye mkutano wake uliofanyika Bangkok nchini Thailand,” inasema taarifa ya ZAA.

Aidha, AAKIA pia ilitunukiwa cheti cha usafirishaji wa mizigo “RA3” kutoka uwanja wa AAKIA kwenda nchi za Ulaya.

**Maboresho**

Lakini mafanikio hayo hayajaifanya ZAA ijione kuwa imeshafika mahali ilipokuwa inapahitaji. Bado inaendelea na mikakati kabambe ya kuboresha zaidi huduma kwa lengo la kuwavutia wadau wengi zaidi.

Mathalani, ZAA imeingia makubaliano na Kampuni ya SEGAP ya Ufaransa inayosaidia Menejimenti ya ZAA katika huduma za uendeshaji viwanja vya ndege ikiwa na lengo la kuimarisha utoaji huduma za anga nchini.

Pia, ZAA imeanza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa jengo la nne la abiria (TB4) katika kiwanja cha AAKIA ambapo ripoti ya awali tayari imeshakamilika na kwa sasa Serikali ipo katika hatua za kukamilisha utaratibu wa upatikanaji fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

ZAA imefanikiwa kuimarisha shughuli za usafiri wa anga katika kisiwa cha Pemba pia ambako taratibu za ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Pemba zimeshaanza kutekelezwa.





*“Katika kipindi cha miaka mitatu tu tangu mwaka 2020 hadi 2023 ZAA ilifanikiwa kuongeza idadi ya abiria wanaoingia na kutoka Zanzibar kupitia viwanja vya ndege toka 840,599 hadi abiria 2,131,406 sawa na ongezeko la asilimia 253!”*

Uboreshaji wa Uwanja wa Ndege Pemba umehusisha pia uwekaji wa taa za kuongozea ndege katika njia ya kurukia ndege.

Kwa muda mrefu kiwanja hicho kilikuwa hakifanyi kazi usiku kutokana na njia ya kurukia ndege kutokuwa na taa na tatizo hilo sasa linaelekea kumalizwa.

Uwanja huo pia unajengewa uzio wa zege katika maeneo ambayo yalikua yakiweza kuhatarisha usalama. Uzio huo utaimarisha usalama kwani utazuia wanyama na watu wasiohusika na shughuli za uwanja huo kuingia kwenye eneo la uwanja.

**Miradi inayoendelea**

Kuna miradi kadhaa ambayo inalenga kuboresha shughuli katika viwanja vya ndege Zanzibar ambayo inaendelea.

Mradi mmojawapo ni ujenzi wa jengo jipya la pili la kuhudumia abiria (TB2).

Mradi huu ulibuniwa kufuatia malalamiko ya uchakavu wa miundominu kwenye jengo la pili la Abiria (TB2).

Kwa mujibu wa ZAA, jengo litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 1,300,000. Ujenzi wa jengo hilo umeshafika asilimia 35.

Pia kuna mradi wa ujenzi wa ukumbi wa kusafiria wa Viongozi Wakuu (VVIP) na pia ukarabati wa kumbi za wageni mashuhuri na eneo kwa ajili ya ndege binafsi katika jengo la Terminal 1.

“Ujenzi wa VVIP umefikia katika hatua ya kuthibitishwa kwa michoro ili kuendelea na hatua za ujenzi,” inasema taarifa ya ZAA.

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Hivi ndivyo EWURA CCC inavyogusa maisha yako

**Na Lugiko L. Lugiko, Dodoma**

Katika ulimwengu wa sasa, ambapo huduma za nishati na maji ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, uwepo wa chombo cha kuwakilisha watumiaji wa huduma hizo na kuhakikisha kuwepo kwa watumiaji wenye maarifa na uelewa wa masuala yahusuyo huduma hizo ni jambo la muhimu sana.

Ukweli huu ndio uliozaa uwepo wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji zinazodhibitiwa na EWURA, yaani EWURA CCC. Baraza hili lilianzishwa chini ya Kifungu cha 30 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 kwa ajili ya kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

## Majukumu ya Baraza

Baraza linayo majukumu muhimu ya kuwa sauti ya watumiaji kwa kufanya mawasilisho, kutoa maoni, na kushauriana na EWURA, Waziri anayesimamia EWURA kwa wakati huo, pamoja na mawaziri wanaosimamia sekta zinazodhibitiwa na EWURA. Pia linashirikiana na wadau mbalimbali kwa kushauriana nao ikiwemo serikali na wenye viwanda katika uboreshaji wa huduma hizo. Sambasamba na hilo, Baraza lina jukumu la kukusanya na kusambaza taarifa muhimu zenye maslahi kwa watumiaji wa huduma hizi, kuunda kamati za watumiaji za kimikoa na za kisekta na kushauriana nazo.

## Mbinu Mbalimbali za Utetezi wa Watumiaji

EWURA CCC imekuwa ikitumia mbinu kadhaa ili kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa, miongoni mwake ikiwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa watumiaji, elimu kuhusu kanuni na sheria zinazohusu huduma za nishati na maji, matumizi sahihi ya huduma na utunzaji wa miundombinu, pamoja na elimu kuhusu usomaji wa mita za maji na umeme. Elimu hii hutolewa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano ya hadhara, semina, na maonesho. Njia zingine ni pamoja na kuwakilisha watumiaji katika michakato ya mabadiliko ya bei za huduma zinazodhibitiwa na kuwasaidia watumiaji kutatua malalamiko katika huduma hizo.

Akizungumza na jarida hili, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alisema kuwa “Dira yetu ni kuwa na watumiaji wenye uwezo na maarifa kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa, jambo ambalo litasadia kuboresha huduma, na kuongeza uwajibikaji kwa pande zote, yaani mtoa huduma na mtumiaji.”

## Mafanikio ya EWURA CCC

### Tathmini ya miaka minne

Ripoti za kiutendaji za kipindi cha 2020/21 hadi 2023/24 zinaonesha kuwa EWURA CCC imepiga hatua kubwa katika kutekeleza majukumu yake ambapo imefanikiwa kuandaa mawasilisho zaidi ya 30 kwa EWURA, yaliyolenga mabadiliko

mbalimbali hususani katika kuwa na bei za huduma ambazo ni nafuu kwa watumiaji. Aidha, Baraza limeandaa na kutekeleza programu za uelimishaji 2,840, likiwafikia watumiaji 708,975 Tanzania bara. Kupitia vyombo vya habari kama radio na televisheni, Baraza limefanya programu 791 kwa ajili ya kueneza taarifa muhimu ambazo zilifikia maelfu ya watumiaji.

Akizungumzia kuhusu ufanisi wa kazi za Baraza, Bi. Lupimo alisema kuwa Baraza limekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa linawafikia watumiaji wengi zaidi na kuwajengea uelewa na uwakilishi katika huduma wanazotumia. "Tumejizatiti kuhakikisha kwamba kila sauti ya mtumiaji inasikika, na tunakuwa msaada kwa watumiaji, na katika kipindi hiki tumesaidia utatuzi wa malalamiko 16,795 ya watumiaji," alisema Bi. Lupimo. Katika kutekeleza majukumu yake, EWURA CCC imegusa maisha ya watumiaji wengi waliokuwa na changamoto ambapo msaada wa Baraza uliacha furaha na kumbukumbu zisizosahaulika katika maisha yao.

Bi. Husna Abdalah, mkazi wa mkoani Tanga, alikumbana na deni kubwa la maji la shilingi milioni 2.6. Hapo awali, ankara yake ya kila mwezi ilikuwa shilingi 120,000/=. Hata hivyo, alishangazwa na ongezeko kubwa la ankara lililosababisha deni kubwa. Bi. Husna alijaribu kufuatilia malalamiko yake kwa zaidi ya miezi minane bila mafanikio. Baada ya kusikia kuhusu EWURA CCC kupitia redio, aliwasilisha lalamiko lake. EWURA CCC ilichukua hatua ya haraka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga (Tanga UWASA), na baada ya uchunguzi, ilibainika kasoro katika mfumo wa ankara. Hatimaye, deni lake likapunguzwa kutoka shilingi milioni 2.6 hadi shilingi 140,000/= tu. "Nashukuru EWURA CCC kwa kunisaidia. Bila wao, nisingeweza kupata haki yangu," alisema Bi. Abdalah.

Bw. Bakari Athumani, mkazi wa mtaa wa Chonjo, mkoani Tanga alikabiliwa na deni la umeme la shilingi milioni 4.1. Hali hii ilisababisha huduma yake ya umeme kusitishwa. Bw. Bakari aliwasiliana na TANESCO mara kadhaa, lakini hakufanikiwa kupata msaada. Alipopata ushauri kutoka kwa ndugu yake kuhusu EWURA CCC, aliwasilisha lalamiko lake kwa Baraza. Baada ya uchunguzi, EWURA CCC ilishirikiana na TANESCO kupitia vikao vya usuluhishi vilivyoitishwa na EWURA, na hatimaye huduma ya umeme ilirejeshwa na deni lake likarekebishwa.

"Kwa kweli, EWURA CCC wamekuwa msaada mkubwa kwangu. Sasa nimepata haki yangu na huduma yangu ya umeme imerejeshwa," alisema Bw. Athumani.

Bw. Abdulsamadi Sharif, mfanyabiashara wa samaki, alipata hasara kubwa baada ya hitilafu ya umeme kusababisha kuungua kwa jokofu lake. Hasara hii iliathiri biashara yake na kusababisha kupoteza bidhaa za samaki. Pamoja na juhudi zake za kufuatilia tatizo hilo kwa TANESCO, hakupata suluhisho. Aliposhauriwa na mwenyekiti wa mtaa wake kufika EWURA CCC, aliwasilisha lalamiko lake. EWURA CCC ilimwelekeza namna sahihi ya kutatua lalamiko na hatimaye akafungua malalamiko rasmi dhidi ya TANESCO kwenda EWURA na baada ya uchunguzi wa kina, TANESCO waliamriwa na EWURA kumfidia kiasi cha shilingi milioni mbili kwa hasara aliyopata, pamoja na gharama za jokofu lake.

"Nimepata fidia kwa msaada wa EWURA CCC. Bila wao, biashara yangu ingekuwa imeathirika zaidi," alieleza Bw. Sharif. Ni wazi kwamba kwa mtumiaji wa huduma za nishati na maji kuna faida kubwa kuitumia EWURA CCC kwani kunaleta manufaa makubwa kwake kwa kupata uwakilishi makini na taarifa sahihi zinazohusu huduma za nishati na maji.

Kwa kuzingatia kauli mbiu yake, "Huduma Bora ni Haki Yako," EWURA CCC ni mshirika wa kuaminika wa kila mtumiaji wa huduma za maji na nishati nchini Tanzania.

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# TIC Yashinda Tuzo ya Kifahari

## Yazindua Mwaka wa Kitaifa wa Uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

Pengine siyo wengi wanajua hili, lakini Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepongezwa kwa kazi yake bora ya kukuza uwekezaji barani Afrika! Katika Mkutano wa Mwaka wa Uwekezaji (AIM) 2024 uliofanyika Abu Dhabi tarehe 8 Mei, 2024, TIC ilipata kutambuliwa kwa juhudi zake. Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, alipokea tuzo hiyo kwa niaba ya TIC. Tuzo hii inaonyesha hadhi inayoongezeka ya Tanzania kama eneo bora la uwekezaji Afrika Mashariki.

Dkt. Kida alisisitiza kuwa tuzo hiyo inaakisi dhamira ya serikali ya kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza imani ya wawekezaji. "Tuzo hii inaimarisha imani miongoni mwa wawekezaji, na kama serikali, hususan Ofisi ya Rais inayohusika na Mipango na Uwekezaji, tutaendelea kuvutia uwekezaji ili kuunda ajira na kukuza uchumi," alisema wakati wa mahojiano na vyombo vya habari baada ya kupokea tuzo hiyo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Bw. Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, alielezea mipango muhimu kama vile motisha maalum kwa sekta na ushirikiano ulioboreshwa na wadau, ambayo imechangia hadhi ya Tanzania kama eneo la uwekezaji lenye ushindani duniani. "Kutambuliwa huku kunaashiria kuibuka kwa Tanzania kama kitovu cha uwekezaji kinachoongoza Afrika Mashariki, sambamba na Mwanaumengo mapana ya kiuchumi yanayolenga kufikia hadhi ya kipato cha kati na ukuaji endelevu," alisema Teri.

### Usajili wa Miradi ya Uwekezaji TIC

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 707, ikilinganishwa na miradi 369 iliyosajiliwa mwaka wa fedha uliopita. Miradi hii ina thamani ya Dola za Marekani bilioni 6.561, ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 5.394 mwaka wa fedha 2022/2023. Miradi hii inatarajiwa kuzalisha ajira 226,585, ikilinganishwa na ajira 53,871 mwaka uliopita. Kati ya miradi hiyo, asilimia 38.19 inamilikiwa na Watanzania, asilimia 42.86 ni ya wageni, na asilimia 19.38 ni ya ubia kati ya Watanzania na wageni.

### Usajili Kisekta

Sekta ya uzalishaji viwandani inaongoza kwa kuwa na miradi 313 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.462, ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji yenye miradi 128 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.035. Sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara inashika nafasi ya tatu kwa kuwa na miradi 76 yenye thamani ya Dola

za Marekani bilioni 1.079, ikifuatiwa na sekta ya utalii yenye miradi 75 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 349.40. Sekta ya kilimo inashika nafasi ya tano kwa kuwa na miradi 56 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 710.02.

### Matokeo ya Uhamasishaji na Ufanikishaji Uwekezaji

Serikali imeendelea kuboresha Kituo cha Utoaji Huduma za Mahali Pamoja kilichoko TIC kwa kuanzisha mfumo wa kusajili miradi ya uwekezaji kwa njia ya mtandao. Mfumo huu unaruhusu wawekezaji kusajili miradi yao mahali popote duniani ndani ya siku moja hadi tatu. Pia, kituo kimeanzisha huduma za haraka kupitia Premier Service Centre ambapo mwekezaji anaweza kusaidiwa kupata vibali na usajili kwa haraka zaidi ndani ya masaa 24.

### Sheria Mpya ya Uwekezaji

Sheria mpya ya uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022 ina uwezo wa kuvutia uwekezaji zaidi nchini. Sheria hizi zinatoa vivutio vya kuvutia na mifumo ya kodi ili kuhamasisha uwekezaji wa kigeni na wa ndani. Vivutio hivi ni pamoja na msamaha wa kodi kwa wawekezaji wa kawaida na wa kimkakati, upunguzaji wa ushuru wa forodha, na vivutio vingine vya kifedha vinavyofanya uwekezaji nchini Tanzania kuvutia zaidi. Kiwango cha chini cha USD 50,000 kwa wawekezaji wa ndani kinatarajiwa kuvutia usajili zaidi wa wawekezaji wa ndani.

### Uhamasishaji Uwekezaji

TIC imeanzisha kampeni mbalimbali za uhamasishaji uwekezaji, ikiwemo kampeni iliyoanza mwezi Agosti 2023 ikihamasisha wawekezaji wa ndani kuja kusajili miradi yao na kituo cha uwekezaji. Hili limeleta ongezeko kubwa la miradi kwa takribani asilimia 106.11 ikilinganishwa na miradi ya Watanzania iliyosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2022/2023.

Kampeni hii inawahimiza wajasiriamali wa Kitanzania kusajili miradi yao ya uwekezaji, ikiwapa fursa ya kusikia hadithi za mafanikio kutoka kwa Watanzania wenzao ambao wamenufaika na vivutio vya TIC. Mpango huu unatarajiwa kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayomilikiwa na Watanzania, hivyo kuwaunganisha zaidi katika uchumi wa taifa.



*Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura (kushoto), akimkabidhi cheti cha udhamini wa Tuzo za EJAT, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gelead J. Teri, Oktoba 4, 2024, katika ofisi za TIC, Dar Es Salaam.*

# KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)

# HUDUMA MAHALA PAMOJA

Labour Services

Occupational, Safety and Health Authority (OSHA)

The Tanzania Electric Company Limited (TANESCO)

Business Registration and Licensing Authority (BRELA)

National Environment Management Council (NEMC)

The Mining Commision

Ministry of Agriculture

Ministry of Lands and Human Settlements

Tanzania Immigration Department

National Identification Authority (NIDA)

Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (TMDA)

Tanzania Revenue Authority (TRA)

Tanzania Bureau of Standards (TBS)

TANZANIA INVESTMENT CENTRE
THE FACILITATOR

Head Office,
P.O. Box 938
Golden Jubilee Tower,
1st Floor, Ohio Street, Dar es Salaam

Email: info@tic.go.tz
Telephone: +255 734 - 989 469
Phone: +255 734 989470
Fax: +255 25 25 - 2504399

# Kampeni ya Mlango kwa mlango ya TRA ilivyovuna mamilioni ya kodi

Usione vyaelea basi ujue vimeundwa, hicho ndicho kinachoonekana katika mwenendo wa ukusanyaji wa mapato wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kuelea kwa TRA kumeonekana baada ya mamlaka hiyo kuanzisha kampeni kupita duka kwa duka, kutoa elimu kwa mlipa kodi, kampeni iliyopewa jina la 'TRA Mlango kwa Mlango'.


TRA Mlango kwa mlango, ilianzishwa kwa lengo la kueneza elimu ya kodi kwa kila mwananchi na kwa urahisi.

Richard Kayombo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipa Kodi wa TRA anasema ni vigumu kwa walipakodi kuacha biashara zao na kuhudhuria semina za kodi hivyo mamlaka hiyo iliamua kuanzisha kampeni hiyo ili kuwarahisishia ikiwa ni pamoja na kuona mazingira yao ya biashara na changamoto zao.

"Ni kazi nyepesi kumuelimisha mlipa kodi akiwa katika eneo lake la biashara kuliko akiwa mbali," anasema.

Kwa mujibu wa TRA, Desemba, mwaka jana mamlaka hiyo iliweka historia kwa kukusanya Sh. trilioni 3.05 kwa mwezi wakati lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. trilioni 2.9 kwa mwezi, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

**MAKUSANYO YA DESEMBA 2023**




"Mafanikio makubwa tuliyoyaona ni kuongezeka kwa makusanyo na mwamko mkubwa wa ulipaji kodi kwa wafanyabiashara na tumekuwa tukitumia mbinu bora na rafiki za ukusanyaji wa mapato na tulishaachana kabisa na matumizi ya nguvu kudai kodi," amesema Kayombo.

Anasema kampeni ya mlango kwa mlango imechangia kwa kiwango kikubwa wananchi kuelewa umuhimu wa kulipa na imesababisha ongezeko la walipa kodi kwa hiari.

Kwa upande wake, Meneja Elimu kwa mlipa kodi wa TRA, Paul Walalaze anasema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepangiwa kukusanya fedha kiasi cha Trilioni 30.4 katika bajeti ya Trilioni 40.35 "Hizi fedha lazima zipatikane na zinapatikana kwa Watanzania walipa kodi," anasema.

Walalaze anasema fedha za kodi zinazokusanywa hazichezewi kwani ndizo zinazokwenda kugusa maisha ya wananchi kwa kuwapa huduma muhimu.

"Kodi hizi tunazowalipa Watanzania ndizo zinazoleta maendeleo. Maendeleo hayo ni pamoja na ya kisiasa, kiuchumi na kijamii," anasema.

Walalaze anasisitiza kuwa TRA mwaka huu inakwenda kusababisha maendeleo nchini na hivyo anawaomba wananchi kulipa kodi lakini pia kudai risiti wanaponunua na wanapouza watoe risiti.

"Tunahimiza ulipaji wa kodi wa hiari, Tunashirikiana na sekta za habari kuhakikisha wananchi wanapata habari kuhusu ukusanyaji wa mapato," anasema Walalaze na kuongeza:"Wananchi wote tukishikamana maendeleo hayatapatikana kwa misaada ya nje. Nikisema maendeleo namaanisha uboreshaji wa uchumi kama miundombinu ya reli, Barabara."

Kwa mujibu wa TRA, fedha za kodi ndizo zinazochangia maendeleo ya kijamii kwa mfano, elimu bure, maji, huduma za afya inapatikana kwa uhakika.

Pamoja na kupita mlango kwa mlango, TRA imeanzisha siku ya kuwasikiliza walipa kodi kwa mkoa wa Dar es Salaam ambayo inaadhimishwa kila Septemba 12. Katika siku hii, ofisi zote huwa wazi na kuwakaribisha wafanyabiashara kuwasilisha kero zao.

"Kadhalika kila alhamisi ya kila wiki, imetengwa kuwa siku ya kuwasikiliza walipa kodi, katika mikoa yote," anasema Kayombo.

Lakini ili kuwafikia watu wengi zaidi, TRA imetumia wasanii wa vichekesho, au komedi kutangaza kazi za mamlaka hiyo ili kuvutia kundi kubwa la vijana wafanyabiashara.

**MFANO WA KUIGWA**

Kampeni ya Mlango kwa Mlango ilianzishwa mwaka 2019, nia ikiwa ni kuhakikisha wafanyabiashara wanafuatwa kule waliko na kuhakikisha wanapata elimu kwa njia rafiki zaidi.

Kwa mujibu wa TRA, mamlaka hiyo inatumia maofisa wake ambao hutengeneza mazingira rafiki zaidi ili kuepusha mitazamo hasi, iliyojengwa na wafanyabiashara kuhusu TRA.

Mafanikio ya Kampeni ya Mlango kwa Mlango unaweza kusema yamechukuliwa kuwa ni mfano wa kuiga na taasisi nyingine ikiwamo Wizara ya Afya.

Kwa mfano, mwaka 2022, Wizara ya Afya, kupitia mpango wa kukabiliana na magonjwa yasiyopewa kipaumbele ilianzisha kampeni ya nyumba kwa nyumba ya Ugawaji wa Kingatiba kudhibiti Ugonjwa wa Matende na Mabusha (Ngirimaji).

*"Kodi hizi tunazowalipa Watanzania ndizo zinazoleta maendeleo. Maendeleo hayo ni pamoja na ya kisiasa, kiuchumi na kijamii,"*

TANZANIA PORTS AUTHORITY

# Mwamba anayeinuka

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ni mtengenezaji wa mustakabali mpya wa Tanzania. Bandari ya Dar es Salaam ambayo awali ilikuwa kichefuchefu, imeboreshwa na sasa ni mtambo wa kusimamia mtiririko wa bidhaa na shehena.

Sasa TPA haishughulikii tu biashara, bali inaiongoza ikijiandaa kuhodhi njia kuu za biashara kwenye ukanda huu wa Afrika. Hadi sasa, asilimia 70 ya shaba ya Zambia inapitia Dar es Salaam. Na kwa hakika si shaba tu, mazao kama mahindi, ngano na pamba pia yanapitia bandarini hapo.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Bw. Plasduce Mbossa, anasema: "Jitihada zetu za kuongeza uwezo na kuboresha ufanisi, zimevuta mizigo mingi kutoka nchi jirani. Sisi si tu bandari, bali ni kitovu cha usafirishaji bidhaa ukanda huu, na Zambia ina mchango muhimu katika maono haya."

### Kufufuliwa TAZARA

Ni asubuhi tulivu ya Septemba yenye baridi na hewa safi jijini Beijing, China; anga ni la buluu, aina ya siku ambayo wenyeji huiita 'ya dhahabu'.

Siku njema huonekana asubuhi, na asubuhi hii ya leo, inaonesha matumaini makubwa.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema na mwenyeji wao, Xi Jinping, wanashuhudia wino ukimwagika na kukauka, kuthibitisha mkataba imara wa dola za Marekani bilioni moja.

Ni mkataba muhimu wa kuifufua reli ya kihistoria ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ukiashiria mabadiliko makubwa si katika sekta ya reli pekee, bali pia kwa TPA; nguvu inayochipuka katika biashara ya usafirishaji ukanda wa Afrika Mashariki.

Mkataba huu wa makubaliano ni ishara ya mageuzi makubwa kwa bandari za Tanzania: Dar es Salaam na Tanga, ambazo sasa zitakuwa malango makuu ya kimataifa, chini ya usimamizi imara wa serikali ya Rais Samia Hassan.

Katika miaka ya 1970, TAZARA ilijengwa kuashiria umoja wa Afrika, ikiunganisha ukanda wa shaba wa Zambia na pwani ya Bahari ya Hindi upande wa Tanzania.

Ulikuwa mradi imara wa kimapinduzi, lakini ukaanguka. Reli ikaharibika na kudhoofisha kasi ya usafirishaji madini, na Zambia ikalazimika kutumia barabara za vumbi hadi pwani kwa shida. Lakini sasa, kwa dola bilioni moja kutoka China, reli hii inafufuliwa. Itaunganisha tena ukanda wa shaba wa Zambia na Dunia, kupitia bandari ya Dar es Salaam.

Ufufuo huu ni muhimu kwa mpango wa muda mrefu wa TPA. Kupitia mradi wa kuboresha lango la bahari la Dar es Salaam wa dola milioni 440, TPA inajipanga kuhudumia tani milioni 30 za shehena kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

Zambia ina mchango mkubwa katika mpango huu, kwa kuongeza kiwango chake cha biashara hadi tani milioni 2 mwaka 2022.

Mwaka 2023/24, Zambia imesafirisha tani 2,248,505 za mizigo kupitia Dar es Salaam, ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 tangu mwaka 2022/23.

### Kudhibiti biashara

TPA si tu sehemu ya mpango, bali ndiye mbunifu mkuu wa udhibiti wa biashara ya kikanda.

Moja ya mikakati muhimu ni kufikiwa kwa makubaliano ya miaka 30 kati ya Tanzania na Kampuni ya DP World ya Dubai.

Upande wa mkataba wa TAZARA, Bw. Mbossa anasema kwa furaha: "Mkataba huu unaendana kikamilifu na mkakati wetu wa muda mrefu wa kuongeza uwezo na ufanisi katika bandari zetu.

"Tumekuwa tukishawishi na kuvutia shehena kubwa kutoka ukanda huu, lakini kufufuliwa kwa reli hii kutatufanya kuwa kitovu muhimu kibiashara kwa kanda yetu. Zambia, kama mshirika muhimu wa biashara, ni sehemu muhimu ya maono haya, na tuko tayari kuchukua hatua zaidi."

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, aliyesimamia makubaliano na DP World, amekuwa akisukuma kwa nguvu uboreshaji wa bandari, akisisitiza kuwa uwekezaji huu mpya utapunguza gharama za usafirishaji kwa karibu nusu na kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara Kusini mwa Afrika.

TPA si mchezaji tu katika ukanda huu wa biashara. Ndiye mtunga mikakati mkuu. Kwani kasha la futi 20, ambalo awali liligharimu dola 240, sasa linagharimu hadi dola 90 tu, ikiwa ni punguzo la asilimia 62.5. Kasha la futi 40, awali liligharimu dola 420 lakini sasa ni dola 180 tu.

Katika usafirishaji shehena nje, kasha la futi 20 lililokuwa likigharimu dola 160 sasa ni dola 75, huku la futi 40 gharama ikishuka kutoka dola 280 hadi 150.

Bandari ya Mombasa, Kenya, iliyokuwa kinara katika biashara hii hapo awali, sasa joto linapanda. TPA imeshinda washindani wake kwa kuvutia wasafirishaji wa Zambia kutokana na uharaka wa huduma, gharama za chini na ofa bora.

Si tu hesabu ya biashara, bali pia ni lazima suala liwe endelevu. Kwa wasafirishaji wa Zambia, punguzo hili ni msaada mkubwa katika soko la kimataifa lenye ushindani mkubwa. Kila dola inayookolewa kwenye ushuru moja kwa moja ni faida.

Faida inakua, uzalishaji unakua na ghafla bidhaa za Zambia: shaba, mahindi na kobalti, zinaonekana kuvutia zaidi kwa wanunuzi wa kimataifa. Sahau bandari za Beira, Msumbiji na Durban, Afrika Kusini: Dar es Salaam sasa imekuwa njia kuu ya dhahabu kuelekea ulimwenguni.

Kama Bw. Mbossa anavyoeleza: "Mpango huu wa kimkakati unaonesha uwezo wetu wa kuleta maendeleo makubwa ya miundombinu kwa kushirikiana na wadau muhimu. Huu si tu ukuaji, ni mabadiliko yanayoifanya Tanzania kuwa kitovu cha usimamizi wa huduma za usafirishaji Kusini mwa Afrika."

### Uhai wa uchumi wa Zambia

Kwa Zambia, Dar es Salaam si tu bandari, bali ni mshipa unaosukuma uchumi wake. Ukanda wa shaba, unaozalisha tani 720,000 za shaba kila mwaka, unategemea ufanisi wa TPA kufikia masoko ya kimataifa. Bila TPA, shaba ya Zambia ingekwama Ndola, ikisafirishwa polepole barabarani au kukwama ghalani.

Reli ya TAZARA na bandari iliyoboreshwa ya Dar es Salaam, ni nguzo zinazowezesha bidhaa za Zambia kuendelea kusafirishwa kwa ufanisi.

Njia mbadala, kupitia Beira au Durban, zina changamoto nyingi. Beira inajulikana kwa msongamano, miundombinu duni na usumbufu wa hali ya hewa kama vimbunga; wakati bandari za Afrika Kusini zinakabiliwa na mahitaji ya ndani na huduma za reli zisizoaminika za *Transnet.*

Hizo husababisha ucheleweshaji wa mara kwa mara unaovuruga mtiririko wa usafirishaji wa Zambia. Lakini Dar es Salaam, kwa muunganiko wake bora na TAZARA, haina vikwazo kama hivyo.

Pia, kwa Zambia, Dar es Salaam si bandari pekee ya Tanzania inayotoa fursa muhimu kufikia soko la kimataifa, ipo pia ya Tanga ambayo imekuwa njia muhimu hasa kwa usafirishaji mafuta.

Katika miaka mitano iliyopita, Zambia ilisafirisha jumla ya tani za ujazo 132,883 za mafuta kupitia Tanga, kiasi ambacho kilipanda kwa zaidi ya mara mbili mwaka jana.


Kutegemea bandari za Tanzania na maboresho ya ufanisi ya Dar es Salaam, ni muhimu kwa uchumi wa Zambia unaotegemea usafirishaji nje ya nchi.

## Mustakabali ni wa TPA

TPA inatambua kwamba dau ni kubwa. TAZARA inayofufuliwa, ndiyo injini, lakini bandari ya Dar es Salaam ni dereva. Kufikia mwaka 2030, bandari itakapofikia lengo lake la kuhudumia tani milioni 30 kwa mwaka, Mombasa itakuwa imeachwa nyuma kabisa.

TPA itakuwa imeibadilisha Dar es Salaam kuwa lango kuu lisilopingika kuelekea Kusini mwa Afrika. Huu ndio mustakabali wa biashara Afrika; jahazi linaloendeshwa kwa ustadi mkubwa na TPA.

Utajiri wa Zambia, tani moja baada ya nyingine, unatiririka kwenda duniani kwa kasi, gharama nafuu na kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyokuwa awali. Mizimu ya zamani imepotea kabisa, na sasa imechukua nafasi ya treni za mizigo zinazokimbia kuelekea siku za usoni. TPA haiendeshi tu bandari, inaunda pia mustakabali wa biashara Afrika Mashariki.



Bandari Ya Dar Es Salaam

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENCING AGENCY

# Miliki Ubunifu: Kipengele Muhimu Katika Mafanikio ya Biashara

**Na Stanislaus Kigosi**

Je, wajua umuhimu wa miliki ubunifu *(Intellectual Property – IP)* katika mafanikio ya biashara yako? Miliki ubunifu inajumuisha uvumbuzi, kazi za fasihi na sanaa, miundo, alama, majina, na picha zinazotumika katika biashara. Bidhaa hizi zinalindwa na sheria ili kuwapa wabunifu haki za kipekee juu ya ubunifu wao kwa kipindi fulani cha muda.

Hapa Tanzania, usimamizi wa sheria za miliki ubunifu unafanywa na Ofisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea, miliki ubunifu bado haijatumika ipasavyo katika kuimarisha maendeleo ya kibiashara na kiuchumi nchini. Hii ni fursa kubwa ambayo wabunifu wengi hawajaitumia kikamilifu. Kusajili miliki ubunifu kunampa mmiliki haki za kipekee za kutumia, kuzalisha, na kuuza ubunifu au uvumbuzi, na pia kunatoa ulinzi wa kisheria iwapo kuna ukiukaji. Hii inazuia wengine kutumia au kunakili kazi yako bila ruhusa na inakupa faida ya ushindani kwa kulinda taarifa za siri na kutofautisha bidhaa au huduma zako na za wengine.

COSOTA inasimamia haki miliki kama vile kazi za fasihi na sanaa, wakati BRELA inasimamia mali za viwanda kama vile hati miliki na alama za biashara. Bila usajili, wabunifu wanakosa ulinzi wa kisheria na wanaweza kupoteza haki zao za kipekee juu ya ubunifu wao, jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kubwa ya kifedha na kibiashara.

Ili kuepuka hili, ni muhimu kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kusajili miliki ubunifu katika tovuti ya BRELA, ili kuchukua hatua za kusajili kazi zako, na kushiriki taarifa hizi na wabunifu wengine ili waweze kunufaika na ulinzi wa miliki ubunifu.

Usikubali ubunifu wako upotee! Chukua hatua sasa na sajili kazi zako za miliki ubunifu ili kuhakikisha unapata faida zote zinazotokana na ubunifu wako.

Kimsingi, miliki ubunifu imegawanywa katika makundi mawili: Haki Miliki ambayo inalinda kazi za fasihi na sanaa kama vile vitabu, muziki, filamu, na programu za kompyuta, ikimruhusu mbunifu kudhibiti jinsi kazi yake inavyotumika; na Mali ya Viwanda ambayo inalinda mali za IP zinazohusiana na uvumbuzi, miundo, alama za biashara, na ubunifu mwingine wenye thamani ya kibiashara unaotumika katika shughuli za viwanda na biashara.

Chini ya bidhaa ya viwanda kuna makundi mengine madogo ya miliki ubunifu kama vile: hati miliki ambazo zinalinda uvumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia unaotoa njia mpya ya kufanya jambo au kutoa suluhisho jipya la kiteknolojia.

Pia, alama za biashara ni kundi jingine dogo la miliki ubunifu ambalo linalinda alama, majina, nembo, na kauli mbiu zinazotumika kutambulisha bidhaa au huduma na kuzitofautisha na nyingine. Zaidi ya hayo, kuna kundi la Siri za Biashara ambalo linalinda taarifa za siri za biashara zinazotoa faida ya ushindani. Miundo ya viwanda ni miongoni mwa sehemu zinazojulikana zaidi za mali ya viwanda ambayo inalinda sura ya nje au kipengele cha mapambo cha bidhaa.

Inapaswa kueleweka vizuri kwamba, bidhaa zote za viwanda lazima zisajiliwe ili zipate ulinzi wa kisheria. Ulinzi wa haki miliki hutolewa moja kwa moja na sheria kwa wabunifu. Hata hivyo, usajili huwapa wabunifu uhakika wa kazi zao kumilikiwa. Nchini mwetu, usimamizi wa sheria ya Haki Miliki unafanywa na Ofisi ya Haki Miliki Tanzania inayojulikana kama *Copyright Society of Tanzania,* kwa kifupi COSOTA.

Kwa upande mwingine, sheria za bidhaa za kiviwanda zinasimamiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). BRELA ni Ofisi ya Kitaifa ya Mali Miliki ya Tanzania, yenye jukumu la kuratibu masuala yote ya mali miliki nchini Tanzania linapokuja suala la mwingiliano wa Tanzania na ulimwengu wa nje kuhusu masuala ya Mali Miliki.

Kama nilivyosema hapo juu, BRELA inasimamia sheria za bidhaa za kiviwanda; Tanzania haina sheria moja ya pekee kuhusu bidhaa za kiviwanda. Katika muktadha huu, BRELA inasimamia Sheria ya Hati Miliki (Usajili) ambayo inatoa ulinzi kwa uvumbuzi wote. Pia, BRELA inasimamia Sheria ya Alama za Biashara na Huduma ambayo inatoa ulinzi wa alama zote za biashara zinazotumika katika shughuli za kibiashara.

Usajili unatoa ulinzi wa kisheria ikiwa mtu yeyote atatumia au kunakili IP yako bila ruhusa. Usajili unakuwezesha kuchukua hatua za kisheria na kutafuta fidia kama vile malipo au amri za zuio. Wakati mwingine ukiukaji wa haki za mali miliki unaweza kusababisha adhabu za jinai kwa wale wanaokiuka haki hizo.

IP iliyosajiliwa inaweza kupewa leseni au kuuzwa, hivyo kuzalisha mapato kwa mmiliki. Pia inarahisisha kujadili mikataba au ushirikiano, kwani IP iliyosajiliwa inatambulika kama mali yenye thamani ya soko.

Ni bahati mbaya kwamba wabunifu wa mali za IP wanasahau kusajili IP zao kabla ya kuzifichua, hasa kwa wale wanaowazingatia kuingia nao katika ushirikiano wa kibiashara. Kinachotokea katika hali hii ni kwamba watu au mashirika yaliyokusudiwa kuwa washirika wanawadanganya wamiliki halali na kuendelea kutumia mali hizo za IP katika biashara zao bila kuwafidia au kuwalipa wabunifu wa mali za IP husika.

Kumiliki IP iliyosajiliwa kunawapa wahusika faida ya ushindani kwa kuwawezesha kutoa kitu cha kipekee ambacho wengine hawawezi kuiga kisheria. Tofauti hii inaweza kuboresha nafasi ya soko na faida. Hata hivyo, watu wengi hasa nchini mwetu wanachanganya usajili wa kampuni, majina ya biashara na mali miliki hasa alama za biashara. Ni jambo la kawaida kumkuta mtu akisajili kampuni au jina la biashara na kutumia nembo au mandhari nzuri na ya kuvutia kwa biashara yake akidhani kwamba amepata ulinzi wa alama hiyo ya biashara inayotumika katika biashara.

Kwa hiyo, ulinzi wa IP ni muhimu kwa kulinda maslahi ya mmiliki na ya kibiashara, kuboresha fursa za soko, na kuhakikisha manufaa ya kisheria na kifedha ya muda mrefu kwa watu binafsi na biashara. Vilevile, ulinzi wa mali za kiakili unahakikisha ushindani wa haki wa kibiashara na wakati huo huo hujenga imani ya watumiaji.

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# Nguvu Inayoongoza Sekta ya Nishati Nchini Tanzania

Taifa Gas Tanzania Limited ni miongni mwa makampuni yanayokua kwa kasi katika sekta ya nishati nchini Tanzania. Kampuni hiyo ni maarufu katika sekta ya nishati nchini Tanzania, ukijikita zaidi katika usambazaji na uhifadhi wa Gesi ya Kupikia ya Majumbani (LPG). Ilianzishwa kwa maono ya kutoa suluhisho za nishati za kuaminika na nafuu, Taifa Gas imekua kwa kasi miaka ya hivi karibuni, ikijipatia umaarufu mkubwa nchini Tanzania na hata nje ya mipaka yake. Safari ya kampuni hii imeanza na kituo kimoja cha kuhifadhi hadi mtandao wa vituo vya kuhifadhi na kujaza gesi nchini kote ni ushahidi wa maono na kujitolea kwake.

Taifa Gas inaendelea kupanuka na kubuni mbinu mpya, ikibaki kuwa kampuni kinara katika kutoa suluhisho za nishati za kuaminika na nafuu kwa Tanzania na ukanda mzima wa Afrika Mashariki. Katika ulimwengu wa nishati, Taifa Gas Tanzania Limited imejipambanua kama nguzo muhimu ya maendeleo na uvumbuzi. Kwa kujitolea kwake kwa ubora na uendelevu, kampuni hii imekuwa kiongozi asiye na mpinzani katika sekta ya nishati nchini Tanzania.

kampuni ya Taifa Gas ilianza shughuli zake kwa kuwekeza katika ujenzi wa kituo cha kuhifadhi na kujaza LPG huko Kigamboni, Dar es Salaam. Kituo hiki, kilichoanza na uwezo wa kuhifadhi tani 1,650 za LPG mwaka 2014, sasa kimepanuka hadi kufikia uwezo wa tani 7,450, na kufanya kuwa kituo kikubwa zaidi cha kuhifadhi LPG nchini Tanzania. Kipaumbele cha kampuni hii ni kuuza LPG kwa wingi na kusafirisha nje ya nchi na hususan katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mwelekeo wa ukuaji wa Taifa Gas ni ushahidi wa maono yake ya kimkakati na kujitolea kwake kwa ubora. Mnamo mwaka 2014, kampuni iliamua kuwekeza katika maendeleo na ukuaji wa soko la LPG ndani ya Tanzania. Kufikia mwaka 2016, mkakati huu ulianza kuonekana, na kufikia mwaka 2018, Taifa Gas ilikuwa imejenga vituo vipya vya kuhifadhi na kujaza gesi angalau ishirini nchini kote. Kufikia mwaka 2024, Taifa Gas ina vituo 24 vilivyoko kimkakati kwa ajili ya kuhifadhi na kujaza LPG. Upanuzi huu umeongeza uwepo wa kampuni sokoni na pia kuhakikisha Watanzania wengi wanapata nishati safi na bora.

Nafasi ya Taifa Gas kama kampuni kiongozi wa sekta ya nishati nchini Tanzania inasisitizwa na miundombinu yake ya kisasa na kujitolea kwake kwa ubora. Vituo vya kisasa na mtandao imara wa usambazaji wa kampuni vinahakikisha upatikanaji wa LPG katika maeneo ya mijini na vijijini. Uaminifu huu umekiwezesha Taifa Gas

kujijengea sifa ya ubora na kuaminika kwa wateja na washikadau wa sekta. Kwa miradi mikubwa michache inayokuja, Taifa Gas itaendelea kukua na kubuni njia mpya za kukidhi mahitaji ya soko la Tanzania na zaidi ya hapo.

**Tuzo na Tuzo za Heshima**

Kwa miaka kadhaa, Taifa Gas imepokea tuzo mbalimbali kwa mchango wake katika sekta ya nishati na kujitolea kwake kwa uwajibikaji wa kijamii. Tuzo hizi zinaakisi kujitolea kwa kampuni katika uvumbuzi, uendelevu, na maendeleo ya jamii. Utendaji wa kampuni na uongozi wake katika sekta vimeonyeshwa na rekodi yake thabiti ya kutambuliwa, huku tuzo ya hivi karibuni ikiwa ni mwaka 2024 kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa "Kutambua Juhudi za Kuhifadhi Mazingira na Mchango katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia."

Taifa Gas haijajikita tu katika ukuaji wa kibiashara bali pia katika kurudisha kwa jamii.

Kampuni inajihusisha na miradi mbalimbali ya uwajibikaji wa kijamii (CSR) inayolenga kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. Miradi hii inajumuisha kuunga mkono sekta ya Elimu, Afya, na Uhifadhi wa Mazingira, ikionyesha kujitolea kwa Taifa Gas kwa maendeleo endelevu. Taifa Gas imekwenda mbali zaidi kuhakikisha kuwa safari ya Tanzania kuelekea nishati safi kwa wote inatekelezwa, kwa kutoa gesi na mitungi ya bure kwa jamii zenye uhitaji na zisizojiweza nchini Tanzania.









# LHRC wasambaza tabasamu kila kona

WAHENGA walituasa kwamba *'samaki mkunje angali mbichi'* ndivyo ilivyo katika juhudi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) katika kupika vijana wangali shuleni ili kupata maarifa ya masuala ya haki za binadamu. Lengo kubwa ni kuwawezesha ili wawe chachu ya kuibadili jamii ili iwe inajali haki.

Ili kutimiza lengo hilo, LHRC walianzisha klabu za haki za binadamu katika shule za sekondari hadi ngazi ya vyuo vikuu kwa kushirikiana na uongozi wa shule na vyuo mbalimbali. Wajibu wa kuzisimamia umechiwa mamlaka za taasisi hizo za elimu, wakati LHRC wanawajibika kutoa miongozo na uratibu wake.

Hatua hii ya kuwapa maarifa vijana kuhusu haki za binadamu, pia ina nia ya kuwapandikiza shauku na kujiamini katika kusimamia na kutetea masuala ya haki za binadamu katika mwenendo mzima wa maisha yao, ndani ya jamii au hata katika utumishi wao baada ya kuhitimu masomo.

Mbinu hizi za kufungua klabu za haki za binadamu katika taasisi za elimu pia zinasaidia kuingiza katika mifumo ya taaluma masuala ya haki za binadamu, imefanya LHRC imechangia kujenga kizazi kinachojali haki za binadamu nchini.

"Kwa kufungua zaidi ya klabu 300 za haki za binadamu katika taasisi mbambali za elimu nchini, tumepiga hatua kubwa," wanaeleza LHRC kujivunia mafanikio haya. Aidha, LHRC wametoa mafunzo kwa zaidi ya walimu 300 ambao wanakuwa ni walezi wa hizi klabu katika taasisi zao za elimu.

Juhudi za LHRC zimefanikisha kupanda mbegu ambayo imestawi vema kwa vijana wapatao 15,000 kuhusu haki za binadamu. Kundi hili kubwa, kokote linakokwenda iwe ni kwenye utumishi wa umma au sekta binafsi, kila mmoja anakuwa amevaa maadili ya kutunza, kulinda na kutetea haki za binadamu hali itakayosaidia kujenga jamii inayolinda na kujali usawa.

Juhudi za kituo hiki kinachoheshimika nchini na kimataifa kwa kazi zake za kutetea haki za binadamu, zimejidhihirisha pia katika progaramu yao ya kufuatilia masuala ya haki za binadamu nchini. Ni katika kutekeleza mkakati huu, LHRC wamejijenga kutumia fursa ya tekinolojia ya kidijiti, kwani wameibuka na kitendea kazi kinachoitwa 'Haki Kiganjani'.

Ni dhahiri dunia sasa iko kiganjani, kutokana na tekinolojia ya kidijiti, simu za mkononi zinatumika kukusanya matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu nchini.

Kwa kutumia 'Haki Kiganjani' kituo hiki kimefanikiwa kuwapatia nyenzo timu ya wataalam zaidi ya 200 wa haki za binadamu ambao wamefunzwa na kuiva, wakiwa wamesambaa nchi nzima uwezo wa kukusanya taarifa mbalimbali za ukiukaji wa haki za binadamu. Ukusanyaji wa taarifa hizi umekiwezesha kitu kushughulikia matukio mbalimbali ya ukiukaji wa haki za binadamu ndani ya muda mfupi, hivyo kuleta nafuu kubwa sana kwa waathirika wa madhila hayo nchini kote.

Matumizi ya Haki Kiganjani yamerahisisha sana ukusanyaji wa taarifa na matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu nchini kwa upande mmoja, pia zana hii imesaidia kurahisisha taratibu za uandaaji wa ripori mbalimbali za LHRC kuhusu hali ya haki za binadamu nchini kwa upande mwingine.

Ni kupitia ukusanyaji wa taarifa hizi, kituo kinapata ujasiri wa kuchakata, kuchambua na kutoa mapendekezo mbambali ya kubadilishwa kwa sera ambazo zinaonekana kuwa chanzo cha ukiukaji wa haki za binadamu ili kusaidia taifa kuwa na mfumo endelevu wa kutoa haki kwa watu wake.

Pia ziko programu nyingine nyingi ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa nchni kupitia LHRC, hususan utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa mwaka 2023 baada ya kufikia wateja 29,491 kutoka wateja 18,294 waliohudumiwa mwaka 2022 likiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 60 ndani ya mwaka mmoja tu.

Hata hivyo kama wasemavyo wahenga kila masika huja na mbu wake, idadi ya wateja wanawake waliofikiwa bado imeendelea kuwa chini kuliko wanaume. Katika takwimu hizo idadi ya wanawake ilikuwa ni asilimia 35 na wanaume asilimia 65. Hali hii inazidi kuamsha maswali, kwamba ni kwa nini wanawake wanabaki nyuma katika kunufaika na huduma hii? Je, ni kutokujua au ni mwendelezo tu wa jinsia hii kubaki nyuma?
LHRC ni kama mtoa huduma anayepita kila mahali, ni kama simulizi ya mcheza mpira wa soka anayecheza namba zote, kwani hata kwenye magereza walibisha hodi kuhudumia wenye uhitaji wa msaada wa kisheria. Wateja 864 wakiwa gerezani walifikiwa na kituo hiki kwa mwaka 2023 pekee. Hapa pia wanaume walikuwa ni wengi zaidi wakichangia asilimia 87 ya waliofikiwa huku wanawake wakiwa ni asilimia 13.

Kwa kutumia maafisa wanaotoa msaada wa kisheria nchi nzima, kituo pia kimewapa tabasamu wateja wake 254 kwa kuwapa msaada wa kisheria kwa ngawanyo wa asilimia 35 wanaume na asilimia 65 wanawake.

Wanufaika wakuu wa msaada wa kisheria wa LHRC ni Dar es Salaam (38%), Arusha (23%), Kilimanjaro (11%), Morogoro (7%), Dodoma na Manyara (6%) na Pwani (5%). Wafungwa waliofikiwa magerezani walisaidiwa kujitetea kwenye kesi zao mahakamani, walipewa ushauri wa kisheria, pia kusaidia ambao walikuwa na changamoto za kupata nakala za hukumu na kibali cha kuwaondoa gerezani.

Huduma hizi na nyingine nyingi zinazotolewa na LHRC kwa jamii ya Watanzania, zinasaidia hasa wale ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za kulipia mawakili kuendesha kesi kwa sababu gharama za mawakili ni kubwa. Kwa kuzingatia kipato cha watu wengi kuwa ni kidogo, ni vigumu kuzimudu.

Mkurugenzi Mkuu wa LHRC, Dk. Anna Henga anasema "Siri ya furaha imejisimika kwenye kusaidia wengine. Kamwe usidharau nafuu unayoweza kutoa kwa maisha ya masikini, aliyedhulumiwa na asiyejiweza."

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# Mafanikio na Weledi Kupitia Uhakiki wa Mita za Maji

**Na Pendo Magambo**

Katika majira ya mchana, kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo (WMA) zilizopo Misugusugu, Mkoa wa Pwani, sauti za mashine za kisasa zinachanganyika na sauti za wafanyakazi wenye ari na bidii. Hapa ndipo hadithi ya mafanikio na weledi inaanza, hadithi ya uhakiki wa mita za maji.

Wakala wa Vipimo, chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ulianzishwa rasmi tarehe 17 Mei 2002 kwa agizo la Serikali. Kabla ya hapo, majukumu yake yalikuwa yakitekelezwa chini ya idara iliyokuwa ndani ya Wizara hiyo. Lengo kuu la kuanzishwa kwa wakala huu lilikuwa ni kuboresha huduma na kupunguza gharama za uendeshaji kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali.

"Tunajivunia kuwa sehemu ya mabadiliko haya," anasema Meneja wa Kitengo cha Bandari, Alfred Shungu, huku akitabasamu. "Kazi yetu ni kuhakikisha kuwa kila tone la maji linalotumiwa na wananchi linapimwa kwa usahihi."

Kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340, WMA inatekeleza majukumu yake kwa uhakiki na ukaguzi wa vipimo, kutoa ushauri wa kitaalam kwa waundaji wa vipimo, na kuidhinisha miundo ya vipimo mbalimbali kabla ya kuingizwa nchini. Hii ni pamoja na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa zinazozalishwa kwenye viwanda vya ndani na zile zinazotoka nje ya nchi.

Katika jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kwa kutumia vipimo sahihi, WMA imepata msaada mkubwa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ilitoa kiasi cha Tsh. 500,000,000.00 kwa ajili ya kununua mtambo wa kisasa wa kuhakiki mita za maji. "Mtambo huu ni mkombozi kwa wananchi," anasema Shungu. "Unatupa uwezo wa kuhakiki mita za maji kwa usahihi mkubwa."

Pia, WMA imenunua mitambo inayobebeka kwa urahisi (portable test kits) kwa ajili ya kuhakiki mita za maji zilizopo kwenye matumizi. Kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, mita hizi zinatakiwa kuhakikiwa kila baada ya miaka miwili kwa mita za DN 15 – 50 na kila baada ya miaka mitatu kwa mita za DN 50 na kuendelea.

"Uhakiki wa vipimo hivi ni muhimu sana," anasema Shungu. "Unahakikisha kuwa mamlaka za maji zinapata tozo sahihi kwa maji yaliyotumiwa na mteja, na mteja analipa gharama sahihi kulingana na maji aliyoyatumia."

Uhakiki wa mita za maji ulianza rasmi mwezi Machi 2019, na mpaka kufikia Juni 2024, WMA imefanikiwa kuhakiki jumla ya mita za maji 256,752 kutoka kwenye mamlaka mbalimbali za maji nchini. "Hii ni hatua kubwa sana," anasema Shungu kwa furaha.

WMA imeagiza mtambo mwingine wa kisasa wenye thamani ya Tshs. 496,000,000.00 ambao unatarajiwa kufungwa mwezi Oktoba. Mtambo huu utakuwa na uwezo wa kupima mita za maji 800 kwa siku, hivyo kusaidia mita nyingi kuhakikiwa na wananchi kupata huduma za maji na kulipa ankara zao kwa usahihi.

"Mtambo huu mpya utaleta mapinduzi makubwa," anasema Shungu. "Tutaweza kuhakiki mita nyingi zaidi kwa muda mfupi."

Katika kituo cha kisasa cha uhakiki wa vipimo kilichopo Misugusugu, kuna mtambo mkubwa na wa kisasa kwa ajili ya kuhakiki mita za maji. Kadhalika, kupitia kituo hicho pamoja na ofisi za mikoa za WMA zilizopo Tanzania Bara, kuna mitambo saidizi ambayo pia inatumika kufanya kazi za uhakiki wa mita za maji.

"Tunafanya kazi kwa bidii na weledi ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za maji," anasema Shungu. "Hii ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya chama tawala kwa kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025."

Kwa ujumla, simulizi ya WMA ni ya mafanikio, weledi, na kujitolea kwa ajili ya wananchi. Ni hadithi ya matumaini na mabadiliko chanya katika sekta ya maji nchini Tanzania. "Tutaendelea kuhakiki mita za maji kama Sheria ya Vipimo inavyoelekeza ili kuwalinda walaji na kuhakikisha kunakuwa na usawa baina ya mamlaka zinazotoa huduma hizo na wateja wao," anahitimisha Shungu kwa matumaini.

# Majukumu ya Wakala wa Vipimo

**Wakala wa Vipimo ina majukumu yafuatayo:**

1. Kumlinda mlaji katika Sekta ya Biashara, Usalama, Mazingira na Afya kupitia matumizi ya vipimo sahihi;
2. Kuilinda jamii kuepukana na madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya vipimo katika Sekta ya Biashara, Usalama, Mazingira na Afya;
3. Kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wanaojihusisha na utengenezaji, uundaji, na uingizaji wa vipimo mbalimbali katika Biashara, Usalama, Mazingira na Afya;
4. Kuwa kiungo kati ya Taifa letu na taasisi za kikanda na Kimataifa katika masuala ya Vipimo (Legal Metrology);
5. Kuhakikisha vifaa vyote vitumikavyo nchini kama standards za vipimo vina ulinganisho sahihi na ule wa Kimataifa;
6. Kukagua na kuhakiki bidhaa zilizofungashwa (Net quantity & labeling);
7. Kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya vipimo kwa wadau.

**Wakala wa Vipimo**
P.O BOX 313, Dar es Salaam,
NSSF House (Mafao), Ghorofa ya 7
Namba ya Simu : +255 (022) 2928158
Barua Pepe : info@wma.go.tz

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# Tanzania Kinara Usimamizi wa Usalama Mitandaoni

KATIKA zama za taarifa na uchumi wa kidijiti, ambapo kila kitu kutoka masuala ya kibenki hadi burudani hufanyika mtandaoni, usalama mtandaoni ni muhimu zaidi kuliko awali.

Kadri taifa linavyokwenda sambamba na mabadiliko ya kidijiti, kuna ongezeko kubwa la watumiaji wanaounganishwa mitandaoni, na huduma salama za mawasiliano ni suala la msingi hasa katika kuhakikisha mtandao salama kwa wote.

Kulinda rasilimali zetu za dijitali ni muhimu kuhakikisha usalama wa watu binafsi, biashara na taifa kwa ujumla.

Kama Doreen Bogdan-Martin, Katibu Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU), alivyosema: "Kujenga imani katika ulimwengu wa dijitali ni muhimu sana."

Kwa kuwekeza katika hatua za usalama wa mitandao zenye nguvu, Tanzania inaweza kulinda miundombinu yake ya dijitali, kulinda taarifa za kibinafsi, na kukuza uchumi wa kidijiti unaofanikiwa.

Kulingana na ripoti ya Usalama Mtandaoni ya Mwaka 2024 iliyotolewa Septemba mwaka huu, Tanzania inaongoza nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika, kwa kuwa na viwango vya usimamizi vya juu vya Usalama Mitandaoni.






Ripoti inaonesha Tanzania kuwa na viwango vya juu vya mfano katika ufanisi wa kusimamia nguzo tano za usalama mitandaoni, zilizowekwa na ITU mwaka 2015.

Shirika hilo kwa kutambua umuhimu wa kuwa na mtandao unaoaminika, jumuishi na salama kwa watumiaji; miundombinu, taarifa binafsi na kukuza uchumi wa kidijiti unaofanikiwa, lilianzisha vigezo vya nguzo zinazotakiwa kufuatwa na kila nchi mwanachama, ili kuwa na usimamizi mzuri wa usalama mtandaoni.

Nguzo tano zinazopimwa kwenye ripoti hiyo ya ITU GCIv5 -2024, (kifupi cha jina lake kwa Kiingereza), ni Hatua za Kisheria na Ujenzi wa Uwezo katika masuala ya Usalama Mitandaoni. Nyingine ni Mipango na Mikakati ya Kiufundi, Mfumo wa Usimamizi na Ushirikiano wa Usalama Mitandaoni.
Mafanikio ya Tanzania yalikuwa asilimia 100 kwenye nguzo ya Sheria, Mifumo ya usimamizi na Ushirikiano; na asilimia 99 kwenye nguzo ya Ufundi na Kujenga uwezo.

Baadhi ya vitu vilivyochangia kupaa kwa Tanzania kwenye CGI ya 2024 ni uwepo wa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama Mitandaoni, Sheria na Kanuni za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi 2022 na Sheria ya Makosa ya Kimtandao 2015.

Pia Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta (CERT) za mwaka 2018 na maboresho yake ya mwaka 2023 na Timu ya Kitaifa ya Mwitikio wa Kukabiliana na Majanga ya Kompyuta (TZ-CERT), timu iliyopo ndani ya muundo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Timu za Kisekta (GSoC ndani ya e-GA na TZ-FINCERT inayosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania).

Ushirikiano wa wadau ndani ya nchi, kikanda na kimataifa pia umechangia kwa kiasi kikubwa kuwezesha Tanzania kufanikiwa katika mchakato huu.


*Dkt. Jabiri K. Bakari*
**Mkurugenzi Mkuu TCRA,**

Akihojiwa Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K. Bakari anasisitiza azma ya taasisi yake kama mwanachama wa ITU, kwa niaba ya taifa kuendeleza dhamira ya kitaifa katika masuala ya usalama na uimara wa mtandao nchini. TCRA itaendelea kushirikiana na taasisi za wazawa, za kikanda na kimataifa. Ripoti ya GCI ilianza kutolewa mwaka 2015 na ITU.

# TBC yaonyesha njia kwenye utangazaji

**Na Peter Nyanje**

Kufikisha matangazo kwa wananchi wote bila kujali umbali ni moja ya Mwanaumengo makuu ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na imefanikiwa kulifikia lengo hilo kwa kiasi kikubwa katika kipindi kifupi.

Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dkt. Ayub Rioba, analiambia Jarida la Tuzo kuwa pamoja na mafanikio ambayo shirika hilo imeyapata, bado kiu yao ya maendeleo haijafika mwisho.

“Sasa hivi tupo kwenye utekelezaji wa mikakati mbalimbali itakayotuwezesha kuboresha shughuli zetu kama shirika la utangazaji,” anasema.

Lengo jingine kubwa la TBC ni kuandaa na kurusha maudhui yanayogusa maisha ya makundi yote ya jamii kwa kuzingatia utamaduni wa kitaifa na kiafrika.

Dkt. Rioba anabainisha kuwa kwa wanaofuatilia vipindi vya TBC, kwenye runinga, redio na mtandaoni ni mashahidi wa hilo.



Dkt. Rioba anasema kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa shirika hilo kuendelea kufanya upanuzi ili kuhakikisha kuwa usikivu wake unaimarika na watu wengi zaidi wanafikiwa. Hii ni kwa sababu TBC ndiye yenye dhima kubwa katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafahamu kile kinachofanywa na serikali yao kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kuhakikisha kuwa maoni na hoja za wananchi zinawafikia walio katika madaraka kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

“Wajibu huo si hiari yetu, ni takwa la kikatiba katika Ibara ya 18 inayotaka kila Mtanzania kupata taarifa na kutoa maoni yake,” anafafanua DKT Rioba

Kwa mujibu wa Dkt. Rioba, ni mkakati wa TBC katika kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo hayana usikivu au usikivu wa redio zake ni hafifu yanapata matangazo ya redio za TBC ifikapo 2025. Hivyo, anasema, wanasukumwa kuhakikisha hilo linafikiwa ili kukwepa maswali magumu yatakayoulizwa iwapo hawatatekeleza Mwanaumengo hayo.

Dkt. Rioba anasema kuwa ili kuhakikisha hayo yanafanikiwa, TBC inaendeela na kazi ya kukamilisha ufungaji wa mitambo ya redio inayojengwa katika maeneo 29 nchini.

Pia shirika hilo linaendelea na ujenzi wa mitambo ya masafa ya FM katika maeneo ya mipakani kupitia mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya utangazaji vijijini.

Kutokana na juhudi hizo, usikivu wa redio za TBC umeongezeka kutoka asilimia 54 (2015/16) hadi asilimia 92 pale ambapo miradi inayoendelea kutekelezwa itakapokamilika.

### Makao makuu

Kuhusu ujenzi wa makao makuu, Dkt. Rioba anasema kuwa kazi hiyo imeshaanza katika eneo la Vikonje jijini Dodoma.

“Ujenzi huu wa awamu ya kwanza utahusisha jengo la utawala, studio za redio, televisheni na TBC mitandao. Ujenzi umeanza Agosti 9, 2023. Mkandarasi anayetekeleza mradi huu ni CRJE (EAST AFRICA) LTD.



“Mipango yetu ni kukamilisha ujenzi huo mwakani na baada ya hapo tuongee na marafiki na wadau wetu kwa ajili ya mipango ya kuweka vifaa vya kisasa na studio za kisasa zitakazo tuwezesha kifanya kazi kisasa zaidi,” anasema Rioba akibainisha kuwa katika awamu ya kwanza ujenzi huo utagharimu shilingi bilioni 54.5.

## Chaneli za kimkakati

Ili kuhakikisha inatekeleza baadhi ya Mwanaumengo yake kwa ufanisi, DKT. Rioba anasema kuwa TBC imeanzisha Chaneli mahsusi za kimkakati, hatua hiyo inalenga kuwafikia wananchi ndani na nje ya nchi hivyo kuitangaza nchi kimataifa.

Kati ya chaneli za mkakati ambazo zimeanzishwa na TBC ni chaneli ya utalii.

Kwa mujibu wa Dkt. Rioba, Tanzania Safari Channel (TSC au Chaneli ya Utalii) ni jukwaa maalumu linalolenga kuendeleza sekta ya utalii nchini.

“Lengo la Chaneli ni kukuza utalii na kuhamasisha uhifadhi kwa kuonesha vivutio vingi vya bayoanuwai vilivyopo nchini na utunzaji wa vivutio hivyo ili kuenzi maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyoyatoa mwaka 1961, kwamba sisi sote tuna jukumu kubwa la kulinda na kuhifadhi vivutio vya utalii kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo,” anasema.

Pia imeanzishwa chaneli ya TBC2 ambayo ina dhima ya kutoa elimu kwa vijana wa rika lote katika jamii. Dkt. Rioba anasema dhamira kuu ya TBC2 ni kufundisha maadili, uadilifu, uzalendo kwa vijana wa Kitanzania kwa kutumia mfumo wa kuhabarisha, kufundisha na kuburudisha.

## Kampeni kubwa

Katika utendaji wake TBC limeshiriki katika kampeni kubwa nyingi za kitaifa na kimataifa. Moja kati ya kampeni hizo ni kampeni ya utunzaji wa mazingira kupitia upandaji miti ijulikanayo kama Mti wa Mama.

TBC kupitia kipindi cha Jambo Tanzania kinachorushwa na chaneli ya Televisheni ya TBC 1 imekuwa ikiendesha na kusimamia kampeni hiyo. Kampeni hii hufanyika tahere 27 ya kila mwezi.

“Hadi sasa jumla ya miti 8,116,230 imepandwa nchi nzima katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara, Songwe, Tanga, Tabora na Unguja huko Zanzibar kutokana na kampeni hiyo,” anasema Dkt. Rioba.

Dkt. Rioba anabainisha kuwa lengo la kampeni hii ni kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali pamoja na wadau wa mazingira duniani kote katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

## Tuzo

Umahiri wa TBC katika utangazaji umeliwezesha shirika hilo kupata tuzo mbali za kitaifa na kimataifa. Lakini si shirika pekee. Kwa sababu kazi inafanywa na waandishi, wapiga picha, wahariri na wengineo, nao pia wamekuwa wakipewa tuzo za aina mbalimbali zikiwamo Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT).

Rekodi zinaonyesha kuwa TBC imepata hati safi kwa Hesabu za miaka 11 mfululizo ikiwemo Mwaka wa Fedha 2022/2023 na pia imeendelea kupata Tuzo ya Uandaaji Bora wa Hesabu kwa kutumia viwango vya kimataifa (IPSAS) kila mwaka.

Tuzo nyingine ambazo TBC imewahi kujinyakulia ni pamoja na Tuzo ya Kinara wa Utoaji Elimu ya Uhifadhi wa Mazingira kupitia Vyombo vya Habari. Kwa upande mwingine, watumishi 10 wa TBC, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, walipata tuzo mbalimbali za umahiri katika masuala ya habari na utangazaji. Tuzo hizo zilitolewa na taasisi za ndani na nje ya nchi.


# Mahiri wa Habari

Karibu usome simulizi za mahiri wa habari. Ni simulizi za kusisimua kutoka miongoni mwa waliopata Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania. Ni simulizi zinazothibitisha ujuzi, maarifa na uzoefu wa hali ya juu katika tasnia ya habari. Ni simulizi zinazochambua uwezo wa mtu katika kuchanganua, kutafsiri na kuripoti habari kwa usahihi na uadilifu. Ni simulizi zinazoangazia kina cha maarifa kuhusu mada iliyofanyiwa kazi na kushinda tuzo.

Simulizi zinazodhihirisha uandishi wa kiufundi unaotumia lugha sahihi kwa mtindo unaovutia na kuelimisha. Simulizi zinazothibitisha uwezo wa kuchunguza kwa kina, kuhoji vyanzo na kuthamini uhalali wa taarifa kabla ya kuziripoti. Utashuhudia juhudi za mahiri wa habari katika ubunifu na uvumbuzi wenye namna mpya za kuwasilisha habari au kuhusisha hadhira kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko. Undani wa maisha na mahusiano kazini na nyumbani uliompa mtu umahiri wa uandishi wa habari umesheheni katika kurasa hizi.

> *Kila kitu ni kwa mara ya kwanza au haijawahi kutokea.*

# Safari ya Mercy





**Na Josephat Mwanzi**

Katika ulimwengu wa uandishi wa habari, kila mwandishi ana hadithi moja ambayo inabaki moyoni mwake, hadithi ambayo inamgusa kwa namna ya kipekee. Kwa Mercy Yasini Mbaya (29), mwandishi wa habari wa UTV, hadithi yake inahusu kijana Colman Ndetembea anayebuni vifaa wezeshi kwa watu wenye ulemavu, Mkoani Arusha. Mercy, akiwa na miaka mitano kazini, anajivunia sana habari hii ambayo imekuwa na athari kubwa kwa jamii.

Safari ya Mercy katika uandishi wa habari ilisukumwa na shauku kubwa ya kuleta mabadiliko kwenye jamii tangu akiwa mdogo. Kwa miaka mitano sasa, amejionea mwenyewe nguvu ya vyombo vya habari katika kuelemisha umma, kukuza maendeleo, na kuwawajibisha walio madarakani. Kazi zake zimemtoa kwenye vyumba vya habari jijini Dar es Salaam na kumfanya asafiri hadi pembe mbalimbali za Tanzania, ili kuandika habari ambazo zina maslahi ya maisha watu.

Mama yake Mercy, Helena Joseph Kamwela, mwenye miaka 57, anasema kwamba ingawa alitamani mwanaye awe daktari, amefurahi kuona Mercy ametimiza ndoto yake. "Mercy alipenda sana kusikiliza redio, na baba yake akirudi nyumbani anatamani amfungulie redio wanaanza kusikiliza pamoja mpaka analala," anasema mama yake Mercy.

"Mama yangu ni mwalimu kwa hiyo wakati wa kukuwa hakutaka tuwe walimu kama yeye. Alitaka tuwe madaktari. Lakini mimi nilikuwa natamani kuwa mwanasheria au mwanahabari. Na hasa wakati nakuja kusoma uandishi wa habari nilitaka kuwa ripota tu, sikujua kama kuna uwanda mkubwa hivi," anasema Mercy.

Baba yake alifariki akiwa darasa la tatu. "Alikuwa fundi wa vifaa vya umeme, mama alinambia nilikuwa namwambia baba kwamba natamani kuingia kwenye redio na mimi nione watu waliomo kwenye redio na mimi nitangaze kama wao. Baada ya mama kunambia hivyo, nilitambua kwamba kumbe nipo sahihi. Nilisoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale SJMC, nikamaliza masomo yangu digrii ya kwanza ya uandishi wa habari. Ila nashukuru kwamba mdogo wangu Johari ametimiza ndoto ya mama na sasa yeye ni daktari," anaongeza Mercy.

VIDEO

Akizungumzia habari ambayo imemfanya kuteuliwa kuwania Tuzo za Umahiri wa Habari Tanzania (EJAT), Mercy anasema, "Jamii yetu bado haijafahamu kikamilifu uwezo wa watu wenye ulemavu wanapopata vifaa wezeshi." Aliona umuhimu wa kuelimisha umma kuhusu jinsi vifaa hivi vinavyoweza kubadilisha maisha ya watu wenye ulemavu na kuwasaidia kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Upatikanaji wa vifaa wezeshi nchini ni changamoto nyingine kubwa. Vifaa vingi havimudu mazingira ya barabara zetu na hivyo kuwa kikwazo kwa walemavu. Mercy aliona umuhimu wa kuangazia suala hili na kuleta mwamko kwa jamii na serikali kuhusu umuhimu wa vifaa wezeshi.

Safari ya Mercy kupata habari hii haikuwa rahisi. Ili kuonesha uhalisia, ilimbidi yeye na waandishi wa habari wenzake kuamka saa tisa usiku kuungana na kijana anayebuni vifaa wezeshi, ambaye hutumia baiskeli maalumu kwenda kazini. "Ilikuwa ni changamoto kubwa, lakini nilijua kuwa ni muhimu kuonesha jinsi Colaman anavyopambana kila siku," anasema Mercy.

Moja ya matukio ya kuvutia zaidi ilikuwa ni wakati walipomtembelea mwanafunzi mwenye ulemavu. "Alikuwa na furaha kubwa kutuona, lakini hali yake ilibadilika na mwili wake ulianza kutetemeka zaidi. Ilitubidi tusubiri saa kadhaa hadi furaha yake ipungue, kwa sababu tuliambiwa akiwa katika hali ya furaha kubwa pia ni changamoto kwake." Mercy anakumbuka. Tukio hilo lilionesha jinsi hali ya kihisia inaweza kuathiri watu wenye ulemavu na umuhimu wa kuwa na subira na uelewa.



Mercy na timu yake walitaka mandhari ya utulivu na ya kufikirisha zaidi kwa ajili ya kurekodi mahojiano. Walipata ziwa Duruti, lakini changamoto ikawa upepo kuyumbisha mtumbwi na kijana kutoka nje ya fremu ya kamera kila walipokuwa wakirekodi. "Ilikuwa ni changamoto kubwa, lakini tulifanikiwa kupata picha nzuri na za kuvutia," anasema Mercy kwa tabasamu.

Moja ya mambo yaliyomvutia Mercy zaidi ni kuona mtoto mwenye ulemavu akiandika kwa kutumia kompyuta kwa usaidizi wa baskeli wezeshi. "Ilikuwa ni picha ya kuvutia sana, kuona jinsi teknolojia inaweza kubadilisha maisha ya mtu," anasema Mercy. Pia, kuona wanafunzi wakifua, kuchota maji, na kucheza kwa kutumia baiskeli wezeshi ilikuwa ni ushahidi wa jinsi vifaa hivi vya Colman vinavyoweza kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu.

Mercy anasisitiza kuwa mafanikio ya habari hii yalitokana na ushirikiano wa timu nzima. "Lakini nimefanya na watu wengi stori hii ikiwa pamoja na



*Mercy Yasini Mbaya akimhoji Bi. Magdalena Simba, Mkuu wa kitengo Cha Ushonaji cha kiwanda cha Kyaro Assistive Tech cha Arusha.*

*"Elimu kwa vitendo ni nyenzo kuu ya vijana kujiajiri,"*

mhariri wangu Frank Sanga, dereva, wapiga picha wawili, mtu wa sauti (sound engineer) mmoja, mtaalamu mwelekezi (director) wa picha mmoja, mimi nilifanya kazi kama mwandaaji (producer) na mtangazaji, lakini pia kulikuwa na mtangazaji wa kiume, na kulikuwa na mhandisi wa masuala ya umeme, na kijana wa Jakaya Mrisho Kikwete Foundation, na mtu wa Ofisi ya Waziri Mkuu maana wanasaidia ubunifu.

"Kwa miaka zaidi ya mitano niliyofanya kazi ya uandishi wa habari, hadithi hii imenipa mtazamo chanya zaidi wa maisha," anasema Mercy. Anaamini kuwa, nafasi ya vijana katika kushiriki kutatua changamoto kwenye jamii inatakiwa kutiliwa mkazo zaidi. "Elimu kwa vitendo ni nyenzo kuu ya vijana kujiajiri," anasisitiza Mercy.


Hadithi ya Mercy Yasini Mbaya ni ushahidi kwamba tunahitaji kuinua uandishi wa habari unaojikita katika kuleta mabadiliko. Kupitia kazi yake, amefanikiwa kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa vifaa wezeshi kwa watu wenye ulemavu, na kwa kufanya hivyo, ameleta mwanga mpya katika maisha ya wengi. Mercy, ambaye bado hajaanza maisha ya familia, anasema ataendelea na fani ya uandishi wa habari katika maisha yake, hasa katika eneo la teknolojia na ubunifu miongoni mwa vijana.

"Mimi ni miongoni mwa watu wanaoshangaa kusikia kwamba China na Tanzania tulikuwa sawa kimaendeleo, lakini leo tunawaomba msaada. Kwa hiyo, nimekuwa na hamu ya kuwaonesha vijana kwamba tuna uwezo na akili sawa na Wachina. Ningekuwa na hela, ningewapa mitaji, lakini kwa kutumia taaluma yangu, naona niwatafute vijana na kuwaibua," anasema. Mercy anashukuru chombo chake cha habari, UTV, kwa kumpatia msaada na kumtia moyo kufanya kazi yake, hasa katika ubunifu. "Hii inanipatia sana chachu kuendelea na kazi hii," anasema.

# Habari zilizogusa **Umma**

Karibu katika kurasa za Habari Pekee za Maslahi ya Umma. Ni habari zilizoshinda Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania. Hatua ya kwanza ya kupatikana kwa habari hizi ilihusisha kazi iliyofanywa na magwiji wa habari waliotafiti kuhusu habari siyo za maslahi ya umma tu bali pia za kipekee. Hatua ya pili ilihusisha jopo huru la majaji waliozingatia vigezo kutathmini umaana, umuhimu kwa maisha ya jamii, athari za kiuchumi, uwajibikaji wa serikali na wajibu wa makampuni kwa umma. Vigezo vingine vilivyotumika ni pamoja na kubainisha kama habari inawasilisha jambo jipya ambalo halikufahamika au jamii haikujua undani wake hivyo kuifanya habari hiyo kuwa ya kipekee. Habari ambayo inaangazia kutokuwepo kwa usawa, ubaguzi, uonevu kwa kundi kubwa la watu. Habari inayogusa hisia za jamii kutokana na kuathiri utamaduni, mila, maadili na desturi. Habari ambayo dhahiri inatakiwa na umma kutokana na ushahidi wa mwenendo wa mijadala kupitia mitandao ya kijamii, majukwaa ya umma au mijadala mizito katika jamii. Habari ambayo kimsingi na kwa vyovyote vile inaathiri kundi kubwa la watu. Habari yenye vyanzo vya kipekee vya watu au nyaraka na takwimu.

# Fursa iliyopotea




Mwaka 2023 ulikuwa na matukio makubwa ya kusisimua ambayo yaliibua mijadala mikubwa nchini. Miongoni mwa matukio hayo ule wa mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirati ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania (IGA); Mchakato wa kuhamisha wafugaji wa jamii ya Kimasai kutoka Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro na janga la maporomoko ya matope katika mji wa Katesh, wilayani Hanang, mkoa wa Manyara watu wengi walipoteza maisha, makazi na mali.

Matukio haya makubwa yalitikisha mijadala mingi katika mitandao ya kijamii, kwenye vijiwe vya kahawa, ndani ya vyombo vya usafiri, kwenye vijiwe vya 'kupata moja moto moja baridi', kiasi cha kuisukuma serikali mara kwa mara kuibuka kutoa taarifa au ufafanuzi mahsusi kuhusu matukio hayo.

Taarifa ya timu ya majaji waliopitia habari zilizoandikwa na kutangazwa na vyombo vya habari vya runinga, magazeti, redio na vyombo vya mitandao (online) kwa mwaka mzima wa 2023, ilihitimisha ripoti yake kwa kuonesha kwamba kulikuwa na woga, uvivu na kukosekana kwa shauku ya kufuatilia masuala haya matatu. Matukio hayo hayakupewa umuhimu wa kutosha katika kufuatilia, kuchakata, kuandika na kusambaza habari zake.

Ni kutokana na ukweli huo, vyombo vya habari vya Tanzania kwa ujumla wake, viliamua kujipa jukumu la kuandika vile tu vilivyokuwa vinasemwa na mamlaka za kiserikali kwa upande mmoja, au mara nyingi kuandika habari ambazo ziliegemea kutokuudhi watawala kwa upande mwingine. Habari za matukio haya matatu makubwa ambayo yalitikisa nchi yalikosa fikra tunduizi katika kuyadadisi na kuyapembua ili kuwa na taarifa huru zisizoegemea upande wowote.

Upitiaji wa taarifa mbalimbali zilizoandikwa na kutangazwa na vyombo vya habari katika kipindi hicho, siyo tu zinaonesha kukosekana kwa taarifa za kina, udadisi na mantiki, bali pia zilikuwa ni sehemu ya kuonesha mafanikio ya upande wa utawala katika kushughulikia masuala hayo matatu. Waandishi wengi wa habari pamoja na vyombo vyao walikosa uthubutu na udadisi katika kuziendea taarifa za Ngorongoro, Kateshi-Hanang na IGA hali inayojenga picha kwamba kulikuwa na maelekezo yanatolewa kutoka mahali fulani jinsi ya kushughulika na habari hizo.

Ifuatayo ni tathmini ya jinsi waandishi wa habari walivyopoteza fursa ya kusaidia jamii kuelewa kwa undani matukio hayo: -

### Kuhamisha Jamii ya Wamasai Ngorongoro

Upitiaji wa vyombo vya habari vyote, magazeti, runinga, redio na mitando ya kijamii, ulithibitisha habari hii ilikuwa inaepukwa kwa makusudi kufuatiliwa kwa kina. Kwa mfano, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2023, magazeti mengi yaliipa mgongo habari hii, na pale iliporipotiwa ilikuwa ni kwa wepesi sana. Hakuna hata gazeti



moja lilikuwa na habari huru ya uchunguzi wa kina kuhusu Ngorongoro, kwa maana hiyo waandishi wa habari walijikuta wakijifanya kila kinachoitwa kujidhibiti kihariri kwa kimombo *self-censorship*.

Hali ilikuwa ni mbaya zaidi kwa redio na runinga. Mbali ya taarifa za habari za vyombo za kieletroniki kusoma tu taarifa zilizokuwa zikitolewa na mamlaka za serikali kuhusu Wamasai walivyokuwa wanaondoka kwa makundi kutoka Ngorongoro kwenda kuanza maisha mapya Msomera, wilaya ya Handeni mkoani Tanga, hakukuwa na habari yoyote huru ya uchunguzi wa kina iliyotangazwa.

Timu ya majaji iliyotembelea vyombo vya habari mbalimbali kuzungumza na baadhi ya wahariri kuhusu uchapishaji wa habari za Ngorongoro, walikutana na majibu yanayofanana. Kwanza, wapo waliosema habari hizo hazikupewa kipaumbele na kwa maana hiyo hawana cha kuwasilisha kwenye shindano la EJAT 2023. "Hatukuchapisha habari zozote ambazo zinakidhi vigezo vya EJAT kama ambavyo mnatafuta," alisema mhariri mmoja wa kituo cha runinga.

Mhariri mmoja akijibu swali kwa nini hawana habari za Ngorongoro zenye kina licha ya suala hilo kuwa na mjadala mkubwa ndani ya jamii hasa kwenye mitandao ya kijamii, alisema: "Kwani wewe hujui? Utachapisha wapi? Kila kitu kinafuatiliwa." Hata hivyo, alishauri majaji wachambue taarifa zao za mitandaoni kwani kulikuwa na habari nyingi za Ngorongoro. Uchambuzi wa majaji kuhusu habari za mtandaoni haukuwa na majibu tofauti na hali ya zile habari za kwenye magazeti, redioni na runinga. Habari hizo zilidhihirika kuwa zimeandikwa kwa hofu, zenye kuegemea upande mmoja na zilizokosa uchambuzi tunduizi wa kina. Hakukuwa na habari hata moja ambayo ingeweza kutajwa kuwa ni huru na ya kiuchunguzi kuhusu suala la kuhamisha Wamasai kutoka Ngorongoro.

**IGA**

Suala la IGA ni kati ya taarifa ambazo zilijaa mkanganyiko na utata kiasi cha kukosekana kabisa weledi juu ya kilichotiliwa saini kati ya Serikali ya Tanzania na Emirati ya Dubai kama ulikuwa ni mkataba au makubaliano. Utata huu uliibuka hata wakati Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukijadili IGA. Wapo wabunge waliosema kuwa ulikuwa ni mkataba ilhali wengine wakisema siyo mkataba.

Ingawa nyaraka kuhusu IGA zilikuwa zimevujishwa kwenye mitando ya kijamii, huku makundi mbalimbali ya kijamii yakikosoa baadhi ya vifungu vyake kwamba vilikuwa vinakwenda kuumiza Taifa, vyombo vya habari vingi viligeuka tu kuwa kasuku wa kuimba kilichokuwa kinasemwa. Hakuna chombo kilichojipa wajibu wa kukaa na kutafiti kwa kina kuhusu IGA ili kuchapisha taarifa huru ambazo hazikuegemea upande wowote. Kulikuwa na taarifa za aina mbili, mosi, zilizokuwa zinatetea IGA bila kuwa na uchambuzi tunduizi kwa upande mmoja, lakini kwa upande mwingine ukosoaji ambao pia haukuwa umejikita kwenye uelewa wa kina.

Kwa mfano, utetezi wa serikali bungeni, mitaani na kwenye mijadala iliyoibuliwa kuhusu IGA ilikuwa ni kwamba hoja zote zinazotolewa kuhusu mapungufu yanayotajwa, zitazingatiwa wakati wa kuingia mikataba ya utekelezaji wa makubaliano kati ya nchi mwenyeji (Host Government Agreement- HGA) na Kampuni ya DP World ya Emirati. Hata hivyo, kazi iliyofanywa na timu ya majaji haikuweza kugundua chapisho lolote huru la chombo cha habari kuelezea kwa uhuru (independently) kwamba kwenye mikataba hiyo kuna nini mbali ya taarifa ambazo wasemaji wa serikali walieleza wakati wa utiaji saini mikataba mitatu Oktoba 22, 2023 Ikulu ya Chamwino Dodoma. Majaji hawakufanikiwa kuona chapisho lolote la chombo cha habari linaloonyesha limetafuta, kuchakata na kusambaza taarifa huru za kina kuhusu mikataba mitatu ya HGA ambayo ilisaniniwa siku hiyo. Hadi sasa hakuna habari huru za kiuchunguzi zimefanywa na chombo chochote cha habari siyo kuhusu IGA wala HGA.





## Maporomoko ya matope Katesh

Tukio hili kwa ujumla liliripotiwa na vyombo vya habari vya aina zote, runinga, redio, mitandao na magazeti. Vipo vyombo vilivyomudu kupeleka waandishi na wapiga picha wake kwenye eneo la tukio. Zipo picha za kuogofya zilizochapishwa na magazeti, kurushwa na runinga na kwenye mitandao.

Pamoja na tukio hilo la bahati mbaya ambalo lilichukua maisha ya watu zaidi ya 80 kuripotiwa kwa idadi nyingi ya habari kwenye vyombo vya aina zote, bado habari zake zilikosa kina na udadisi tunduizi.

Kwa mfano, hakuna chombo cha habari kilichochunguza kwa kina thamani ya rambirambi zilizopatikana, zilivyogawanywa na kupata taarifa za kina kuhusu maafa hayo, mbali tu ya kutangaza tu taarifa kama zilivyokuwa zinatangazwa na wasemaji wa serikali.

Mbali ya taarifa nyingi za maafa ya Katesh kutegemea zaidi taarifa za wasemaji wa serikali, vyombo vingi vya habari havikupeleka waandishi wake ili kuripoti kwa kina taarifa kutoka uwanja wa maafa, hali ambayo iliacha tukio hilo kupambwa zaidi na picha bila kuwa na mahojiano ya udadisi yanayoakisi uandishi tunduizi ambao ungeibua uwajibikaji.



# Kumbukizi **Gwiji** wa Habari

Karibu katika kumbukizi ya gwiji wa habari. Utakutana na historia ya maisha ya gwiji ama akiwa hai au ametangulia mbele ya haki. Simulizi itaanzia alipozaliwa, alikosoma na jinsi alivyoanza safari yake ya uandishi wa habari. Utajua maendeleo ya kazi kutokana na uchambuzi wa hatua kwa hatua jinsi alivyopanda ngazi katika uandishi wa habari, akianzia na kazi za mwanzo hadi kufikia kuwa gwiji. Utajifunza mafanikio makubwa ya kitaaluma kama vile tuzo alizoshinda, Makala muhimu alizoandika, vipindi muhimu alivyotangaza na athari kubwa alizoziacha katika tasnia ya habari. Utatambua ushawishi wake ulivyobadilisha maoni ya umma, kuchochea mijadala muhimu au kuleta mabadiliko ya kijamii, kisiasa au kiuchumi. Utajifunza maadili ya kazi kutokana na uadilifu wake katika kuripoti, jinsi alivyofuata maadili ya uandishi wa habari na jinsi alivyokuwa mfano wa kuigwa kwa wengine. Utatambua uwezo wake wa kufanya uchunguzi wa kina na kutoa taarifa zenye ukweli na zisizo na upendeleo. Utaujua mchango wake katika kutoa mafunzo na kuwaongoza waandishi wa habari wachanga na jinsi alivyokuwa na nafasi ya kuwa mlezi kwa wengine katika tasnia. Utabaini matukio muhimu ya kazi ikiwemo uthubutu wa kipekee kama vile kuripoti kutoka katika maeneo hatari au wakati wa mizozo. Utatambua sifa za kibinafsi ambazo zilimfanya kuwa mtu wa kipekee, kama vile usikivu, ujasiri, huruma au kujitolea kwa kazi yake na alivyojenga uhusiano mzuri na watu ikiwa ni pamoja na vyanzo vya habari, wenzake na wasomaji, wasikilizaji au watazamaji wa habari. Utaufahamu urithi aliouacha katika tasnia ya habari kama vile shule za uandishi alizosaidia kuanzisha, miradi ya habari aliyoshiriki au sheria na kanuni za maadili alizosaidia kuunda. Simulizi za gwiji wa habari zinajumuisha ushuhuda kutoka kwa watu waliomfahamu wakiwemo marafiki, familia na wenzake kuhusu alivyoathiri maisha yao.

> *“Utajua maendeleo ya kazi kutokana na uchambuzi wa hatua kwa hatua jinsi alivyopanda ngazi katika uandishi wa habari, akianzia na kazi za mwanzo hadi kufikia kuwa gwiji. Utajifunza mafanikio makubwa ya kitaaluma kama vile tuzo alizoshinda, Makala muhimu alizoandika, vipindi muhimu alivyotangaza na athari kubwa alizoziacha katika tasnia ya habari.”*

Kumbukizi
**Gwiji** wa Habari



# Fili Karashani

## Gwiji la Uandishi, alama isiyofutika

Saa sita na dakika ishirini na moja mchana wa Jumapili, Mei 10, 2020 nilizungumza na Kagina Karashani kuhusu maendeleo ya matibabu ya baba yake, Fili, na mipango ya kumtembelea hospitali katika mazingira ya homa kali ya mapafu (Covid-19) yaliyofanya uongozi wa Hospitali ya Muhimbili (MNH) kuamua awe anaonwa na mtu mmoja tu kwa siku!

Alikuwa amelazwa Muhimbili kwa matatizo ya moyo ambayo yamekuwa yakimsumbua kwa muda wa miaka kadhaa.

Saa sita baadaye, saa kumi na mbili na dakika ishirini na tatu, nikapokea simu ya Kagina: "Habari ni mbaya. Mzee amefariki." Anasema Kajubi.

"Nilimfahamu Fili Karugahale Karashani kama rafiki mcheshi, rafiki wa kifamilia, mtu wa masihara ambaye katika nyakati za furaha alinihakikishia kuwa ataandika wasifu wangu pindi nitakapofariki. Nilikuwa nikimjibu kuwa mimi ndiye nitakayeandika wa kwake" anasimulia rafiki wa gwiji huyu, Kajubi Mukajanga.

Anasema alimfahamu pia kama mwanataaluma mahiri wa uandishi wa habari, na mkufunzi bora. Kabla hajawa Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) walizunguka nchi nzima kufundisha maadili ya uandishi, stadi za uongozi katika klabu za waandishi, mbinu za uandishi wa uchunguzi, uandishi wa habari za uchaguzi na uandishi wa makala.

Machi 30, 2012, Fili, kama anavyojulikana kwa wengi, alikuwa mtu wa kwanza kutunukiwa Tuzo ya Maisha ya Mafanikio katika Tasnia ya Habari (Lifetime Achievement in Journalism Award) ambayo alikabidhiwa na Rais Mstaafu Jakaya Kikwete katika Ukumbi wa Diamond Jubilee. Tuzo hizo huandaliwa na MCT na washirika wake, na hutolewa katika kilele cha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT).

Alikuwa mmoja wa wanahabari Watanzania ambao usingeweza kuongelea uandishi wa habari uliotukuka bila kuwataja. Gwiji huyu alikuwa katika taaluma hii kwa miongo mitano kama ripota, mwandishi wa makala, mhariri, mkufunzi, mtafiti na mtaalamu mshauri wa masuala ya habari hapa nchi na ughaibuni. Kwa maneno yake mwenyewe, alijinasibu: "I am a child of the Media" (Mimi ni mtoto wa Tasnia ya Habari).

Fili alianza maisha ya kazi kama msaidizi wa duka la vitabu mjini Dodoma mnamo mwaka wa 1960, ambapo alijenga tabia ya kujisomea, na baadaye, kuandika. Akahudhuria warsha ya uandishi wa habari huko Kiomboi, mkoani Singida, iliyoandaliwa na *Christian African Writing Centre* iliyokuwa na makao makuu Kitwe, Zambia, na kumaliza akiwa mwanafunzi bora darasani. Ushindi huo ulimwezesha kupata udhamini wa kusomea cheti cha uandishi huko Kitwe, akiwa mmoja wa vijana 30 waliokusanywa kutoka Kusini, Mashariki na Magharibi mwa Afrika. Baada ya kupata cheti chake akaajiriwa kama ripota katika magazeti ya *Target* na *Lengo*, ambayo yalikuwa ndiyo kwanza yameanzishwa kwa ushirikiano kati ya mabaraza ya Kikristo ya Kenya na Tanzania.

Miaka miwili baadaye mwajiri wake akampeleka kusomea Diploma ya Uandishi iliyoandaliwa na taasisi ya kimataifa ya wahariri, *International Press Institute*. Kwa mara nyingine, Fili akawa wa kwanza katika darasa la wanafunzi 30 toka Kusini na Mashariki mwa Afrika.

"Wakati wa sherehe za mahafali, Mhariri wa Taifa Leo, linalochapishwa na Nation Media Group (NMG) ya Kenya akamfuata na kumweleza kuwa angependa kumpa kazi. Fili akakubali. Hiyo ilikuwa mwaka 1964. Miezi mitatu tu baadaye, wahariri wa Daily Nation, gazeti jingine la NMG, "wakamwiba" toka gazeti lao dada. Akaingia chumba cha habari cha gazeti lao la Kiingereza akiwa Mtanzania pekee" Anasimulia Kajubi Mukajanga.

Tangu hapo, Fili hakuwahi kutazama nyuma.

Kwa Fili, ukweli na usahihi (truth and accuracy) ndiyo msingi wa uandishi wa habari. Mhariri wake wa habari pale Daily Nation, Mike Chester, alikuwa kati ya watu waliosaidia kumfinyanga Fili kuwa gwiji wa taaluma hiyo. Chester hakuwa na masihara kazini, na kwake, stori ilikuwa haijakamilka bila kujibu maswali "kwa nini" na "kwa jinsi gani".

Kati ya kazi alizofanya wakati huo ni pamoja na kuripoti machafuko ya kijamii, ukame na njaa huko Wajir, mpakani mwa Kenya na Somalia. Baadhi ya stori alizoandika zilimuudhi aliyekuwa Waziri wa Kilimo wa Kenya wakati huo, Jeremiah Nyagah. Lakini ukweli na usahihi ukamwokoa, hakufanywa chochote.

Aliandika pia matatizo ya wananchi huko Baringo, jimboni kwa Daniel Arap Moi, wakati huo akiwa Makamu wa Rais na Waziri wa Mambo ya Ndani. Mzee Moi hakupendezwa sana na stori za Fili, na akaagiza aletwe kwake. Alipofika, akamtazama Fili kwa mshangao toka chini hadi juu na kumaka, "Oh, huyu ndiye Karachani – nilidhani ni Mhindi! Kwenda!"

Awali, lengo lilikuwa kumsweka korokoroni. Ukweli na usahihi vikamwokoa.

Tom Mboya alipouawa, Fili ndiye aliyeliandikia Daily Nation mkasa huo.

Mwaka 1967 akahamishiwa Dar es Salaam kwa mwaka mmoja na kuendelea kupeleka Nairobi stori kemkem. Asilimia kubwa ya stori za Tanzania zilizochapishwa ukurasa wa mbele wa Daily Nation wakati huo ziliandikwa na Fili.

Aliporudi Nairobi, Fili alikwea vidato toka ripota hadi mwandishi mkuu wa habari za Bunge, akawa pia mwanasafu, na baadaye Mhariri-usu/Msanifu Habari (Sub-editor). Alikuwa pia akiandika safu kuhusu masuala ya Tanzania katika gazeti hilo lililoongoza kwa mauzo Afrika Mashariki.

Baadaye akaacha kazi na kujiunga Chuo Kikuu cha Dar e Salaam na kupata shahada yake ya kwanza mwaka 1978, kisha shahada ya uzamili toka Chuo Kikuu cha Queens, Canada, mwaka 1981.

Baada ya chuo kikuu Fili akajiunga na gazeti la Daily News kabla ya kuwa mkufunzi katika Chuo cha Uandishi wa Habari Tanzania, TSJ. Akiwa mkufunzi, akawa pia akiandikia majarida na taasisi za nje zikiwamo jarida maarufu la Africa Now na shirika la Inter Press News Agency (IPS). Kwa bahati mbaya, jambo hili lilitafsiriwa na wakubwa wake kuwa ni "kufanya kazi mbili", japo kwake yeye aliona ni njia ya kuwaonyesha wanafunzi kwa vitendo jinsi uandishi bora ulivyo. Alipoona anasakamwa sana, akaacha kazi na mara moja IPS wakamchukua na kumpa kazi Roma, Italia, na baadaye wakampeleka Harare, Zimbabwe, kama Mkuu wa Kituo (Bureau Chief).

Aliporudi Tanzania 1989 akawa Mhariri mwanzilishi wa Business Times, akiwa na kina Rashid Mbuguni, Narendra Joshi, Ali Chimbyangu na Richard Nyaulawa.

Mwaka 1991 Fili Karashani aliajiriwa kama Mhariri wa Southern Africa Economist jijini Harare, kabla ya kurudi Dar es Salaam na kuwa Mhariri mwanzilishi wa The Guardian na baadae Sunday Observer.

Mnamo 2004 hadi 2005 alikuwa The Citizen kama Mhariri wa Mafunzo.

Katika miaka ya mwisho ya maisha yake, Fili Karashani , ambaye waandishi wengi wamepitia mikononi mwake akiwa mhariri na mwalimu, aliendelea kutoa mafunzo ya uandishi, hususan uandishi wa habari za uchunguzi, makala, na maadili. Alitoa pia huduma kama mtaalamu




*Rais Mstaafu Jakaya Kikwete akiwa kwenye picha ya pamoja katika meza kuu na kulia kwake ni washindi Fili Karashani (Tuzo ya mafanikio ya maisha) wakati wa hafla ya Tuzo ya Wanahabari Bora 2011 katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.*

mshauri wa masuala ya habari, huku akichangia katika majarida ya kitaaluma yakiwamo Scribes la MCT na The Global Journalist la Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Missouri, Marekani.

Vitabu alivyoandika au kushiriki kuandika ni pamoja na: To Write or Not to Write – Ethical Concerns in Journalism; Poverty Reporting – A Manual for Tanzanian Journalists; Media Ethics: Duties and Responsibilities; Feature Writing Manual na Investigative Journalism Practice in Tanzania.

Fili Karashani alizaliwa Agosti 23, 1938 mjini Dodoma. Baba yake alikuwa Yakobo Kagina, mchungaji wa kanisa la Anglikana, na mama yake aliitwa Blandina.

Fili na mkewe, Geraldina, walijaaliwa watoto watano: Magezi, Baraka, Kagina, Koku na Bahati. Baraka, aliyechukua kazi ya baba yake ya uanahabari, alishatangulia mbele ya haki. Fili pia ameacha wajukuu wanane. (Maelezo hayo ni kwa hisani ya Kajubi Mukajanga)

# **Anayeinukia** kwa Umahiri wa Habari

Karibu katika simulizi ya kijana anayeinukia kwa umahiri wa habari. Utajifunza kuhusu kijana mwenye kipaji na mdogo zaidi miongoni mwa wateule wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari au aliyeibuliwa na watafiti huru waliowekwa kufuatilia vijana waandishi wa habari wenye vipaji. Lengo ni kukuza ubora wa vijana ambao unawapa kazi wafuatiliaji kubaini umuhimu wa vijana kwa mafanikio ya baadaye kutokana na jinsi ambavyo hata sasa wanajikita vema katika ulimwengu wa uandishi wa habari. Vijana wenye vipaji, msukumo na wanaozingatia maadili wanajiweka katika nafasi nzuri ya kuwa viongozi wa baadaye katika sekta ya habari. Simulizi ya maisha yao inaanzia shuleni, waliowashawishi kuingia katika taaluma ya habari, mafanikio ya ujana wao katika uandishi wa habari, ujuzi na uimara, viwango vya kimaadili na uadilifu, maono binafsi na Mwanaumengo, ushawishi na mguso, changamoto na ustahimilivu, udadisi na shauku, sifa za uongozi na maono kwa sekta ya habari.

> “*Lengo ni kukuza ubora wa vijana ambao unawapa kazi wafuatiliaji kubaini umuhimu wa vijana kwa mafanikio ya baadaye kutokana na jinsi ambavyo hata sasa wanajikita vema katika ulimwengu wa uandishi wa habari.*”

**Anayeinukia**
kwa Umahiri wa Habari



# Lukelo Francis

## Chipukizi, anayeonyesha njia kwa vijana kuwika katika tasnia ya habari

**Florence Majani. MCT**

Katika tasnia yenye kupanda, kushuka, shida na raha zikiwamo, wachache wameweza kung'ara kwa haraka kama ilivyotokea kwa Lukelo Francis. Lukelo, kijana wa miaka 25 tu, ambaye ni miongoni mwa wateule wenye umri mdogo zaidi katika Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) za mwaka huu, anasimama kama somo kwa vijana wanahabari ambao wanadhani ili kufanikiwa ni lazima uwe umekaa ndani ya chumba cha habari kwa miaka mingi.

Ameingia rasmi katika tasnia mwaka 2021, mara baada ya kumaliza shahada yake ya kwanza ya mawasiliano ya umma katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (SJMC).

"Niliona tangazo la kazi lililotolewa na kampuni ya habari ya The Chanzo, nikaomba na kwa bahati nzuri nikafanikiwa kupata nafasi kama mwanahabari mnamo Julai mwaka 2021," anasema.

Lukelo na uchanga wake katika tasnia ya Habari, ameweza kuibua habari lukuki ambazo zimemuwezesha kushinda tuzo za EJAT mara tu baada ya kuanza kazi, 2021.

"Ripoti yangu niliyofanya mwaka ule wa kwanza nilipoanza kazi, niliiwasilisha kwenye tuzo za EJAT na mwaka 2022, ikashinda," anasema

Mwaka 2022 aliwasilisha kazi EJAT aliingia kama mteule lakini makala yake haikushinda na mwaka huu 2023, ameibuka tena mteule.

Makala ama Habari za Lukelo zinajikita katika masuala ya uwajibikaji, na zinazogusa maisha ya watu katika jamii yake, si mara zote zikaandikwa au kurushwa na hali ikawa salama salmini, mara kadhaa amekutana na changamoto, na hapa anatoa mfano: "Nimeshawahi kutishiwa kushtakiwa baada ya kuchapisha Habari fulani, lakini changamoto nyingine, ni pale unapohitaji kupata taarifa lakini vyanzo vya taarifa havitaki kutoa," anasema




*Lukelo F. Haule akipokea Tuzo ya Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora kutoka kwa Bi. Stellah Lupimo, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC.*

**KIPI KILICHOMVUTIA KATIKA UANDISHI WA HABARI?**

"Kwanza mimi naupenda uanahabari, lakini wapo watu ambao wamenishawishi na kunitamanisha kuingia kwenye hii tasnia wapo wawili, Jenerali Ulimwengu, huyu mwandishi mkongwe, amenipa hamasa kubwa na, wa pili ni Salim Kikeke, ambaye nimekuwa nimuangalia sana wakati nakua, ni mtangazaji mzuri,"anasema.

Anasema hakulazimishwa wala kushikwa mkono na yeyote ili kuwa mwanahabari bali ni yeye mwenyewe ndiye aliyechukua fomu na kuomba kozi hiyo SJMC.

Kuhusu uchanga wake katika tasnia na mafanikio haya ya kazi zake kutambulika, Lukelo anasema anapata ari ya kufanya kazi kwa bidii zaidi.

"Sikujua kama mimi ni mchanga kuliko wateule wengine, jambo hili linanipa moyo wa kuendelea kuandika habari zinazogusa maisha ya watu," anasema na kuongeza: "Hakuna uhusiano wowote wa umri na kupata tuzo, yeyote mwenye juhudi anaweza akafanikiwa. Mimi ninaamini katika uwezo na haijalishi umri."

Kijana huyu, hasiti kumtaja Khalifa Said muasisi wa The Chanzo kuwa ndiye mwalimu na mhariri wake.

"Mhariri wangu, ambaye amenitengeneza ni Khalifa. Habari zangu zinapita kwake, hizo stori zote zilizowahi kuingia katika tuzo, amenihariria na kunishauri yeye. Mimi ninamuangalia yeye, na ninapenda anavyonishauri," anasema.

Ushauri wa Lukelo kwa wanahabari wachanga ni huu: “Kazi ya uandishi ya uanahabari ni kazi ngumu, ina mambo mengi. Kwa hiyo cha kwanza kabisa uipende, na ujue umekuja kufanya nini kwenye tasnia hiyo.Ukiyajua hayo, kazi hii itakuwa rahisi sana. Utakuwa na uwezo wa kufuatilia, kuchambua mambo na hii itakusaidia hata kupata tuzo. Kazi yako itakutambulisha endapo tu utafanya juhudi,” anasema.

Ndani ya The Chanzo, Lukelo ni zaidi ya nyota, anatajwa kama msaka ukweli, msaka habari za kina na mchambuzi mahiri wa ripoti.

Kwa mujibu wa Khalifa, kiongozi na mhariri wake, Lukelo anaongozwa na shauku isiyo na kikomo katika kazi zake, na hilo limemfanya akabiliane na stori bora zaidi kuliko wengine.

“Ujasiri wake na namna anavyoipenda taaluma, kumemfanya aanze kuyaona mafanikio ya tasnia hii mapema zaidi,” anasema Khalifa.

Lukelo mtoto wa pili kati ya wawili, wa familia ya Mzee Francis Haule, amezaliwa na kukulia mkoa wa Njombe, akipata elimu yake ya msingi, Shule ya Msingi Mpechi iliyopo Njombe na baadaye elimu ya sekondari katika shule ya Hagafilo, Njombe na baadaye kidato cha tano na cha sita shule ya sekondari ya wavulana ya Rungwe, Mbeya.

Historia yake haikumzuia kufanya kazi yake kwa umahiri akizichambua taarifa katika mifumo ya kidijitali.




*Lukelo F. Haule akielekea kupokea Tuzo yake ya Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora.*

# **Jicho** la Wahariri

Karibu katika jicho la wahariri. Hii ni fursa ya mhariri kutoa maoni kuhusu mwenendo wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa kuangazia mambo kadhaa muhimu ili kuhakikisha tuzo zinaleta heshima kwa tasnia ya habari na kuhamasisha waandishi wa habari wengine kufuata nyayo. Maoni yao yatazingatiwa katika kuboresha tuzo zijazo. Moja ya mambo yanayoangaziwa ni pamoja na ukweli na usahihi wa habari inayopewa tuzo, uwiano na haki, uchambuzi wa kina, utumiaji wa vyanzo, ubunifu wa lugha, mchango kwa jamii, ujasiri na uthubutu, matumizi ya kiteknolojia, mbinu za kipekee kutofautisha na habari nyingine za kawaida, uthabiti wa maadili ya uandishi wa habari, ubora wa uhariri

VIDEO AUDIO PHOTO WEB



# Wahariri
## watoa ya moyoni

HAKUNA ubishi kuwa wahariri waliotoa maoni yao kuhusu Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) zinazoratibiwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa niaba ya wadau wengine maslahi na tasnia ya habari nchini wanakubaliana kwamba tuzo hizo ambazo sasa zinaingia muongo mmoja na nusu, zimesaidia kukuza ubora wa kazi za waandishi wa habari nchini na hivyo kusaidia kuibua uwajibikaji kwa wenye mamlaka.

Wakitoa maoni yao kwa nyakati tofauti, wahariri hao walisema tuzo hizi zimesaidia kuwasukuma waandishi wa habari kufanya kazi kwa weledi zaidi kwani ili kuwasilisha kazi zao kwenye tuzo inabidi ifanyiwe kazi ya ziada ili kukidhi vigezo vilivyowekwa ambavyo vinazingatia msingi bora ya taaluma ya uandishi wa habari.

"Kuwepo kwa tuzo kumeongeza chachu ya wandishi wengi kuongeza umakini katika kazi zao. Nikitolea mfano wa Mwananchi waandishi wengi wamekuwa wakipambana kuandika kazi zenye weledi ili nao waingie katika hicho kinyang'aniro," amesema Rashid Kejo Mhariri wa Mafunzo wa Kampuni ya Mwananchi Communications (MCL) ambao ni wachapishaji wa magazti ya The Citizen, Mwananchi na Mwanaspoti na wamiliki wa Mwananchi Digital.

Kejo ameongeza kwamba kwa MCL wanazichukulia tuzo za EJAT kuwa ni za heshima kubwa na zenye kujenga taswira bora ya chombo cha habari katika mwelekeo chanya. Waandishi wa MCL kwa miaka mingi sasa wamekuwa wakipata tuzo mbalimbali ikiwamo ya mshindi wa jumla mara kadhaa.

"Sisi tuna slogan (kauli mbiu) inayosema tunaliwezesha taifa," anasema na kufafanua kwamba katika kutelekeza kauli mbiu hiyo ni kwa kuwazesha wananchi wawe na taarifa sahihi za kuwawezesha kuamua juu ya mustakabali wao. Anasisitiza habari hizi ni lazima ziwe na matokeo chanya kwa jamii.

Anaeleza kwamba ndiyo maana wamekuwa wanashirikiana na taasisi kama Tanzania Media Foundation (TMF) kuangalia habari zenye tija, ambazo kwao siyo tu zimewafanya waandishi wao kupata tuzo nyingi, bali pia zinazoleta matokeo chanya kwa jamii.

Hata hivyo, Kejo anashauri yawepo maboresho katika kutoa tuzo kwa kuangalia habari ambazo zimeandikwa kwenye tovuti mbalimbali na waandishi wa nje ya Tanzania, lakini zikaleta matokeo chanya. Kwa maana hiyo, anashauri pia kuwepo kwa tuzo kwa kundi la waandishi wa habari ambao wameitangaza Tanzania kimataifa.

"Kwamba wameandika stori ambayo imeleta impact (matokeo) kimataifa, siyo kitaifa tu," anashauri kwa kuwa tovuti zinasomwa duniani kote siyo ndani ya nchi tu.

Kejo anashauri pia ziingizwe tuzo mpya za mwandishi anayechipukia, kwani kwa kufanya hivyo itasaidia waandishi wachanga kuona kwamba nao kazi zao zinathaminiwa, pia itawapa chachu ya kufanya kazi vizuri zaidi.

Mhariri Mtendaji wa UTV, Frank Sanga anasema kwamba kuwapo kwa tuzo za EJAT ni jambo zuri ambalo kwake anaona lina faida kuu tatu. Mosi, zinafanya uandishi wa habari uwe na heshima;

pili, zinafanya uandishi wa habari uwe na viwango vyake, kwa sababu mtu anapotaka kushinda tuzo ni lazima ajiwekee Mwanaumengo ya kufanya kazi kwa viwango kama vilivyowekwa na tuzo.

Anasema kwa kufanya hivyo inaufanya uandishi wa habari uendelee kuwa juu. Anaeleza kwamba pamoja na kuwepo kwa changamoto katika uandishi wa habari, ni hakika bila tuzo za EJAT uandishi wa habari ungekuwa wa ovyo sana kwa hali ilivyo nchini kwa sasa; na tatu tuzo hizi zinaleta umoja kwani kila mwaka waandishi wanakaa pamoja kusheherekea.

Sanga ambaye kabla ya tuzo za waandishi wa habari kuratibiwa kwa pamoja chini ya MCT alipata kushinda tuzo ya mwandishi bora wa mwaka 2003 wa habari za michezo zilizokuwa zinaratibiwa na Chama Cha Waandishi wa Michezo Tanzania (TASWA), anaeleza kuwa tuzo za EJAT zinaleta ushindani.

"Uandishi bila ushindani unakuwa siyo mzuri sana. Kama chombo hiki kimepata tuzo nyingi mwaka huu, chombo kingine kinasema mwakani tutafanya kazi nzuri zaidi ili nacho kishinde. Ule ushindani tu unafanya uandishi wa habari uwe juu," anasisitiza Sanga.

Anapendekeza kwamba kama ikiwezekana kuwe na mfumo kupata kazi za kushindanisha waandishi wa habari kupitia kamati itakayokuwa anafuatilia kazi hizo kwenye magazeti, runinga na redioni.

"Kuwe na kamati maalum ya kufuatilia habari nzuri. Naamini pale MCT wanapata magazeti yote kila siku. Ukienda pale TCRA (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania) wanaona vipindi vya televisheni vyote kila siku. Kwa hiyo, badala ya mtu kupeleka kazi zake MCT kwa kushirikiana na TCRA waangalie maudhui ya TV na redio," anasema na kuongeza kuwa anajua kuwa kazi hiyo ni ngumu sana, lakini itasaidia kupata hata kazi ambazo ni nzuri, lakini waandishi wake hawapeleki MCT ili zishindanishwe.

"Mimi niliposhinda wala nilikuwa sijui kama nimeshinda. Sikuwa nimepeleka kazi. Niliambiwa tu nimeshinda na wala sikuwa Dar es Salaam. Nilikuwa Mwanza kuripoti mechi ya Simba na Enyimba, nikaambiwa tu nimeshinda tuzo hiyo," anakumbuka kwamba mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika ukumbi wa Diamond Jubilee alikuwa Jakaya Kikwete wakati huo akiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Tuzo yake alipokelewa na mfanyakazi mwenzake, Selemani Mbuguni, wakifanya kazi wote Kampuni ya Business Times (BTL).

Mhariri Mkuu wa kituo cha runinga cha Channel Ten, Esther Amandus Zelamula anasema kwamba tuzo za EJAT ni nzuri kwa sababu zinahamasisha waaandishi kushiriki kikamilifu. Pia ameongeza kwamba kwa kuwa kazi zinazoshindanishwa ni zile zilizofanyiwa utafiti wa kina, zinakuwa na manufaa makubwa kwa jamii.

"Kubwa ninaloliona mimi uwepo wa tuzo hizi wajaribu kuwa wanatoa maelekezo ya mara kwa mara ili wengine ambao hawajapata taarifa za kutosha waweze kushiriki wengi zaidi. Unajua ni walewale wanashiriki mara kwa mara kwa sababu tayari wana ufahamu wa kutosha," anafafanua Zelamula.

Anaeleza kwamba wapo ambao hawana taarifa au wanajisahau na wakija kushtuka tayari muda wa kushiriki na kuwasilisha kazi zao unakuwa umekwisha kupita.

Anaeleza faida za kuwakumbusha mara kwa mara waandishi juu ya shindano la EJAT watapiga hatua mbele na kuacha kuandika habari za kawaida za chanzo kimoja tu cha habari, na kujikita katika kuandika makala na kuandaa vipindi kwa kufanya utafiti wa kina zaidi hivyo waandishi kujijengea uelewa zaidi wa mambo.

Zelamula anashauri kwamba majaji wanaopitia kazi za waandishi wa habari ambazo zimewasilishwa

kwa ajili ya kushindanishwa, ni vema wakawa na utaratibu wa kufanya mrejesho kwa waandishi juu ya kasoro ambazo zilionekana kwa nia ya kuwajengea zaidi uwezo. Anasema makosa yanayobainika yawe ndiyo msingi wa kutoa mafunzo, ili kuwasaidia kuboresha zaidi kazi zao kwa kujifunza kutokana na makosa yao wenyewe.

Mhariri Mkuu wa Habari Leo, Mgaya Kingoba mbali ya kupongeza tuzo hizo kwamba ni nzuri, anashauri utafutwe utaratibu mwingine wa kupata kazi za waandishi za kushindanishwa. Anaamini wengi wanapeleka kazi zao ili washinde, lakini ingeliwezekana MCT ndiyo iwatafute.

Anafafanua kuwa anajua MCT wanafuatilia kazi za vyombo vya habari kila siku, na wamekuwa na utaratibu wa kuwapigia simu wahariri kama wakigundua kuwapo kwa makosa ya kitaaluma kwenye kazi zilizochapishwa.

"Kwa nini basi kwa zile kazi zilizokwisha kupitiwa na MCT na zikaonekana ni nzuri zisichukuliwe? Ingefaa zikapelekwa kwenye jopo zikapitiwe badala ya waandishi kupeleka wenyewe," anaeleza Kingoba.

Kingoba anasema kwa kawaida waandishi wanawasilisha kazi nyingi sana kwa MCT kwa ajili ya kushindanishwa, lakini zinazokidhi vigezo ni chache kutokana na kushindwa kufikia viwango vilivyowekwa. Anaeleza hali hiyo huenda inatokana na uandishi duni ambao labda hauna vyanzo vingi vinavyorejewa katika habari husika.

Kwa maana hiyo, anashauri kwamba MCT iwe na mpango wa kusaidia waandishi kwa kuanzisha mafunzo ya uandishi bora ambao unazingatia viwango, ili hata kazi zitakazokuwa zinawasilishwa zifikie vigezo vilivyowekwa.

Kingoba anashauri kuongezwa kwa kundi la habari za nishati safi, kwa kuwa sasa ni ajenda siyo ya Tanzania tu, bali ya dunia nzima.

Joyce Shebe, Mhariri Mkuu wa Clouds Media Group, anapongeza tuzo za EJAT, kwake haziangalii kama tuzo tu bali fursa ya kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Anaeleza kuwa fursa hiyo inawapa watu morali wa kufanya kazi kwa bidii na kushindana miongoni mwa waandishi kwani kila anayepata anaongeza juhudi zaidi ili mwaka mwingine aweze kufanya vizuri zaidi.

"Kikubwa zaidi kwangu mimi hizi tuzo zimetuonesha kwamba ni jukwaa kubwa na zuri kwa wanawake kuonyesha umahiri wao, kuonyesha uwezo wao," amesema na kuongeza kwamba wanahabari wanawake wanashiriki kwa wingi sana na imeshuhudiwa wakitwaa tuzo ya jumla.

Anaeleza hali hiyo inaonyesha kuwa tuzo hizo ni ulingo sawa kwa wanawake na wanaume ambao ni waandishi wa habari kushiriki pia kushinda.

"Haiangalii huyu ni mwanamke ashinde yeye au huyu ni mwanaume ashinde yeye. Hapana. Watu wote wanashinda kulingana na vigezo vilivyowekwa, sifa zilizowekwa au zinazotakiwa za mtu kushinda au kushiriki," anasisitiza Sheba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Mbali ya kukiri kwamba tuzo hizo mwaka baada ya mwaka zinazidi kuboreshwa, pia ameeleza kuwa ni ulingo unaotoa fursa sawa kwa wanahabari wote kushiriki bila kujali anatoka mjini au kijijini. Kadhalika, hazibagui chombo chochote cha habari, kiwe mjini au kijijini, kila mmoja anakuwa na haki sawa ya kushindanisha kazi zake kwenye shindano hilo la kila mwaka.

# Jicho la Majaji

Karibu katika jicho la majaji. Hii ni fursa ya jopo la majaji kwa umoja wao kueleza walivyozingatia vigezo muhimu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kazi bora kabisa inatambuliwa na kutuzwa. Kigezo cha kwanza ambacho majaji wanapaswa kuangazia jicho lao na kukisimulia ni ubora wa uandishi na uwasilishaji ambapo wataangazia uandishi wa kina, ufasaha na mtiririko na ubunifu katika uwasilishaji. Kigezo cha pili ni Uadilifu na Maudhui ambapo wataangazia usahihi na ukweli, haki na uwiano. Kigezo cha tatu ni Uwezo wa Kuathiri Jamii ambapo wataangazia athari kwa jamii kwa kuangalia kama kazi hiyo imechangia kuhamasisha mijadala, kubadili sera au kutoa mwamko juu ya masuala muhimu. Pia wataangazia umuhimu wa mada kama iliendana na masuala ya wakati huo. Kigezo cha nne ni Ujasiri na Uthubutu ambapo wataangazia namna mwandishi alivyokabiliana na vikwazo na uchunguzi wa kina kwa maana ya kuonesha uthubutu katika kuchunguza masuala ambayo ni magumu au yenye hatari kama vile ufisadi, ukiukwaji wa haki za binadamu au masuala ya usalama. Kigezo cha tano ni Maadili ya Uandishi wa Habari ambapo wataangazia habari ilivyozingatia maadili ya kitaaluma na pia wataangazia uwajibikaji kwa umma. Kigezo cha sita ni Mchango wa Kitaaluma ambapo wataangazia ushawishi wa kazi ya mwandishi kwamba inachochea au kutoa mfano kwa waandishi wengine kwa ukuaji wa taaluma ya uandishi wa habari. Pia wataangazia kujitolea na ari ya mwandishi katika kazi yake, ikiambatana na juhudi kubwa za kukamilisha habari kwa ubora. Kigezo cha saba ni Ubunifu na Matumizi ya Teknolojia ambapo wataangazia ubunifu wa kipekee katika ukusanyaji, uwasilishaji au usambazaji wa habari. Pia wataangazia matumizi ya teknolojia na kama yameongeza ufanisi wa kazi ya mwandishi. Kigezo cha Nane ni Ushiriki wa Kijamii na Ushawishi ambapo wataangazia jinsi habari hiyo ilivyopokelewa na wasomaji, watazamaji au wasikilizaji na jinsi ilivyochangia katika kuhamasisha mazungumzo ya kijamii au kuchochea mabadiliko. Pia wataangazia ushawishi na usikivu kwa kuangalia uwezo wa habari kushawishi maoni ya umma na kuwa na ushawishi mkubwa kwa wasomaji, watazamaji na wasikilizaji.



# Yaliyojificha nyuma ya pazia majaji wakipitia kazi EJAT 2023

**Na Salome Kitomari**

UBORA za kazi za uandishi wa habari kwenye magazeti na redio umeonyesha kuwagusa majaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2023, huku kiwango hicho kikikosekana kwa maudhui mtandaoni kwa kile kinachoelezwa ni kushindwa kutambua wasomaji halisi.

Aidha, habari za matukio zinaelezwa kuwa nyingi ambazo zilisukumwa na waandishi kualikwa kwenye tukio fulani, jambo ambalo ni vigumu kupata umahiri wa uandishi.

Jaji Kiongozi Halima Shariff anasema: "Tulifanya kazi kuanzia asubuhi hadi saa tano au sita usiku; tukianza kundi fulani ilikuwa lazima twende nalo hadi mwisho. Pia hakuna jaji ambaye unamuona anaegemea upande wowote, walikuwa na uadilifu wa hali ya juu, wakati mwingine kusaini fomu maalum ya mgongano wa maslahi.

Anasema walipangiana kazi na kwamba sio kila jaji alipitia kila kipindi au gazeti bali waligawana ili kuhakikisha kazi inakuwa rahisi na waliongozwa na vigezo, na wakati mwingine wanasikiliza au kusoma zaidi ya mara moja kabla ya uamuzi.

"Kulikuwa kuna kuchoka sana, kucheka sana ili kuifanya kazi kuwa rahisi. Kwangu ilikuwa ni mara ya kwanza ila ilikuwa ni wakati mzuri sana kwangu," anasema.

## Maudhui mtandaoni

Kiongozi wa jopo la majaji Halima anasema walibaini kuwa vyombo vya mtandaoni bado vina tatizo la maudhui ambalo linapaswa kuimarishwa.

Aidha, anasema walipokea kazi nyingi za mtandaoni na wengine wakiandika makala ndefu kama ya gazeti, picha zisizo na ubora, usimuliaji unaopishana na picha na wakati mwingine kujirudia.

"Wachache walitumia *'hyperlink'*, wengi walielezea sana jambo ambalo sio sawa kwa maudhui mtandaoni. Lazima jambo hili liangaliwe," anasema.

Kauli hiyo inaungwa mkono Katibu wa jopo ya majaji Dkt. Egbert Mkoko akisema: "Huwezi kuchukua makala ya gazeti namna ilivyo na kuipeleka mtandaoni na kudhani itamvutia msomaji, hawa ni wasomaji wa aina mbili tofauti ambao wanahitaji aina tofauti za maudhui. Moja ya kazi ilikuwa na aya 64 ambayo huwezi kumpata msomaji mtandaoni."

Aidha, Jennipher Sumi anasema eneo la mtandaoni liko nyuma na zinahitajika jihitada na uwekezaji ili kutengeneza maudhui mazuri, na kwamba kazi za magazeti zilihamishiwa huko. "Tulikutana na habari yenye aya zaidi ya 60 imewekwa digital, watu hawataki mambo marefu; tunatarajia tuone *'hyperlink'* na sio kubwaga yote hapo," anasema.

"Unakuta mtu ameleta kazi yake ila ukibonyeza *link* inakutaka ulipie, unaona mtu anajiangusha mwenyewe, alipaswa kuweka utaratibu mzuri ili kazi yake iwafikie majaji. Bado naona vyombo vingi vya mtandaoni havijajua walaji wao au wanataka nini; lazima kuwekeza ili kupata matokeo chanya," anasema Jennipher.

### Kazi ya uhariri

Jaji Absalom Kibanda anasema aliona kazi ambazo ziliandikwa na waandishi lakini zilizoboreshwa na wahariri, jambo lililodhihirisha kuwa ubora wa kazi unategemea watu wote wawili.

"Zipo kazi unaona kabisa iliandikwa na huyo huyo, akahariri na kuitumia bila kuwa na jicho jingine. Unakutana na makosa kuanzia mstari wa kwanza na hii ilikuwa kwenye magazeti na mtandaoni."

### Habari za matukio

Halima anasema: "Binafsi niliona makala nyingi zilikidhi vigezo vya kitaaluma vya 5W+H. Nyingine zilikosa ushahidi zimewekwa tu. Wengi bado wanaandika habari za matukio hawajajiongeza zaidi kupata kitu cha tofauti," alisema.

"Hakuna kujituma kwenda hatua ya ziada, mwandishi kaandika, so what (kwa hiyo?). Tumeona sana kwa walioandika makala zilizofadhiliwa kwamba mwandishi alipelekwa mahali na watu fulani kuandika habari zao.

"Kupelekwa mahali na chanzo ni sawa ila ni wajibu wa mwandishi kuchimba kwa kina kupata habari ambayo haipo, mtu akisikiliza aone kuna kitu. Zote tulizozichagua tulizingatia sana hilo kwa sababu tunataka uandishi ubadilike ili tunaposema vyombo vya habari ni muhimili wa nne iwe ni halisi. "Hapo bado sana tunahitaji kufanya kazi ya ziada, ili mwandishi asiishie kuripoti tu zimeongezeka kutoka asilimia 25 kwenda asilimia fulani, tueleze ongezeko hilo lina maana gani kwenye jamii yetu." Kauli hiyo inaungwa mkono na Dkt. Mkoko ambaye anasema waandishi wengi walionyesha walisubiri matukio au siku rasmi ndipo wapate habari ya kuandika, jambo ambalo sio sahihi.

"Wale ambao walijiongeza hawakutegemea matukio ndio wafanye habari bora, wamefanya habari nzuri sana. Mtu anasubiri siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia wakati ukatili upo miaka yote, maana yake umesukumwa na tukio au siku husika ndipo ukapata habari. Huwezi kuwa na habari yenye kuleta matokeo kwenye jamii," anafafanua. "Ipo haja ya wahariri kuwasaidia waandishi wao kukua, waachane na habari za matukio bali wawe na habari zilizotokana na mawazo binafsi au yaliyoanzia ndani ya chombo cha habari," anasema Dkt. Mkoko.

Kauli hii pia inaungwa mkono na Jennifer ambaye anasema kazi nyingi zilikuwa za kukimbizana na matukio.

"Vyombo vingine vilionyesha kuwa waandishi wao wavivu, hawakujiongeza; waligeuka kuwasemea viongozi, taasisi, ndio maana hatukuwa na habari za uchunguzi," alisisitiza Jennifer .

Jennifer alisema kazi nyingi zilizopitiwa moja kwa moja zilionyesha zilikuwa zimewezeshwa na vyanzo vya habari, huku wengine wakijikita kwenye habari za kusikia, huku waliojiongeza wakiandika habari zilizotoa matokeo.

### Vyanzo vya habari

Jaji Kiongozi Halima anasema waandishi wengi walijitahidi kuwa na vyanzo vingi lakini vingine visivyohusika na kile anachokiandika jambo lililosababisha kukosa mwelekeo na kumpoteza msomaji.

Kibanda anasema, "Kulikuwa na tatizo kwenye kupata vyanzo sahihi kulingana na mada husika, mwingine aliweka vyanzo ili kutimiza uwepo wake. "Ni vyema ikaeleweka hata walioshinda sio kwamba walipata alama asilimia 100 bali walipishana kwa alama chache. Kuna waliopata alama 85, 95, 75 au 71. Kuna mapungufu hadi kwenye misingi ya kitaaluma," anasema.

Adha, Jennifer anasema walikutana na habari zimeandikwa bila chanzo, jambo ambalo halikupaswa kuwa hivyo kitaaluma.

### Ubora wa kazi

Hata hivyo kiongozi wa jopo Halima Shariff anasema kuna hali ya kuongezeka kwa ubora

katika uwasilishaji, kuzingatia taaluma, mtiririko na kutafuta ushahidi wa data ambazo ni muhimu.

"Hili nimeliona kwenye magazeti, TV na redio lakini tukiangalia kwa ujumla sio wengi maana ilitarajiwa ushindani ungekuwa mkali sana kwamba kazi 200 hadi 300 zingekidhi vigezo. Hatujafika kiwango cha aina hiyo lakini ubora upo," anasema Halima. Aidha, anasema kwenye magazeti msomaji anaposoma aya tatu za mwanzo lazima zimpeleke kwenye mada, lakini habari nyingine walisoma aya nyingi na bado hawakuona jambo mwandishi alilotaka kuzungumzia jambo linalompoteza msomaji.

Jaji mwingine Mkumbwa Ally, anasema kwa ujumla ubora wa uandishi umeongezeka kidogo, ingawa kuna udhaifu katika kuandika kwa kina, mizania na ndio maana nusu ya kazi hazikufaulu.

"Hatukukutana na ubora wa kupigiwa mfano. Vinara walioonekana ni wale wale wa miaka iliyopita ikiashiria ukosefu wa uhai kwenye vyombo. *Story telling* (uwezo wa kusimulia) haijaboreka," alieleza Mkumbwa ambaye aliongoza jopo la majaji wa (EJAT) 2022.

Dk. Mkoko anasema: "Ubora kwenye magazeti unazidi kukua siku hadi siku na kwenye redio niliona wengi wanaandika script na kipindi kimeandaliwa vyema... kwenye TV na mtandaoni bado kuna kazi kubwa inapaswa kufanyika."

**Maadili**

Jaji Kiongozi Halima anasema waandishi wengi walizingatia maadili ingawa kulikuwa na kazi chache ambazo hazikukidhi vigezo hivyo kama matumizi ya picha za watoto na wenye ulemavu hasa kwenye runinga na mtandaoni.

Jaji Mkumbwa anasema kuna tatizo kubwa la kuzingatia maadili kwa vyombo vya habari mtandaoni, zikiwemo TV za mtandaoni na blogs.

Kibanda anasema kazi zilizozingatia misingi ya uandishi wa habari zilionekana kutokana na ushirikiano ndani ya chombo cha habari.

Jennifer anasema baadhi ya habari hazikuwa na ujumuishi na kuegemea upande mmoja bila kutoa haki ya kusikika, kwa kuwa walipelekwa kwenye eneo la tukio na taasisi fulani.

**Habari kuathiri jamii**

Jaji Kiongozi Halima anasema moja ya kigezo walichoangazia ni namna habari ilivyoleta matokeo kwenye jamii, na sio kuelezea bila kusisimua na kusukuma hatua kuchukuliwa.

Mkumbwa anasema: "Bado kuna udhaifu mkubwa kwenye uwezo wa kuathiri jamii. Kazi chache zilisababisha mabadiliko lakini hazikuhusu masuala muhimu zaidi kwa jamii."

Dk. Mkoko alisema uwezo wa habari kuathiri jamii vilijitokeza zaidi kwenye magazeti na runinga, ambazo walionyesha moja kwa moja namna hatua zilivyochukuliwa mara baada ya habari husika kuandikwa.

"Kuna kazi zilizozaa matokeo, mfano suala la udumavu Njombe, hadi Makamu wa Rais alikwenda, na Rais anazungumzia udumavu, hii ndiyo kazi ya uandishi wa habari. Nyingine zimeshinda na nyingine hazikushinda ila mamlaka zilichukua hatua," alisema.

Jennifer alisema kazi nyingi zilikosa matokeo kwa kuwa wengi hawakuandika habari kwa kina kuhusiana na Loliondo, Ngorongoro na DP World na kuishia kuandika habari za viongozi pekee.

**Teknolojia**

Kwa mujibu wa Dkt. Mkoko ubunifu na tekonolojia bado ni tatizo kwa kuwa wengi hawajaweza kulionyesha jambo hilo.

Kibanda anasema aliona kazi za TBC1 kwenye Safari Channel ambazo zilipigwa kwa ndege zisizo na rubani (drone), hali inayoonyesha ukuaji wa

tekinolojia, pia kamera za kisasa, nao pia Pangani FM walitumia vifaa vya kisasa kufanya kazi.

“Bado tupo kipindi cha mpito kupokea *new media*, ni lazima tujifunze namna ya kuwamudu walaji tofauti. Tunasema magazeti yamekufa ila kupitia mashindano haya nimebaini kuna maudhui mazuri sana kwenye magazeti. Tunaamini wasomaji wataanza kurudi,” anasema Kibanda.

Mkumbwa anasema ubunifu na matumizi ya tekonolojia vilionekana kwa uchache kwa vyombo vya mtandaoni na baadhi kwenye magazeti, na kwamba juhudi zaidi zinahitajika.

**Mvutano wa majaji**

Kibanda anasema kuna nyakati walibishana na kuamua kwa kura, kwa kuwa kuna kazi baadhi waliamini zimefikia vigezo na wengine waliona zilipwaya.

Naye Jennifer anasema kuna nyakati majaji walikubaliana na kutokukubaliana, lakini walisimama kwenye vigezo, pamoja na kukumbuka viapo kwa kutumia vitabu vyao vitakatifu.


Aidha, Mkumbwa anasema Baraza la Habari Tanzania (MCT) wamefanya vyema kufuatilia kazi muhimu ambazo hazikukusanywa mfano DP World, Ngorongoro na maporomoko ya Hanang’. “Bahati mbaya hatukuona kazi *outstanding* (zenye ubora). Mwanzo ni mzuri. Lengo ni kuwa na kazi nzuri hata kama mwenyewe hakuileta.”



Bi. Halima Shariff
**Jaji Kiongozi**



Dkt. Egbert Mkoko
**Jaji**



Bw. Mkumbwa Ally
**Jaji**



Bi. Msellem Halima Issa
**Jaji**



Bi. Jennifer Sumi
**Jaji**



Bi. Eshe Muhiddin Hussein
**Jaji**



Bw. Absalom Norman Kibanda
**Jaji**

# Jipange kufurahia simulizi bomba toleo lijalo:

1. **Alichoandika mshindi wa jumla:** Toleo lijalo tutakuletea ushahidi wa habari ya mshindi wa jumla iliyopelekea mamlaka kuchukua hatua.
2. **Kishindo:** Tunakuandalia simulizi ya kusisimua ya kijana aliyefukuzwa shuleni kwa kukosa viatu. Badala ya kukata tamaa, alijitosa katika kazi mbalimbali kama uvuvi na ukondakta wa daladala. Hatimaye, aliamua kuingia kwenye kilimo cha nyanya, ambacho kimebadilisha maisha yake na ya familia yake.
3. **Je, Wajua?** Umewahi kujiunga na SACCOS au umesikia kuhusu SACCOS? Unajua chimbuko lake? Unajua upo salama kiasi gani na nani anayekuhakikishia usalama wa pesa zako katika SACCOS? Unajua ni mabilioni ya shilingi kiasi gani yamewekezwa katika SACCOS? na uwekezaji umejikita katika miradi gani? Usikose toleo lijalo la Jarida la Tuzo lililosheheni historia ya ushirika kupitia SACCOS na jinsi usimamizi thabiti unavyogusa na kubadilisha maisha ya Watanzania.
4. **Mahiri:** Utakutana na mwandishi mahiri wa habari za uchunguzi, ambaye anajulikana kwa ujasiri na uthubutu wake katika kufuatilia habari za uchunguzi. Moja ya habari yake ambayo imemfanya kuwa maarufu na imempatia tuzo, inahusu madarasa yaliyoezekwa kwa nyasi. Habari hii ilisababisha madarasa hayo kubomolewa na kujengwa upya kwa vifaa vya kisasa.
5. **Gwiji wa Habari:** Utaburudika na stori ya mwandishi wa habari maarufu wa Kitanzania anayejulikana kwa kazi yake ya uandishi wa habari na utangazaji. Amewahi kuendesha mijadala ya kisiasa na masuala ya kijamii kwa ustadi wa hali ya juu. Anajulikana kwa uchambuzi na ufahamu wa kina juu ya siasa na masuala ya kijamii nchini Tanzania. Ni nani huyo? Usikose toleo lijalo la Jarida la Tuzo.
6. **Anayeinukia:** Je wazazi wako walitaka uwe nani? Katika toleo lijalo utasoma simulizi ya mwandishi wa habari chipukizi ambaye awali wazazi wake walipanga awe daktari bingwa, lakini ndoto nyingine iliibuka, baada ya kukosa nafasi katika vyuo vya udaktari. Akachagua uandishi wa habari ambao umeanza kumpatia mafanikio na kuwa gumzo katika hili Jarida la Tuzo.



Uzinduzi wa Jarida la Tuzo la kwanza














# Usiku wa EJAT katika picha

Picha zote na  Mwanzo Millinga.

Ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar Es Salaam, ulipambwa kwa mabango, zulia jekundu na waalikwa wengi walitambua thamani na tukio hilo adhimu kwa kuvaa mavazi rasmi na ya heshima. Ukumbi ulikuwa umetamalaki suti za kila mtindo, magauni na vilemba vyake. Kwa ujumla, sherehe za 15 za EJAT (2023), kwa mara ya kwanza, zilikuwa za tofauti.







## Maelezo ya Picha

1. Washindi wote wa EJAT 2023
2. Mgeni rasmi, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu, akitoa hotuba na salamu za Spika wa Bunge hilo, Dkt. Tulia Ackson, ambaye alimuwakilisha.
3. Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura (kushoto), akimpongeza Naibu Spika, Mhe. Mussa Azzan Zungu, baada ya kuhutubia waalikwa.
4. Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura, akitoa maelezo ya ufunguzi na salamu za ukaribisho kwa waalikwa wote.
5. Mwandishi Imma Rashid Mbuguni wa Majira Online, akionesha tuzo yake ya Kundi la Wazi.
6. Rais wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji Bernard Luanda, akifuatilia ratiba ya usiku wa EJAT.
7. Mtangazaji wa zamani wa Redio Tanzania, Bi. Edda Sanga, akimtangaza mmoja wa washindi wa EJAT 2023.



EJAT
The 15th Excellence in Jo
MARIE STOPES
TAIFA
8




9




EJAT
MARIE STOPES
TAIFA
11




Tanzania (EJAT)
10




Tanzania (EJAT)
12



13



14



15

# Maelezo ya Picha

8. Mshindi wa Jumla wa EJAT 2023, Mukrim Mohamed, akitoa neno la shukrani baada ya kutangazwa na kukabidhiwa tuzo yake. Kushoto, ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura.
9. Zourha John Malisa, mwandishi wa Gazeti la Mwananchi, mshindi wa tuzo ya uandishi habari za afya ya uzazi.
10. Veronica Natalis Mataba, mtangazaji wa redio ya DW Swahili, akipokea tuzo ya uandishi wa habari za Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji, kutoka kwa Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Bi. Beatrice Bandawe.
11. Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura (kulia) katika mjadala na Mwendesha sherehe Taji Liundi (kushoto) na Mhariri wa Uzalishaji wa Jarida la TUZO, Josephati Mwanzi.
12. Waandishi Stephen Mzinga na Rodgers Peter Simon, wote wa ITV, wakipokea tuzo ya pamoja ya uanshi wa habari za Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora, kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari Maelezo, Bi. Zamaradi Kawawa Zamaradi Kawawa.
13. Hamis Makungu Hamis, wa Pangani FM, katika mwitikio wa hisia baada ya kutangazwa mshindi wa Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi.
14. Mwandishi na mtangazaji wa TBC1, Irene Tumpe Mwakalinga, akipokea tuzo yake ya Habari za Jinsia na Watoto kutoka kwa Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), Bw. John Chikomo.
15. “Kwa mara ya kwanza,”EJAT 2023 ilikuwa na kiwamba cha kudokeza majina na kuonesha kazi za waandishi zilizoshinda.

# EJAT 2023 ilivyovunja rekodi zake

UMRI wa miaka 15 si haba. Kwa mtoto mwenye umri huo wazazi wanaanza kuwa na matumaini kwamba atavuka muda si mrefu, kwa sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ya Tanzania, wenye umri huo unawaruhusu kuanza familia. Naam, ni hatua. Ukitafakari umri huo hakika huwezi kuchukulia kirahisi Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) ambayo sasa zimefikisha miaka 15, miongo mmoja na nusu.

Jumamosi ya Septemba 28, mwaka 2024, katika Ukumbi Aga Khan Diamond Jubilee, sherehe za Tuzo za EJAT 2023 zilifanyika, ukumbi huu uliopo maeneo ya Upanga, jijini Dar es Salaam, ulikuwa kitovu cha shamrashamra ambazo ziliwakusanya waandishi wa habari wa Tanzania kutoka kila kona ya nchi, Bara na Visiwani.

Mwalikwa yeyote ambaye aliwasili katika ukumbi huo, kwanza akipokewa na mabango makubwa yaliyokuwa yamepamba sherehe hizo yakitambulisha uwapo wa tukio hilo adhimu kwa wanahabari nchini. Mabango hayo mbali ya kutambulisha kwamba tuzo hizo za mwaka wa 15 mfululizo tangu ziasisiwe mwaka 2009, pia yalitambulisha wadau mbalimbali ambao walijitoa kwa hali na mali kufanikisha sherehe hizo. Sherehe hizi sasa zimekuwa ni kalenda ya kudumu kwa tasnia ya habari nchini kwani huwakutanisha waandishi kila mwaka kushuhudia kazi bora za kihabari zilizofanywa kwa mwaka husika.

Zulia jekundu nalo lilikuwa linakaribisha waalikwa, huku eneo la mlango mkuu kukiwa kumepambwa mahususi kwa ajili ya washiriki, washindani na wabeba tuzo kupata picha za kumbukumbu ya tukio hilo muhimu katika kuandika historia yao katika taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Tofauti na miaka ya nyuma, tuzo za mwaka huu zilikuwa na mambo ya kushangaza (surprises). Kwanza ni idadi ya kazi zilizowasilishwa ambayo ilivunja rekodi ya miaka ya nyuma, zikiongezeka kutoka kazi 893 zilizowasilishwa mwaka 2022 hadi kazi 1,135 mwaka 2023; kikubwa zaidi kilichoshuhudiwa ni vyombo vya habari vya mikoani kuchangamkia fursa kwa wingi zaidi. Siyo tu viliwasilisha kazi bora kwa mujibu wa majaji wa EJAT 2023, bali pia vilishinda tuzo kadhaa. Mshangao mwingine ulikuwa ni idadi ya kazi bora kutoka Zanzibar, hazikuwa bora tu kwani mshindi wa jumla safari hii ametoka Zanzibar na kuvunja mwiko wa miaka 14 ambao washindi wa jumla walikuwa wanatoka Tanzania Bara tu. Mshindi wa jumla ni Mukrim Mohammed Khamis wa KTV TZ Tanzania.

Mshangao haukuwa mshindi kutoka Zanzibar tu kwa mara ya kwanza, kulikuwa na mishangao mingine miwili kutoka visiwani, mosi, kupatikana kwa wafadhili wengi kutoka visiwani kuliko miaka ya nyuma ambako ilikuwa kazi ngumu kuwapata. Pili, mshindi wa jumla kutoka Zanzibar pia alivunja rekodi ya chombo cha habari cha mtandaoni kutoa mshindi wa jumla kwa mara ya kwanza. Mwelekeo huu mpya unaacha somo na swali gumu kwa vyombo vya habari rasmi kama magazeti, runinga na redio juu ya hatma ya uandishi wa habari nchini.

Sherehe za Tuzo hizo zilizorushwa moja kwa moja na vituo vitatu vya runinga, TBC1, Channel 10 na UTV bila kusahau runinga za mitandoni, zilijawa na sura za kupendeza zenye bashasha za waandishi wa habari. Hakika waandishi waliohudhuria sherehe hizi 'walivunja makabati yao', ni dhadhiri waandishi walizingatia maelekezo ya uvaaji kwenye shughuli hiyo kwani kila mwalikwa alitarajiwa awe amevalia vazi rasmi.

Ni hakika ukumbi uliokuwa umepambwa vema, kwa mabango, mapambo na zulia jekundu, haukufanyiwa masikhara na waalikwa wengi, kwani kila mmoja alitambua thamani na tukio hilo adhimu hivyo akajitahidi kuvaa vazi rasmi tena la heshima. Ukumbi ulikuwa umetamalaki suti za kila mtindo, magauni ya heshima na vilemba

vyake. Kwa mavazi tu, sherehe za EJAT 2023 ziliheshimishwa.

Baraza la Habari Tanzania (MCT) ambao ndiyo taasisi kiongozi ya uandaaji wa tuzo hizi kila mwaka kwa niaba ya taasisi nyingine za kihabari nchini, nao walivunja rekodi yao katika kuzingatia ratiba na muda uliopangwa. MCT walivunja ule utamaduni unaodaiwa ni wa Waafrika wa kutokuzingatia muda. Kadi za mwaliko zilijieleza vema kabisa kwamba sherehe zingeanza saa 10:00 jioni, waandaji walikuwako ukumbini kwa wakati, ingawa hawakuanza juu ya alama, hawakuvuka dakika 20 baada ya muda uliopangwa kuanza kwa sherehe hizo, pia rekodi nyingine iliwekwa ambayo ni kumaliza shughuli zote za tuzo ilipofika saa 2:00 usiku. Kwa miaka kadhaa sasa sherehe hizi zimekuwa zinaanza usiku na kumalizika usiku mwingi.

Kitendo cha kuanza kwa ratiba kwa wakati, kiliwapiga butwaa baadhi ya waalikwa, hasa kutoka kundi la wafadhili wa tuzo za EJAT 2023 na wale waliokuwa wamepangwa rasmi kwa ajili ya kutoa tuzo kwa washindi. Kuchelewa huku kulisababisha baadhi ya wafadhili kushindwa kupokea vyeti vyao vya shukrani kutoka kwa mgeni rasmi, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu ambaye alimuwakilisha Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Zungu alikuwa na ujumbe wake wa kutia moyo waandishi, aliwataka wawasilishe mapendekezo yao serikalini juu ya kuwapo kwa sheria kandamizi dhidi ya uhuru wa habari, ili Bunge izirekebishe. Alisema ni nia ya Bunge kujenga mazingira wezeshi ambayo yatawasaidia waandishi wa habari kufanya kazi kwa weledi.

Hotuba ya Halima Sharif ambaye alikuwa Jaji Kiongozi wa jopo la majaji waliojifungia kwa siku 10 kupitia kazi zilizowasilishwa, ilikuwa na marudio ya miaka yote juu ya hadhi ya uandishi wa habari nchini. Kwamba ubora wa kazi nyingi ulikuwa wa kiwango cha chini. Pengine kombora hili ambalo limekuwa likirudiwa mwaka baada ya mwaka lilikuwa ni la wahariri kwa sababu ndiyo walezi wa kuwajengea uwezo wandishi, ambao pia kazi zote hupita katika mikono yao. Ni bahati mbaya, wahariri wengi hawakuhudhuria sherehe hizo. Huenda ujumbe huu ambao ungewafaa, ulipita na kuacha udhaifu uendelee kama ilivyo sasa mwaka baada ya mwaka.

Sherehe za EJAT 2023 zilijaa ubunifu pia, kwanza ni matumizi ya tekinolojia ya kidijitali kwa kuandaa mapema njia ya kudokeza majina ya washindani wa tuzo kwa kila kundi, ambao walikuwa wanasomwa kidijitali, hivyo kuongeza vionjo kwa uendeshaji wa sherehe za tuzo za mwaka huu.

Ubunifu mwingine ni kuandaliwa kwa Jarida la TUZO, ambalo sasa litakuwa likifanya rejea ya kazi zilizoshinda, ambazo zitakuwa zinaeleza yaliyo nyuma ya pazia, kuwapa fursa wafadhili mbalimbali wa tuzo kueleza mafaniko ya kazi zao katika jamii, na la muhimu zaidi kuweka kumbukumbu za tuzo.

Kuna msemo maarufu mitaani unaosema ‘kazi na dawa’, katika eneo la vyakula na vinywaji hakika Tuzo za EJAT 2023 zilifana. Ubora na umakini haukuwa kwenye utoaji wa huduma na vyakula tu, bali pia kuwapo kwa vinywaji na vyakula vya kutosha vyenye viwango. Mpangilio wa upatikanaji wa huduma hii ulikuwa wa viwango vya juu kwani waalikwa walijihudumia kuchukua chakula kwa kujinafasi.

Burudani ya muziki nayo ilikuwa na vionjo vyake, mchanganyiko wa kikundi cha ngoma za kiutamaduni na muziki wa kisasa vilipamba vema shughuli nzima, na kuwapatia waalikwa uhondo wa miondoko yote kwa ustadi mkubwa.

EJAT 2023 imeacha kumbukumbu muhimu isiyofutika, imeongeza ushindani na kufungua milango kwa ushiriki mpana zaidi wa wadau mbalimbali kwa tuzo zijazo. Kongole kwa maandalizi bora ya EJAT 2023.

# Vigezo vya Kumpata Mshindi wa Jumla wa EJAT

Majaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) walikutana kujadili na kuainisha vigezo vya umahiri ambavyo, kwa usahihi, vitatumika kumpata mshindi wa jumla wa EJAT. Majadiliano kuhusu vigezo hivi yalijengwa katika msingi wa uchambuzi wa vigezo vya awali na kwa kuzingatia maendeleo na mabadiliko ya Tasnia ya habari, yanayojidhihirisha katika maendeleo ya teknolojia na matarajio ya jamii yanayobadilika.

Majaji wanaamini kwamba vigezo hivi vitatoa mchango madhubuti katika kumtambua na kumtuza mshindi wa jumla wa EJAT (2023) (Mwandishi wa Mwaka) ambaye atakuwa na mchango mkubwa katika kuielimisha na kuishirikisha jamii. Kwa ujumla, kazi ya kiuandishi ya mshindi wa jumla inapaswa kuakisi viwango vya juu vya weledi katika mambo mtambuka, kuanzia ubora na athari hadi maadili na ubunifu.

**Utaratibu:**

**Hatua ya 1:** Orodha ya washindi wote pamoja na wastani wa alama kutoka katika kila kundi.

**Hatua ya 2:** Chagua washindi walioshinda zaidi katika makundi mbalimbali.

**Hatua ya 3:** Chagua washindi matatu walioshinda zaidi ambao alama zao ni za juu zaidi.

**Hatua ya 4:** Tumia vigezo vilivyokubaliwa hapo chini kufanya uamuzi wa mwisho wa kumpata mshindi wa jumla au mwandishi wa mwaka wa EJAT (2023).

| Na. | Vigezo | Alama ya Juu | Alama Aliyopata |
|---|---|---|---|
| 1. | **Wastani wa juu wa ushindi:** Wastani wa alama uliokokotolewa kutoka kwa washindi tarajiwa wote katika makundi yote. | **10** | |
| 2. | **Kiwango cha Utafiti na Uchunguzi:** Habari zina akisi uasili, utafiti wa kina, pamoja na ushahidi wa uchunguzi asili au uandishi. Matokeo dhahiri ya uchunguzi yanadhihirisha uwezo wa kuibua taarifa mpya na muhimu kama kigezo cha umahiri. | 15 | |
| 3. | **Umuhimu na Manufaa kwa Jamii:** Habari zinazoelezea mambo ambayo yana umuhimu na yanayohusu umma. Zina athari dhahiri, zinashawishi maoni ya umma, zinasukuma mabadiliko ya sera au kumulika masuala mahsusi ya jamii. Habari yapasa iwasilishe matukio ya sasa katika muktadha mpana ili kuisaidia hadhira kuelewa umuhimu wake. | 15 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | **Uwazi, Ushirikishaji na Ubunifu**: Habari lazima ziwe wazi, zenye mvuto na kuishirikisha hadhira kuanzia mwanzo hadi mwisho. Zinapasa zitumie ubunifu kwa kutumia mbinu bunifu za masimulizi, miundo anuwai, au mielekeo tofauti. | 10 | |
| 5. | **Viwango vya Maadili:** Habari lazima ziendane na viwango vya maadili, ambavyo vinajumuisha usahihi, haki, muda, kujali faragha, kuzuia mgongano wa maslahi na uwazi wa vyanzo vya taarifa, uwajibikaji na uandishi unaojali. | 15 | |
| 6. | Umahiri wa Kiufundi: Habari iwe katika kuandika, picha jongefu, sauti au mchanganyiko wa sauti na taswira, ubora wa ufundi unapaswa kuwa katika kiwango cha juu cha weledi, kinachoboresha zaidi badala ya kuvuruga maudhui. Habari zinapasa kujumuisha mifumo anuwai ya taarifa (maandishi, picha jongefu, sauti, na mchanganyiko wa taswira, takwimu na michoro). | 10 | |
| 7. | **Ujasiri na Uadilifu:** Kumtambua mshindi wa jumla ambaye anaripoti katika mada ngumu au hatari, daima katika kiwango binafsi au kitaaluma na bado akawa amejizatiti katika ukweli, uadilifu wa kiuandishi hata kama yupo katika changamoto au upinzani. | 10 | |
| 8. | Uwajibikaji: Kumtambua mshindi wa jumla ambaye anawajibika kwa kazi au uandishi wake, anajenga kuaminika na analekea kuaminika kwa vyombo vya habari mbele ya hadhira. Uandishi unaolenga kuwawajibisha wenye mamlaka na watawala. | 15 | |
| | **Jumla ya alama:** | 100 | |

Majaji wote wamekubaliana kwamba vigezo hivi vitumike katika kumpata mshindi wa jumla wa EJAT (2023).

**Jaji Kiongozi** (Jina): Halima Shariff

**Saini**:

**Tarehe:** 07/9/2024

**Katibu Mtendaji wa MCT**: Ernest Sungura

**Saini:**

**Tarehe:** 07/9/2024

# VIGEZO VYA KUTATHMINI HABARI SHINDANI

Majaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) walikutana kujadili na kuainisha vigezo vya umahiri ambavyo vitatumika kutathmini habari zinazoshindanishwa katika vyombo mbalimbali vya habari: redio, runinga, magazeti, na majukwaa ya mtandaoni. Majadiliano kuhusu vigezo hivi yalijengwa katika msingi wa uchambuzi wa vigezo vya awali na kwa kuzingatia maendeleo na mabadiliko ya tasnia ya uandishi wa habari, yanayojidhihirisha katika maendeleo ya teknolojia na matarajio ya jamii yanayobadilika.

Majaji wote wanaamini kwamba vigezo hivi vilivyokubalika vitatoa mchango madhubuti katika kutathmini habari shindani kutoka vyombo mbalimbali vya habari. EJAT inalenga kuwatambua na kuwatuza waandishi mahiri wenye mchango kwa jamii kuwa na uelewa na ushiriki katika mambo yanayoihusu, kwa kuwekea mkazo usahihi, haki, ubunifu, athari kwa jamii, na maadili. Vigezo vilivyokubalika ni hivi vifuatavyo:

## Vigezo kwa ajili ya habari za runinga

| Na. | Vigezo | Alama | Alama Aliyopata |
|---|---|---|---|
| 1. | **Uwazi na Mtindo:** Kuandika na/au mbinu za masimulizi (inajumuisha ubora wa uandishi, ushirikishaji na athari za kihisia, uwasilishaji dhahiri, mvuto/umakini. | 10 | |
| 2. | **Nguvu ya Kuripoti:** (inajumuisha marejeo ya taarifa zilizokusanywa, wigo wa utafiti au idadi ya vyanzo vya taarifa, utimilifu wa kuripoti, taarifa mpya, na maelezo ya kweli. | 10 | |
| 3. | Inachangia/inatoa maarifa mapya na uelewa wa mambo anuwai kwa mtazamaji. | 10 | |
| 4. | Inashikamana na viwango vya uandishi na maadili - ukweli, usahihi, usawa, na haki. Utofauti wa wazi kati ya ukweli na maoni. | 10 | |
| 5. | Habari inahusu jambo lenye umuhimu kwa umma/maslahi ya binadamu/ inasongesha ajenda za kitaifa. | 10 | |
| 6. | Uhalisi, uvumbuzi na ubunifu. Habari ya kweli na ya kipekee ni ile inayoibua taarifa mpya. Inapasa kuchunguza jambo jipya, inaibua wazo halisi; uvumbuzi na inayoonesha maana au ubunifu. | 10 | |
| 7. | Maadili ya kipekee na ubora katika uzalishaji wa maudhui. Habari au vipindi vya runinga vyenye viwango vya kushindanishwa vinatokana na viwango vya juu vya uzalishaji. Hii inajumuisha vitu kama: ubora wa taswira (HD), sauti, ubunifu na nyongeza ya vionjo. | 10 | |
| 8. | Nguvu ya masimulizi na muundo wa uwasilishaji. Masimulizi yaliyopangiliwa. Kuwe na urari wenye mwanzo, kati, na mwisho, wenye azimio pamoja na muundo mzuri wa uwasilishaji. | 10 | |
| 9. | Maarifa, uchambuzi, au uchunguzi wa muktadha wa habari. (Maswali: Kwa nini? Na jinsi gani? Ya upande wa pili wa habari). | 10 | |
| 10. | Inaibua jambo lililofichika au lisilo la kawaida. Kiwango cha maarifa ya utafiti na uchunguzi. | 10 | |
| | **JUMLA** | **100** | |

## Vigezo kwa ajili ya habari za magazeti

| Na. | Vigezo | Alama | Alama Aliyopata |
|---|---|---|---|
| 1. | Kusomeka, uwazi na muundo. Kuandika na/au mbinu za masimulizi (inajumuisha: ubora wa uandishi, ushirikishaji na athari za kihisia, uwasilishaji dhahiri, mvuto/ umakini. | 10 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | **Nguvu ya Kuripoti:** (inajumuisha idadi ya marejeo ya taarifa zilizokusanywa, wigo wa utafiti au idadi ya vyanzo vya taarifa, utimilifu wa kuripoti, taarifa mpya, na maelezo ya kweli. | 10 | |
| 3. | Inachangia/inatoa maarifa mapya na uelewa wa mambo anuwai kwa msomaji. | 10 | |
| 4. | Inashikamana na viwango vya uandishi na maadili - ukweli, usahihi, usawa, na haki. Utofauti wa wazi kati ya ukweli na maoni. | 10 | |
| 5. | Umuhimu na athari kwa umma au faida zitokanazo na habari husika. Mada/ thamani ya habari/umuhimu. Habari inahusu jambo lenye umuhimu kwa umma/ faida kwa binadamu. Inasongesha ajenda ya jamii au umuhimu wa kitaifa. | 10 | |
| 6. | **Uhalisia**: (hii inajumuisha: uhalisia wa wazo, na/au umuhimu wake, uhalisia wa jambo, uhalisia wa kiutendaji, bidii, taarifa yenye mshangazo, na mada ya kuvutia. | 10 | |
| 7. | Habari au makala ina uwakilishi mpana wa sauti za watu tofauti ikijumuisha watu maarufu na wa makundi maalum kama wanawake, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu. | 10 | |
| 8. | Ubora wa mbinu za kuhoji na mahojiano, uwasilishaji na usahihi wa lugha. | 10 | |
| 9. | Maarifa, uchambuzi, au uchunguzi wa muktadha wa habari. (Maswali: Kwa nini? na jinsi gani? Ya upande wa pili wa habari). | 10 | |
| 10. | Inaibua jambo lililofichika au lisilo la kawaida. Kiwango cha maarifa ya utafiti na uchunguzi. | 10 | |
| | **JUMLA** | **100** | |

## Vigezo kwa ajili ya habari za redio

| Na. | **Vigezo** | **Alama** | **Alama Aliyopata** |
|---|---|---|---|
| 1. | **Uwazi na Mtindo:** Kuandika na/au mbinu za masimulizi (inajumuisha ubora wa uandishi, ushirikishaji na athari za kihisia, uwasilishaji dhahiri, mvuto/umakini. | 10 | |
| 2. | **Nguvu ya Kuripoti:** (inajumuisha idadi ya marejeo ya taarifa zilizokusanywa, wigo wa utafiti au idadi ya vyanzo vya taarifa, utimilifu wa kuripoti, taarifa mpya, na maelezo ya kweli. | 10 | |
| 3. | Inachangia/inatoa maarifa mapya na uelewa wa mambo anuwai kwa msikilizaji. | 10 | |
| 4. | Inashikamana na viwango vya uandishi na maadili - ukweli, usahihi, usawa, na haki. Utofauti wa wazi kati ya ukweli na maoni. | 10 | |
| 5. | Habari inahusu jambo lenye umuhimu kwa umma/maslahi ya binadamu/ inasongesha ajenda za kitaifa. | 10 | |
| 6. | **Uhalisia**: (hii inajumuisha uhalisia wa wazo, na/au umuhimu wake, uhalisia wa jambo, uhalisia wa kiutendaji, bidii, taarifa yenye mshangazo, na mada ya kuvutia. | 10 | |
| 7. | Habari au kipindi kina uwakilishi mpana wa sauti za watu tofauti ikijumuisha watu maarufu, na wasio na sauti, wa makundi maalum kama wanawake, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu. | 10 | |
| 8. | Ubora wa uwasilishaji wa kipindi. Ubora wa sauti, masimulizi mujarabu, ubunifu, muundo au werevu, na ustadi wa mtangazaji. | 10 | |
| 9. | Maarifa, uchambuzi, au uchunguzi wa muktadha wa habari. (Maswali: Kwa nini? na jinsi gani? Ya upande wa pili wa habari). | 10 | |
| 10. | Inaibua jambo lililofichika au lisilo la kawaida. Kiwango cha maarifa ya utafiti na uchunguzi. | 10 | |
| | **JUMLA** | **100** | |

## Vigezo vya habari za mtandaoni

| Na. | **Vigezo** | **Alama** | **Alama Aliyopata** |
|---|---|---|---|
| 1. | Habari ya mtandaoni inapasa kuonesha umahiri wa kiufundi, taswira na umahiri kiuandishi, pia ujuzi katika kurekodi nyakati muhimu na zinazovutia, kuacha alama za kihisia kwa hadhira. | 15 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Habari ya mtandaoni inapasa kudhihirisha ubunifu, matumizi ya mitindo tofauti (kama vile: sauti, picha jongefu, michoro, picha, viunganishi, n.k.), katika kusimulia habari vizuri. | 20 | |
| 3. | Inapasa kudhihirisha muunganiko wa umahiri katika maudhui na uzoefu wa mtumiaji, pamoja na thamani kwa hadhira. | 10 | |
| 4. | Maudhui ya mtandaoni yanapaswa kutoa maarifa mapya, ubunifu, na uelewa wa jambo muhimu/mada kwa hadhira. | 10 | |
| 5. | Inapasa kutoa usomaji jumuishi kwa wanaoingia katika jukwaa husika. Inashikamana na viwango vya uandishi wa habari na maadili – uhalisia, isiyochukuliwa kutoka katika maeneo yaliyozuiliwa kisheria, isiyo na maudhui yasiyofaa, isiyofinyangwa kidijiti. | 20 | |
| 6. | Maudhui ya mtandaoni yanapaswa kuwa na umuhimu, yenye athari chanya na faida kwa umma au jamii, na thamani ya habari. | 10 | |
| 7. | Inapaswa kuwepo na fikra za uwiano unaofaa wa maandishi/sauti au picha jongefu kwa majukwaa maalum ya mtandaoni (kwa mfano: X (zamani Twitter), Instagram, FaceBook na YouTube). | 10 | |
| 8. | Inapaswa kuwa na fikra mahsusi za matumizi sahihi ya lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza. | 5 | |
| | **JUMLA** | **100** | |

## Vigezo vya habari za uchunguzi

| Na. | **Vigezo** | **Alama** | **Alama Aliyopata** |
|---|---|---|---|
| 1. | Habari ya uchunguzi inapasa kusomeka na kutokana na vyanzo vya uhakika vya taarifa. Uwazi na muundo. Uandishi na/au mbinu za masimulizi (yanayojumuisha ubora wa uandishi, ushirikishwaji na athari za kihisia, uwasilishaji dhahiri, kuvutia na umakini. | 10 | |
| 2. | Habari zieleze kilicho tokea: ieleze nini, na kwa nini hadhira ijali? Nguvu ya kuripoti (inayojumuisha marejeo ya taarifa zilizokusanywa, wigo wa utafiti au idadi ya vyanzo vya taarifa, utimilifu wa kuripoti, taarifa mpya, na maelezo ya kweli. | 10 | |
| 3. | Habari ya uchunguzi inapasa kutambua chanzo cha tatizo na kupendekeza au kuainisha /gundua uhusiano. Inatoa maarifa mapya na uelewa wa jambo/mambo kwa hadhira. | 10 | |
| 4. | Habari inapasa kueleza kama kuna viashiria vya hatari, au uwezekano wa kuwepo/kutokea - mahali pengine tena. Inashikamana na viwango vya uandishi wa habari, maadili - ukweli, usahihi, usawa, na haki. Kuwe na tofauti ya wazi kati ya ukweli na maoni. | 10 | |
| 5. | Habari inapasa iseme nani alifanya hiyo, alifanyaje, athari zake ni nini, na inawezaje kuwekwa sawa/kurekebishwa? Habari iwe ni ya jambo muhimu kwa umma/umuhimu kwa binadamu/inayosongesha ajenda yenye maslahi kwa taifa. | 5 | |
| 6. | Habari ya uchunguzi inapasa iseme iwapo matokeo yaliyopatikana yalitelekezwa kwa makusudi. Uhalisia (hii inajumuisha: uhalisia wa wazo, na/au umuhimu wake, uhalisia wa jambo, uhalisia wa kiutendaji, bidii, taarifa yenye mshangazo, na mada ya kuvutia. | 10 | |
| 7. | Habari ya uchunguzi inapasa kuanisha: Nini kilikwenda mrama? Nini kilisababisha kiende mrama? Kwa nini kilienda mrama? Athari zake ni nini na inawezekanaje kurekebishwa/kuwekwa sawa? Je, habari imehusisha sauti za watu tofauti zinazojumuisha watu maarufu na wasio na sauti kama wanawake, watoto, wanaume, wazee na watu wenye ulemavu. | 5 | |
| 8. | Habari ya uchunguzi inapasa iweke umuhimu kwamba, kwa kuandikwa kwake nani atanufaika na nani ataumia? Ubora wa habari/uwasilishaji wa kipindi. Mtindo na usanifu, ubunifu, werevu, na mbinu za sauti na masimulizi. | 10 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Habari ya uchunguzi inapasa ieleze kwa uwazi ni nani ambaye habari hiyo inamkosoa au kumwajibisha? Maarifa, uchambuzi, na uchunguzi wa muktadha wa habari husika. Maswali kama “Kwa nini?” na “Jinsi/Namna gani?” ya upande wa pili wa habari. | 10 | |
| 10. | Habari ya uchunguzi inapasa ihusu mambo muhimu, iainishe makosa ya kimfumo au mchakato unaoweza kuibua mambo ambayo hayakujulikana kabla, na kusababisha mdahalo kuhusu maadili au tabia. Inaibua jambo lililofichika au lisilo la kawaida. Maarifa/ujuzi wa uchunguzi na utafiti vilivyotumika. | 10 | |
| 11 | Vyanzo vya habari havipaswi tu kuwa sahihi bali vinapaswa kutajwa, labda iwapo kuna ulazima wa kutovitaja – na iwe kwa kwa ajili ya usalama wao, au kama hawapendi watajwe. | 10 | |

## Muhtasari wa vigezo vya jumla

| Na. | **Vigezo** | **Alama** | **Alama Aliyopata** |
|---|---|---|---|
| 1. | Uhalisia: Wazo na mada vinaibua uhalisia wa fikra/kufikiri. | 10 | |
| 2. | Kushikamana na viwango vya uandishi wa habari: Miongozo ya kiweledi, maadili, desturi za kitaifa, mila na mifumo ya kisheria. | 10 | |
| 3. | Mawanda na kina cha kuripoti na utafiti: Majibu kwa maswali matano muhimu: Nani? Nini? Kwa nini? Lini? Wapi? na Jinsi/namna gani? | 10 | |
| 4. | Vyanzo mbalimbali na stahiki vya taarifa: Ijumuishe vyanzo vya msingi na vya upili, wakati wote ikiwezekana. | 10 | |
| 5. | Jambo linaloendana na muhimu: Kwa umma na linalosongesha ajenda ya taifa. | 10 | |
| 6. | Ubora wa kazi: Uwazi, ubunifu na uwasilishaji unaovutia. | 10 | |
| 7. | Ujuzi wa kuhoji: Hojaji zinaibua taarifa muhimu zinazoongeza thamani ya jambo/mada na muktadha. | 10 | |
| 8. | Inatoa/kuchangia maarifa mapya: Inahoji, inaelimisha na kuburudisha. | 10 | |
| 9. | Umahiri katika kazi na taaluma: Lugha, ubunifu na miundo ya mawasilisho ya sauti na picha jongefu. | 10 | |
| 10. | Athari na faida kwa umma: Inaibua mwitikio, mabadiliko na suluhisho. | 10 | |
| | **JUMLA** | **100** | |

Majaji wote wamekubaliana kwamba vigezo hivi vitumike katika kuwapata washindi wa EJAT (2023).

**Jaji Kiongozi** (Jina): Halima Shariff

**Saini**:

**Tarehe:** 07/9/2024

**Katibu Mtendaji wa MCT**: ERNEST SUNGURA

**Saini:**

**Tarehe:** 07/9/2024

VIDEO AUDIO PHOTO WEB

# ORODHA YA WASHINDI

| NA | WASHINDI | JINSIA | CHOMBO CHA HABARI | KUNDI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Haika E. Kimaro | Mwanamke | The Citizen | Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo - Mtandaoni |
| 2 | Anna Peter Mbuthu | Mwanamke | TBC | Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo - TV |
| 3 | Waryoba Musa Waryoba | Mwanaume | Montessorry Tanzania | Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo - Magazeti |
| 4 | Esau Ezra Ng'umbi | Mwanaume | Nukta Habari | Uandishi wa Habari za Mafuta, Gesi na Uchimbaji Madini - Mtandaoni |
| 5 | Halfan Ramadhani Chusi | Mwanaume | Nipashe | Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora - Magazeti |
| 6 | Hamisi Makungu Hamisi | Mwanaume | Pangani FM | Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora – Radio |
| 7 | Benjamin Stephen Mzinga | Mwanaume | ITV | Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora -TV |
| 8 | Rodgers Peter Simon | Mwanaume | ITV | Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora -TV |
| 9 | Lukelo Francis Haule | Mwanaume | The Chanzo | Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora -Mtandaoni |
| 10 | Eliya Solomon | Mwanaume | Mwanaspoti | Uandishi wa Habari za Data -Print |
| 11 | Pamela Nasphory Chilongola | Mwanamke | Mwananchi | Uandishi wa Habari za, Biashara, Uchumi na Fedha - Print |
| 12 | Mukrim Mohamed Khamis | Mwanaume | KTV TZ Online | Uandishi wa Habari za, Biashara, Uchumi na Fedha -Mtandaoni |
| 13 | Sanula Renatus Athanas | Mwanaume | Nipashe | Uandishi wa Habari za Elimu-Magazeti |
| 14 | Huwaida Nassor Moh'd | Mwanamke | As Salaam FM | Uandishi wa Habari za Elimu-Radio |
| 15 | Benson Eustace Jacob | Mwanaume | UTV | Uandishi wa Habari za Elimu-TV |
| 16 | George Henry Helahela | Mwanaume | Mwananchi Digital | Uandishi wa Habari za Elimu - Mtandaoni |
| 17 | Zourha John Malisa | Mwanamke | Mwananchi | Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi - Magazeti |
| 18 | Said Ally Sindo | Mwanaume | Storm FM | Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi - Radio |
| 19 | Khamis Mohamed Salum | Mwanaume | Zanzibar Leo | Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto- Magazeti |
| 20 | Shekha Seif Suleiman | Mwanamke | ZBC | Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto - Radio |
| 21 | Irene Tumpe Mwakalinga | Mwanamke | TBC1 | Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto - TV |
| 22 | Zacharia Ignas Nyamoga | Mwanaume | IPC Mkombozi TV | Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto - Mtandaoni |
| 23 | Jacob Mogesi Mosenda | Mwanaume | The Citizen | Uandishi wa Habari za Uchunguzi-Magazeti |

| NA | WASHINDI | JINSIA | CHOMBO CHA HABARI | KUNDI |
|---|---|---|---|---|
| **24** | Thomas Masalu Lunyalo | Mwanaume | Mazingira FM | Uandishi wa Habari za Uchunguzi-Radio |
| **25** | Hamisi Makungu Hamisi | Mwanaume | Pangani FM | Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi-Radio |
| **26** | Margareth Msafiri. Geddy | Mwanamke | TBC Safari | Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi-TV |
| **27** | Julius Maricha Maricha | Mwanaume | The Citizen | Uandishi wa Habari za Utamaduni na Michezo-Print |
| **28** | Brown Benny Mbwawa | Mwanaume | Wasafi FM | Uandishi wa Habari za Utamaduni na Michezo-Radio |
| **29** | Fatma Abdallah Chikawe | Mwanamke | UTV | Uandishi wa Habari za Utamaduni na Michezo-TV |
| **30** | Warioba Igombe Warioba | Mwanaume | Uhuru | Uandishi wa Habari za Afya-Magazeti |
| **31** | Saa Mbwana Zumo | Mwanamke | Pangani FM | Uandishi wa Habari za Afya-Radio |
| **32** | Anna Potinus | Mwanamke | Mwananchi Digital | Uandishi wa Habari za Afya-Mtandaoni |
| **33** | Mgongo Kaitira Mafuru | Mwanaume | Mwananchi Digital | Uandishi wa Habari za Afya-Mtandaoni |
| **34** | Mohamed Hammie Rajabu | Mwanaume | Habari Leo | Uandishi wa Habari za Walemavu - Magazeti |
| **35** | Mercy Yasin Mbaya | Mwanamke | UTV | Uandishi wa Habari za Walemavu - TV |
| **36** | Julius Maricha Maricha | Mwanaume | The Citizen | Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto-Magazeti |
| **37** | Amina Deogratias Semagogwa | Mwanamke | Radio Kwizera | Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto-Radio |
| **38** | Irene Tumpe Mwakalinga | Mwanamke | TBC1 | Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto-TV |
| **39** | Hellen Nachilongo Mkisi | Mwanamke | The Citizen | Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji -Print |
| **40** | Veronica Natalis Mataba | Mwanamke | DW Swahili | Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji -Radio |
| **41** | Anna Peter Mbuthu | Mwanamke | TBC | Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji -TV |
| **42** | Mukrim Mohamed Khamis | Mwanaume | KTV TZ Online | Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji -Mtandaoni |
| **43** | Sanula Renatus Athanas | Mwanaume | Nipashe | Kundi la Wazi - Magazeti |
| **44** | Adam Gabriel Hhando | Mwanaume | CG FM | Kundi la Wazi -Radio |
| **45** | Dickson Shukran Kanyika | Mwanaume | RFA | Kundi la Wazi -TV |
| **46** | Imma Rashidi Mbuguni | Mwanaume | Majira Online | Kundi la Wazi -Mtandaoni |

MARIE STOPES TANZANIA

**HUDUMA**

- Huduma za baada ya mimba kuharibika
- Huduma na Taarifa za afya za uzazi
- Huduma za kawaida za kitabibu
- Uzazi wa Mpango
- Huduma za Kujifungua
- Huduma na Ushauri wa Afya ya Uzazi kwa Wanaume

# Tunatoa Huduma na Taarifa za Afya ya Uzazi na Uzazi wa Mpango kote Tanzania



Tupigie: **0800 753 333**

Au tuma Ujumbe mfupi kwenye namba ya WhatsApp: **0755 896 996**